**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 27 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista Mhagama) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa tunataka kufukuzana na muda na kuendana na ratiba yetu sawasawa, ninaomba matangazo yote ambayo yako kwenye meza yangu niyatoe saa nne baada ya kipindi cha Maswali na Majibu. Tunaendelea na Katibu ametuambia tunaendela na Maswali na Majibu.

Na. 88

**Muafaka wa CCM na CUF**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, muafaka wa Chama cha CCM na *CUF* ulitungiwa sheria na Barala za Wawakilishi Zanzibar na kuweka hatua 30 za utekelezaji, na moja kati ya hatua hizo haijatekelezwa, yaani kuunda Kamati ya Kudumu ya Vyama vyote yaani *Interparty Committee (IPC).*

Je, kitu gani kinachocheleweshа uundwaji wa Kamati hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya kudumu ya vyama vyote imeshaundwa kutokea tarehe 23 Julai, 2005. Kamati hii ni ya Makatibu Wakuu na itashughulikia

uundwaji wa Baraza la mashauriano ya kitaifa ambalo litakuwa linasimamia muafaka wa kitaifa wa vyama vyote baada ya Muafaka wa *CUF* na CCM kwisha muda wake tarehe 3 Septemba, 2005.

Kamati hiyo ina wajumbe saba, Mwenyekiti wake akiwa Katibu Mkuu wa CCM Mheshimiwa Philip Mangula na Katibu Mkuuu wake akiwa Katibu Mkuu wa *UPDP* Mheshimiwa Abdula Nasoro Ally. Wajumbe wengine wa Kamati hiyo ni Makatibu Wakuu kutoka Chama cha *SAU, CUF, FORD, NCCR – Mageuzi* na *TADEA.* Kamati hii bado ipo na inaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imeshakaa vikao kadhaa na kujadili mambo mbalimbali kuhusiana na kuundwa kwa Baraza la Taifa la Mashauriano la vyama vya siasa (BTMVS) ikiwa ni pamoja na kupendekeza majukumu, muundo, maadili na ofisi za Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mapendekezo ya kuundwa kwa baraza hili yameshawasilishwa Serikalini ili kupata baraka za Serikali kabla ya kuendelea na hatua ya uundwaji wa baraza hili. Serikali kwa upande wake itayashughulikia mapendekezo hayo pamoja na mambo mengine.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali moja la kwanza ni kwamba Je, muafaka utungiwa sheria na Baraza la Wawakilishi badala ya Bunge hili ni sawasawa?

Swali la pili kwa kuwa mazungumzo kati ya vyama *enter party dialogue* ni jambo muhimu sana katika *Common Wealth* na hasa Uingereza tunayo *best practice* inayotokana na mazungumzo kati ya vyama, kwa mfano Spika wa Uingereza akiwa anatoka kwenye Jimbo kama ilivyohapa inapofika wakati wa uchaguzi vyama vyote havimwekei upinzani. Swali langu ni Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba katika mazungumzo yatakayokuwa yanaendelea, vyama vikubaliane kwamba ifikapo mwaka 2010, Mheshimiwa Waziri Mkuu Lowasa na Mheshimiwa Spika Sitta, wasiwekewe wapinzani wowote wale katika majimbo yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu Baraza la Wawakilishi kutunga sheria kuhusu muafaka, hili ni sahihi kwa sababu vyama vilivyokuwa vinazozana wakati ule *CUF* na CCM na mazingira makubwa yalikuwa kule Zanzibar, na Zanzibar Baraza lililopo ni Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo ni muafaka kwao kabisa kutunga sheria ya kuweka mazingira mazuri ili maendeleo ya kisiasa kule yawe mazuri. La pili kuhusu kuwekewa wapinzani Waziri Mkuu au Spika, wakati wa uchaguzi hili ni jambo nzuri lakini ni vizuri likazungumzwa katika mazungumzo hayo yanayoendelea na hivi vyama. Kama katika mazungumzo yale wakikubaliana mimi naona hakuna kizuizi ni suala la makubaliano tu. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Je, Serikali itakuwa tayari hii *Enter Party Committee* kuiundia Sheria ya Bunge ili waweze kufanya kazi zao chini ya misingi ya kisheria.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nchi inakwenda kwa taratibu za sheria ndio maana tumefika hapa tumefanikiwa sana, kwa sababu nchi yetu mpaka hivi sasa tunakwenda vizuri kwa mujibu wa Sheria, Katiba na Kanuni tuliyojiwekea. Ni kweli alichosema na mimi naunga mkono, ni vizuri kila jambo kuliwekea sheria, lakini nafikiri ni vizuri atakubaliana na mimi tusubiri hayo mazungumzo kwanza yatakapofika mahala pakaiva wakakubaliana basi suala la kutunga sheria halina tatizo mradi kuwe na makubaliano. Lakini kama nilivyosema katika kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai ni vizuri haya hasa yakajitokeza zaidi kule kule Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi na kule ndiko ambako vizuri kukawekwa na sheria za namna hii maana ndiko kwenye mtafaruku ule ambao tumeushuhudia, nashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 89

**Posho kwa Watumishi wa Idara ya Afya**

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA** sliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wa Idara ya Afya wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kuhudumia wagonjwa, hasa wanapowahudumia wagonjwa wa magonjwa ya kuambukiza na katika mazingira ya uhaba wa watumishi ambao hulazimika wakazi mwingine kufanya kazi kwa masaa 24:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwarudishia posho za *On Call Allowance*,taaluma na mazingira magumu?

(b) Kwa kuwa Serikali mwaka 2005 iliamua kuwalipa watumishi wa afya wa Idara zote Mkoani Kigoma malimbikizo ya *On Call Allowance* likizo, magonjwa na uhamisho, lakini badhi ya watumishi hawakulipwa malipo hayo. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwalipa watumishi hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilihuisha posho na mishahara ya watumishi wake wakiwemo wa Idara ya afya kwa kujumuisha posho zote kwenye mishahara yao watumishi. Wakati wa zoezi hilo posho ya *On Call Allowance* taaluma na mazingira

magumu zilijumuishwa kwenye mishahara yao. Baada ya kujumuisha posho zote kwenye mishahara, Serikali ilianzisha mpango wa kulipa *Extra Duty Allowances* ambayo hulipwa pale mtumishi anapofanya kazi masaa ya ziada. Posho hii hulipwa pia kwa madaktari wanaoitwa kazini kwa muda wa ziada.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2005 Serikali iliamua kuwalipa watumishi wa Idara ya afya Mkoani Kigoma. Jumla ya sh. 204,813,000/= zililipwa kwa watumishi wa Idara ya Afya Mkoani Kigoma mpaka sasa. Watumishi ambao hawajalipwa posho zao ni waganga 3, Mhudumu 1, na mpishi 1 wa Halmashauri ya Kigoma. Malipo hayakufanyika kwa sababu kumbukumbu zao hazikukamilika. Jumla ya sh. 4,210,000 zitalipwa mara baada ya kupatikana kumbukumbu zao. Jitihada zinafanywa kuzipata kumbukumbu husika.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa kuwa watumishi wanaofanya kazi za kuwahudumia wagonjwa wenye magonjwa ya kuuambukiza hasa gonjwa hili la UKIMWI. Je, Serikali ipo tayari kuwapatia vifaa vya kuwakinga, na ni lini itawapatia posho maalum.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaangalia posho zote kwa ujumla, kama Naibu Waziri alivyosema posho zote tulijumuisha kwa sababu kulikuwa na utitiri wa posho na ikatokea wakati hizi posho zilikuwa zaidi ya mshahara. Kwa hiyo tukaona inakuwa vigumu hata kubajeti, lakini tukizungumza habari za UKIMWI peke yake kuna magonjwa mengine mengi sana. Sasa hivi tunachoangalia ni kujaribu kuangalia kitu kinachoitwa *incentive package* ili tuweze kuwapa *incentive* hawa watu wetu ikiwa ni pamoja na wale ambao tunawapeleka katika maeneo ambayo ni magumu. Kwa hiyo, ni *incentive package* ambayo itaangalia suala lote kwa upana na si UKIMWI peke yake au malaria peke au na magonjwa mengine. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana hapo hapo katika swali la msingi tunafahamu kwamba watumishi wa Hospitali ya Mkoa ya Bombo, Tanga wanadai *extra duty allowances* kwa kipindi cha muda mrefu sana, ambazo hazizidi shilingi milioni 300?

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatuambia wana mpango gani wa kuwalipa hawa watumishi ambao wako katika idara nyeti?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, malimbikizo ya madai ya wafanyakazi si katika idara yetu peke yake inakuwa vizuri mamlaka zinazohusika ziweke katika bajeti ili waweze kulipwa. Hakuna mfuko ambao ulitengwa kwa ajili ya maombi kama haya. Kwa hiyo, mimi ningewashauri wote wanaohusika katika Bajeti waweke haya malimbikizo na Serikali itaangalia namna ya kuwalipa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Pamoja na kuweka posho zote kwenye mshahara hawa watumishi wa idara ya afya lakini kwa kuwa kuna kazi za dharura kwa mfano kunapokuwa na mlipuko ya magonjwa kama ya kipindupindu. Watu hawa hufanya kazi nzuri sana huko vijijini, kazi ya kupambana na kipindupindu na magonjwa mengine ya kuambukiza.

Je, kuna sababu gani za kutokuwalipa wakati wanapokwenda kupambana na magonjwa hayo vijijini pamoja na kuweka posho zao kwenye mshahara?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kunapotokea mlipuko kama alivyosema Mheshimiwa Lubeleje, tunatenga pesa. Matatizo inakuwa kwamba wanalalamika kwamba pesa hazitoshi, lakini kunapokuwa na kipindupindu tunatambua kwamba wanafanya kazi ya ziada, wanakuwa kwenye yale mahema na wanalipwa hiyo posho. Sasa labda malalamiko kama nilivyosema yanakuwa wanasema posho haitoshi na sisi tunaitoa kulingana na uwezo na taratibu za Serikali.

Na. 90

**Kuboresha barabara**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ni mdogo sana kiasi cha kutoweza kutumia barabara muhimu zinazounganisha vijiji vya Magarama, Kigina, Lukaya, Mikonko na Kibuye na kwa kuwa vijiji hivyo vina wakazi wasiopungua 4,000 kwa kila kijiji ambao ni wakulima:-

Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa kuna haja ya barabara hizo kushughulikiwa na ngazi nyingine kama vile *TANROADS* ili kuboresha mawasiliano ya wananchi na urahisi wa kusafirisha mazao yao.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa lna Serikali za Mitaa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibanda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Barabara Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hupokea asilimia 30 tu ya fedha za Mfuko huo kwa ajili ya kuhudumia matengenezo ya barabara zilizopo chini ya Halmashauri. Asilimia hii ni ndogo kuweza kuhudumia mtandao wa Barabara zote za Halmashauri kwa wakati mmoja. Barabara anazozizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni za Halmashauri ya Wilaya ambazo ni barabara ya Kichananga – Kigina na Kumsenga –

Kibuye ambazo zinaunganisha vijiji vya Kigina na Kibuye. Mikonko ni Kitongoji cha Kibuye na Magerama na Rukaya ni vitongoji vya kijiji cha Kigina. Vitongoji vyote hivi vinaunganishwa na barabara za vijiji husika ambazo ni:-

(i) Kibuye-Mikonko, Kigina-Rukaya na Kigina-Magarama.

Barabara ya Kichananga – Kigina ilifanyiwa *Grading* mwaka 2004/2005 kwa fedha za msaada wa *Game Reserve* Moyowosi Sh.3,000,000 na barabara ya Kumsinga – Kibuye ilichongwa kwa nguvukazi mwaka 2004/2005 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara Sh.4,000,000/=. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Halmashauri imetenga kutumia fedha za Mfuko wa Barabara Sh.42,000,000/= kwenye barabara ya Kumsenga – Kibuye-Kagezi na Sh.24,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mawili kwenye barabara ya Kichanganga-Kigina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara hizo kushughulikiwa na *TANROADS* Bodi ya barabara ya Mkoa chini ya Mwenyekiti wake ambaye ni Mkuu wa Mkoa ndio Bodi inayoangalia barabara zilizoko Mkoani zenye hadhi ya kupandishwa madaraja toka za Wilaya kwenda za Mkoa. Barabara hizo zinapitishwa kwenye Kikao cha Bodi kwa kuzingatia vigezo vyote. Bodi hutuma maombi kwa Waziri mwenye dhamana ya barabara nchini ambaye ni Waziri wa Miundombinu. Hata hivyo Halmashauri itaendelea kuzihudumia barabara hizo.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza.

Je, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba fedha zinazotolewa na Wizara ni kidogo mno kwa Halmashauri ambazo sasa naweza nikasema ni Halmashauri zote sio Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo peke yake?

Je, haoni kwamba kuna umuhimu wa Wizara hiyo kuongeza kiwango cha fedha zinazotolewa kwa Halmashauri ili Halmashauri ziweze kufanya kazi zake vizuri kwa sababu fedha zinazotolewa na Halmashauri, ni fedha ambazo zinazotolewa na Halmashauri na ni fedha ambazo zinatokana na kipato ama kodi za wananchi, ni fedha ambazo haziwezi kutunza barabara hizo. Kwa kufanya hivyo nina hakika kwamba barabara zitatunzwa lakini Wizara hiyo ifike kwenye barabara hizo kuzitembelea na kuhakikisha kwamba zinaongezewa fedha kwa ajili ya kuziimarisha.

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uhaba wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara chini ya Halmashauri wote tunajua ni kubwa sana. Miaka yote umekuwa unaliuliza na tunajitahidi kulieleza, kuna namna mbili tu za kuweza kuongeza mapato kuhusiana na mfuko wa barabara.

Moja ni kurekebisha sheria ambayo ndio zimeweka kiwango cha asilimia 30 wakati mtandao unaohudumiwa na Halmashauri kwa sasa ni karibu kilomita 50,000. Kwa hiyo ni dhahiri kabisa fedha hiyo ya asilimia 30 ni kidogo. Lakini ya pili ni

kuongeza makusanyo ya mapato yetu kwa kadri yatakavyoongezeka asilimia hiyo 30 kwa maana ya fedha tutakazopata nayo vilevile itaongezeka. Kwa hiyo, mimi nafikiri Serikali itaendelea kulitazama jambo hili kwa upana wake ili hatimaye pengine tuweze kupata ufumbuzi wa namna ya kuhudumia barabara hizi vizuri zaidi.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza, kwamba ninakumbuka katika miaka ya 60,70,80 wananchi vijijini walikuwa wanahamasika sana kujenga barabara na kutengeneza barabara zinazounganisha vijiji vyao, na hivyo basi ukienda vijiji ulikuwa unaweza kuona barabara zilizo safi sana lakini zimetengenezwa na wananchi wenyewe.

Je, hivi sasa moyo uko wapi na Serikali inafanya nini katika kurudisha hali hiyo. Kwa mfano nikiangalia mahali kama wilaya ya Rombo, barabara ni safi sana zilizounganishwa kati ya kijiji na kijiji, Je, moyo ule huko wapi hivi sasa ahsante sana?

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa kauliza swali nzuri mimi naweza kulijibu lakini hata yeye anaweza kulijibu maana ni letu wote hapa. Moyo ule wa kujitolea umekwenda wapi?

Sasa ninafikiri tupeane changamoto wote mimi nimetembelea baadhi ya maeneo ambayo bado moyo huo upo wanajitolea kutengeneza barabara kwa nguvu zao wenyewe. Lakini yapo baadhi ya maeneo ambayo huo umekufa na hata unapojaribu kuhamasisha hata kama ni kilomita moja tu bado mwananchi anataka kwamba athibitishiwe kwamba atalipwa posho kwa ajili ya matengenezo ya barabara yake hiyo.

Kwa hiyo, mimi nafikiri tuendelee kutoa hamasa, tuendelee kuelimisha, ninaamini kabisa jambo hili linawezekana, lakini lazima wote tushirikiane Wabunge na viongozi wengine wote.

Na. 91

**Mikakati ya Kitaifa ya Kupambana na Rushwa**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa umehusisha wadau mbalimbali na Bunge likiwa miongoni mwa wadau hao, na kwa kuwa, Bunge lilianishwa majukumu na kwa hiyo linatakiwa kupanga mikakati ya utekelezaji wa majukumu haya:-

Je, Bunge limeshaandaa mikakati ya jinsi ya kutekeleza majukumu hayo na kama jibu ni ndiyo. Je, Waziri mhusika anaweza kuwasilisha Bungeni mikakati hiyo?Kama jibu ni hapana. Je, ni sababu gani zilizosababisha mikakati hiyo isiandaliwe?

Kwa kuwa mkakati wa kupambana na Rushwa wa mwaka 2001-2005 umekwisha.

Je, Serikali imeshaandaa mikakati/mipango itakayotekelezwa katika mkakati huo mpya wa kitaifa.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, mkakati wa kitaifa wa kupambana na rushwa hapa nchini na hata nje ya mipaka yetu, umehusisha wadau mbalimbali na Bunge likiwa miongoni mwao. Serikali imeendesha semina kwa wanachama wa *African Parliamentarians Network Against Corruption (APNAC)* ili wapate utaalam utakaosaidia katika maandalizi ya mikakati dhidi ya rushwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Bunge kama Taasisi, ndio inaandaliwa sasa kwa sababu kilichokuwa kinasubiriwa ni maandalizi ya mpango wa pili wa utekelezaji wa *National Anti-Corruption Strategy Action Plan* yaani *NACSAP II* ambao utazinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni.

(c) Uzinduzi huo utafanyika baada ya maandalizi yote muhimu kukamilika ikiwa ni pamoja na kuwahusisha wadau muhimu yaani Bunge, Mahakama, Vyama visivyo vya Serikali, Wanahabari na pia Sekta Binafsi.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Taifa kupambana na rushwa uliandaliwa na Serikali mara ya kwanza mwaka 1999 ikiwa ni utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya kero ya Rushwa iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba.

Ni kweli kuwa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati huo ulianza rasmi mwaka 2001 baada ya Serikali kuunda kitengo cha uratibu wa masuala ya utawala bora katika ofisi ya Rais – Ikulu kinachojulikana zaidi kama *Coordination and Good Governance Unity* na ulikamilika mnamo Desemba, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeaandaa mipango mingine ya kupambana na rushwa itakayoelekezwa kuanzia mwaka huu wa 2006 hadi 2010.

Mipango ya sasa itazihusisha pia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na Mashirika ya Umma, tutakuwa na Kamati za maadili yaani *Integrity Committees* katika maeneo hayo, pamoja na kuwasilisha taarifa kuhusu mapambano dhidi ya rushwa

katika maeneo husika kwa kitengo cha utawala bora katika ofisi ya Rais Ikulu Kamati hizi za maadili pia zitatakiwa kuwaelimisha watumishi wao kuhusu wajibu na haki zao.

**MHE. DR. ZAINAB GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa jitihada zake mpaka imeonekana na Wabunge wa dunia wanaopambana na rushwa kuja kufanya mkutano wa dunia wa kupambana rushwa hapa nchini, naomba niwapongeze.

Nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa, mkakati huu wa 2001/2005, Bunge, na ninaomba nitumie lugha hii nadhani mtanisamehe, lilizembea kupambana mikakati ya kulisimamia Serikali au kuisaidia Serikali katika suala hili;

Je, kwenye mkakati wa sasa, Bunge litahusishwa na likihusishwa litahakikisha Bunge kwamba na lenyewe linasimamia kutokana na *point* zile ambazo watakuwa wamepewa? Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kilichokuwa kinatendeka mwaka 2001/2005 ni kuandaa mkakati huu unaosemwa kwamba sasa tutaanza rasmi mwaka huu na hivi karibuni utazinduliwa na Mheshimiwa Rais, Bunge litahusishwa kikamilifu kwa maana ya kwamba katika Ofisi ya Bunge pia kutakuwa na hii Kamati ndogo ya Maadili yaani *Integrity Committee.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatarajia ya kwamba kwa upande wa Wabunge wenyewe kutakuwa na Kanuni za Maadili kwa Wabunge yaani *Cord of Conduct* lakini pia katika Bunge la mwezi Novemba mwaka huu tunatarajia kuleta Sheria mpya ya kupambana na rushwa kuchukua nafasi ya sheria ya zamani ya mwaka 1971.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Rushwa inaweza kugawanywa katika mafungu matatu, rushwa kubwa sana yaani *grand corruption*, rushwa ya katikati rushwa kubwa na rushwa ndogo tunaita *corruption* katika nchi yetu ni rushwa ipi ambayo imekithiri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimjibu Mheshimiwa Shellukindo Mbunge wa Bumbuli swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Matukio ya rushwa na matendo ya rushwa yanaweza yakagawanyika katika maeneo mengi tu kama ambavyo Mheshimiwa William Shellukindo ametuambia.

Kuna rushwa kubwa katika nchi yetu hakuna siri, kuna rushwa ya kati pia hakuna siri, kuna rushwa ndogondogo lakini tunalotaka kusema hapa ni kwamba kwa miaka 10 iliyopita Serikali imefanya kila jitihada kuondoa hii rushwa ndogondogo katika Sekta kama ya Elimu na Afya kadri ambavyo Serikali imeboresha huduma za elimu na afya kiasi cha kwamba kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule sasa anaweza kwenda shule bila mzazi kutoa rushwa, huduma zimekuwa karibu zaidi na wananchi bila kuwalazimika wananchi kutoa rushwa.

La msingi hapa ni kwamba tatizo la rushwa ni la sisi wote, tatizo la rushwa ni la raia wema wote hivyo siyo tu tushirikiane kupambana nalo lakini pia tusikalie haki zetu tujue majukumu na haki zetu muda wote na Wabunge tuwafundishe na tuwaelimishe wananchi wetu wajue haki zao na watetee haki zao ili hii iwe ni mbinu mojawapo ya kupambana na tatizo hili baya katika jamii yetu.

Na. 92

**Uhaba wa Vitendea Kazi kwa Polisi**

**MHE. FATMA OTHMAN ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi Jeshi la Polisi linalaumiwa kwa kutowajibika kwenye kazi zake na kwa kuwa Jeshi hilo lina uhaba mkubwa wa nyenzo za kufanyia kazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa Jeshi la Polisi Zanzibar vitendea kazi kama Magari, *Radio Call* na pikipiki?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Othman Ally, Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Jeshi la Polisi Tanzania Zanzibar lina uhaba wa vitendea kazi kama alivyoelezea Mheshimiwa Mbunge. Suala la uhaba wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi ni kwa Jeshi lote ikiwa ni pamoja na Tanzania Bara. Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu wa kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi na tayari Serikali imechukua hatua mbalimbali kushughulikia upatikanaji wa vifaa hivyo. *(Makofi)*

Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, Jeshi la Polisi limetengewa fedha kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali ikiwemo magari, vifaa vya mawasiliano, pikipiki n.k. kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ili kuimarisha ufanisi wa kazi. Serikali pia itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuliimarisha Jeshi la Polisi kwa vifaa, kadri uwezo utakavyoruhusu.

**MHE. FATMA OTHMAN ALLY**:- Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hoteli nyingi za kitalii Zanzibar ziko kandokando ya bahari na majambazi hutumia boat kwenda kufanya uhalifu kwenye hoteli hizo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kulipatia Jeshi la Polisi boat za doria katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** :- Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Fatma Othaman Swali la nyongeza kama ifuatayo:-

Serikali imeona umuhimu huo na hivi karibuni tu ilinunua *boat* mbili, moja imewekwa Dar es Salaam na moja iko Zanzibar kwa ajili ya kupambana na uhalifu baharini. (*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa suala la gari ni tatizo kubwa sana kwa kituo cha Chwaka kikishirikiana na kituo cha Dunga katika Jimbo la Chwaka.

Kwa kuwa, kwa mwaka wa 10 kuwekwa matumaini ya kwamba gari inaweza kupatikana kushirikiana na Kituo cha Chwaka na Dunga.

Je, Waziri atatueleza nini kutokana na hizo gari ambazo zitakuja kwa kipindi hiki kutokana na kituo cha Chwaka na Dunga?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** :- Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, swali lake na nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli upo umuhimu wa vituo vyote vya Polisi viweze kupata magari lakini kutokana na hali ya uwezo wa nchi yetu tunavipanga kutokana na mahitaji na mazingira yalivyo na jinsi uhalifu unavyojitokeza. Kwa hiyo, pale tutakapokuwa na nguvu vituo vyote hivyo vitapata magari. Lakini kwa sasa tunaomba tufanye mgao kufuatana na mahitaji halisi yanayohitajika.

Na. 93

**Ulipaji wa Malipo ya Pensheni**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:

Kwa kuwa, kiutaratibu malipo ya pensheni kwa wastaafu inapswa ilipwe mara mbili kwa mwaka yaani kila mwisho wa mwezi Desemba, na mwisho wa mwezi Juni.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba malipo ya pensheni yanayopaswa kulipwa mwezi Desemba, hulipwa mwezi Februari na yale ya Juni hulipwa mwezi Agosti?

(b) Kama Serikali inafahamu hivyo. Je, kuna hatua zozote zilizo chukuliwa kurekebisha na kuondoa kabisa adha hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo kuanzia mwaka 2005 pensheni ya Januari hadi Juni hulipwa katikati ya mwezi Januari, na ya Julai hadi Desemba hulipwa katikati ya mwezi Julai ya kila mwaka.
Kabla ya hapo malipo hayo yalikuwa yanalipwa kila tarehe 31 Januari na tarehe 31 Julai ya kila mwaka. Hata hivyo mstaafu halazimika kwenda Benki kwa wakati huo kwani fedha hiyo hubaki Benki kwa kipindi cha miezi mitano zaidi hivyo kwa maelezo hayo hapo juu hatujawahi kulipa malipo ya pensheni kwenye mwezi wa Februari au mwezi wa Agosti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu unaandaliwa wa kuweza kuwalipa wastaafu mapemda zaidi yaani tarehe 31 Desemba na tarehe 30 Juni ya kila mwaka ili kuwawezesha wastaafu wastaafu kulipa ada za watoto wao kama walivyoomba.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:-**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali moja la nyongeza.

Hivi sasa kuna wastaafu ambao walistaafu miaka ya 1980 na 1990 na wakati huo kwa kweli mishahara yao ilikuwa ni midogo sana. Je, Serikali haiwezi ikafikiria angalau kuwaongezea kidogo kulingana na hali ya maisha ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr.Guido G. Sigonda, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Unayosema ni ya kweli na kweli tumekaa na baadhi ya wastaafu kwa ngazi mbalimbali na kuona kwamba kuna mahitaji ya kupitia upya hayo mafao wanayoyapata sasa hivi na kuangalia hali inavyoweza kuturuhusu kifedha na tuweze kuwarekebishia pensheni yao kwa mujibu wa hali ilivyo hivi sasa. Hilo bado tunalifanyia kazi na tunaahidi wajumbe wastaafu hao kwamba tutakapokuwa tunafanya zoezi hili tutawaita watusaidie ili tuweze kujua wastaafu wa ngazi mbalimbali, wa hadhi mbalimbali wako wapi na kama bado wapo ili tuweze kufanya hili zoezi kwa ufanisi zaidi.

**MHE. SAID S. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna baadhi ya watumishi wastaafu wanaotembea masafa marefu kufuata malipo yao ya pensheni kwa mfano kutoka Sikonge kwenda Tabora, kwa nini usiwepo utaratibu wa kupeleka pensheni za wastafu kwenye benki zilizo karibu na wastaafu hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Nkumba, kama ifuatavyo:-

Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba wastaafu wanalipwa pahali ambapo wako karibu na hapo ili wasipate matatizo hayo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niulize swali moja.

Kwa kuwa matatizo ya wastaafu yamekuwa yakitajwa kwenye Bunge hili mara nyingi na kwa miaka mingi, hivi ni kweli Serikali imeshindwa kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba wastaafu hao wanalipwa kila mwezi wawe na *pay roll* na tatizo hili likaisha moja kwa moja?

**WAZIRI WA FEDHA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali hilo kama ifuatavyo.

Kwa kweli suala la wastaafu kama tunavyojua limekuwa na matatizo lakini hata hivyo Serikali imekuwa inashughulika nalo. Hivi sasa tunasema kwamba wastaafu wanalipwa kila baada ya miezi sita na pale ambapo pana matatizo kwa kweli tunaweza kushughulikia lakini utaratibu ndiyo huo wa kulipa kila baada ya miezi sita, wazo hilo la kulipa kila baada ya mwezi mmoja pamoja na wazo lile ambalo lilitolewa kabla la kuongezea fedha kwa ajili ya wastaafu kama tunavyosema kwamba Serikali italifanyia kazi suala hili.

Na. 94

**Ulipaji Kodi kwa Mtindo wa PAYE**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004 wafanyakazi walioajiriwa wanalipa kodi kwa mtindo wa *PYE* imeonekana wanalipa kodi kubwa zaidi ya wafanyabiashar na hata Watanzania wengine ambao hawalipi kodi kwa njia hiyo na wana mapato yaliyo sawa au zaidi ya mapato ya wafanyakazi hewa wanaolipa kwa mifumo ya *PAYE*.

(a) Je, Serikali inafikiriaje kuviangalia upya viwango vya kodi vilivyowekwa na Sheria hiyo ili kumpunguzia mfanyakazi mzigo huo?

(b) Je, ni Watanzania wangapi walioajiriwa kwenye Ofisi za Kibalozi ambao mwajiri hawajibiki kuwakata kodi kwa mtindo wa *PAYE* ambao wanalipa kodi kwa hiari yao na ni kiasi gani cha mapato Serikali inakusanya toka kwa Watanzania hao katika kipindi cha 2004/2005?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza wigo wa kodi kama njia ya kuongeza mapato ya Serikali huku ikipunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi wanaolipa kodi kwa mfumo wa *PAYE*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mara kwa mara imekuwa ikivifanyia mapitio na marekebisho viwango vya kodi kwa sababu mbalimbali pamoja na kuboresha mfumo wa kodi, kupunguza mzigo wa kodi (*Tax Burden*), kurahisisha uwajibikaji wa kodi (*Tax Compliance*) na kadhalika. Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi ili kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi wa kipato cha chini. Kwa mfano, mwaka 1998/1999 kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi kilikuwa shilingi 45,000/= mwaka 2002/2003 kilikuwa shilingi 50,000/=, mwaka 2004/2005 kilikuwa shilingi 60,000/= na mwaka 2005/2006 ni shilingi 80,000/=. Marekebisho hayo yamekuwa yakifanyika ili kuwaondolea mzigo wa kodi wafanyazi wote. Serikali itaendelea kufanya hivyo kwa awamu jinsi hali ya uchumi inavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 wafanyakazi mia nne (400) walioajiriwa kwenye Ofisi za Kibalozi walilipa kodi ya Mapato ya Ajira, ambapo kiasi kilicholipwa ni shilingi milioni mia tano nina nane nukta saba ( 518.7m). Kati ya hawa, wafanyakazi hamsini na ne (54) walikuwa wanatoka kwenye Balozi na walichangia kodi ya shilingi milioni mia moja hamsini nukta tisa(150.9m) wakati wafanyakazi mia tatu arobaini na sita (346) wanatoka kwenye ofisi zenye hadhi ya kialozi na walichangia kodi ya shilingi milioni mia tatu sitini na saba nukta nane (367.8m)

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imejizatiti kuongeza wigo wa kodi na mapato ya kodi. Imedhamiria kupambana na ukwepaji kodi na kuhakikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inakusanya kodi kwa kiwango cha ubora wa hali ya

juu zaidi ya kile kilicho kwenye Bajeti. Katika kufikia azma hii Serikali inachukua hatua za makusudi za kuboresha utawala wa kodi kwa kuboresha uwezo wa utendaji kazi wa *TRA.* Aidha, imejizatiti kufichua na kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi, kuboresha elimu kwa walipa kodi na kuwapunguzia walipakodi gharama za kuwajibika kikodi (*Tax Compliance Cost*)

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wote imekuwa ikijitahidi kuondoa kodi zenye kuleta kero au zenye gharama zaidi ya mapato yanayokusanywa ili kuwaondolea usumbufu wananchi wake.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, kwa mujibu wa vifungu 7(1) na 8(1) Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 pato linalotozwa kodi ni ile faida inayotokana na ama ajira ama biashara yaani *Gains or Profits from employment of business* lakini kanuni inayotumika yaani *formular* ya ukokotoaji wa faida hii ni tofauti kati ya waajiriwa na wafanyabiashara ambapo kwa upande wafanyabiashara inaruhusu gharama za uendeshaji kutolewa au kusamehewa kodi kama gharama ya nyumba na kadhalika wakati kwa wafanyakazi sivyo.

Je, Serikali inafikiriaje kurekebisha tatizo hili kwa upande wa wafanyakazi ili nao waruhusiwe kusamehewa gharama za kawaida za kazi yaani kikodi tunaita *expenses hully and exclusively incard for the production of employement income* kama gharma ya usafiri kwenda kazini, gharama ya chakula mfanyakazi anapokuwa kazini, gharama ya kupanga nyumba inawalazimika kupanga ili aweze kufanya hiyo kazi na gharama nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokuwa anatoa hotuba yake ya Bajeti tarehe 15 Juni, 2006 ukiangalia kipengele nambari 30, kipengele kidogo cha 4 imeelezwa vizuri kabisa kwamba haya ni kati ya yale mambo ambayo yataangaliwa ili kuhakikisha kwamba kodi yote inayostahili inalipwa na itafunguliwa vizuri na watu wale ambao watakuwa kuna matatizo kuangalia ni namna gani hao wafanyakazi tufanye nini katika kipengele hicho cha nne ukurasa wa 30 inakupa namna gani Serikali itaendesha Bajeti yake na kipato chake kitakuwa cha aina gani na kwa mujibu wa kodi ya aina gani na kwa mujibu kodi mbalimbali.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kodi ya wafanyakazi ambayo ni *PAYE* inaonekana inaleta mzigo mkubwa sana kwa wafanyakazi kwa sababu inakusanyika kiurahisi na ukilinganisha na kodi ya makampuni yaani *Cooperation Tax* na kwa kuwa kuna makampuni ambayo yamekuwa yakifanya kazi zaidi ya miaka mitano na ku – *declare* kwamba yanapata hasara na kwa sababu yanapata hasara hayaruhusiwi kulipa kodi. Je, Serikali haioni sasa kwamba ni wakati muafaka wa kubadilisha Sheria ili yale makampuni ambayo yanafanya kazi ya biashara na yanaleta hasara na kutokulipa kodi ya kampuni. Sasa iwekwe sheria ya kuweka kiwango kamili ambacho kitafanya walipe kodi hata kama hawatengenezi faida kwa sababu wanakuwa wanaongeza gharama za uendeshaji?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Hayo ni kweli unayoyasema na hayo ni mojawapo ya mambo tutakayoyaangalia kuhakikisha ukwepaji wa kodi unafanyika namna gani na vipi na njia gani zifuatwe ili kuhakikisha kwamba kodi zetu zote zinalipwa. Kwa hiyo, hilo tunalikubali lakini tutalifanyia kazi.

Na. 95

**Kuwasaidia Wazee Wasiojiweza na Watoto Yatima.**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika nchi yetu wapo wazee wengi wasiojiweza na ambao hawana msaada wa kutosha na kwa kuwa pia wapo watoto yatima wanaoishi katika mazingira ya kukosa Elimu, Malazi bora na pia lishe bora.

Je, Serikali imeandaa mpango wa kukabiliana na matatizo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuwepo kwa wazee wasiojiweza na ambao hawana msaada wa kutosha. Wazee hao wanakosa mahitaji ya msingi ya maisha ikiwa ni pamoja na malazi, mavazi, huduma za afya, chakula, ulinzi, kupendwa, kuthaminiwa na kupewa ushauri nasaha.

Kwa kutambua umuhimu wa wazee kama raslimali katika maeneleo ya nchi, Wizara iliandaa Sera ya Taifa ya Wazee ambayo ilipitishwa na Baraza la Mawaziri mwaka 2003. Madhumuni ya Sera hiyo ni kuhakikisha kuwa Wazee wanatambuliwa na kushirikishwa katika mambo yanayohusu maisha yao ya kila siku na kuhakikisha kwamba wazee wanapata huduma zote muhimu ambazo zitawawezesha kuishi maisha bora kama watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Pamoja na kuwepo kwa sera na mipango mbalimbali inayohusu wazee, Wizara inaendesha makazi 17 ya wazee wasiojiweza na ambao hawana msaada na inaratibu na kusimamia makazi 24 ya wazee hao yanayoendeshwa na Wakala wa Hiari.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na watoto yatima wanaoishi katika mazingira ya kukosa elimu, malazi bora na lishe bora, Serikali inatekeleza kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wa maendeleo Mpango shiriki Jamii wa utambuzi kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu. Mpango huu hutekelezwa kwa kuziwezesha jamii kuweka vigezo vinavyotumika katika kutambua watoto hao na mahitaji yao ikiwa ni pamoja na na elimu, malazi bora na lishe bora.

Kupitia mpango huu jamii hupanga mipango ya kuwahudumia watoto hao na Serikali pamoja na wadau wengine mbalimbali wakiwemo wadau wa maendeleo,

mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya dini na watu binafsi hujitokeza kuwadaidai watoto hao. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2005/2006 Mpango huu umekwishatekelezwa katika Halmashauri 33 za Tanzania Bara.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wadau wengine unaandaa mpango wa kitaifa wa Hifadhi ya Jamii wa *Social Protection Plan* ili kuweza kuwapatia huduma za uhakika wazee, walemavu, watoto wanaoishi katika mazingira magumu wakiwemo watoto yatima.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na Serikali kuandaa mikakati hiyo na kwa kuzingatia kwamba bado nchini kwetu tunazo ombaomba nyingi zilizotawala. Je, Serikali iko tayari kutenga fedha maalum kwa ajili ya kuwasaidia angalau hifadhi ya elimu ili kuepusha kuathirika kisaikolojia watu hao?

Je, ikiwa kwa sasa Serikali haijawa tayari au haijawa na uwezo wa kufanya hivyo. Je, iko tayari kuomba wafadhili wa nje na wa ndani kusaidia matatizo haya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maida Abdallah kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama nilivyosema katika swali la msingi inajitahidi lakini kama tutarejea nyuma katika swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Mariam Mfaki, namba 23 la Mwezi Juni pamoja na mambo mengine tulisema kwamba Serikali inaendesha haya makazi na imekuwa ikitenga fedha mwaka hadi mwaka.

Kama tunakumbuka tulisema jumla ya shilingi miliomi 200 zilitengwa mwaka 2004/2005. Mwaka 2005/2006 tulitenga milioni 284 na mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba bado Serikali inaendelea kuona umuhimu na kuweza kusaidia jinsi gani ya wazee tutaweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba pamoja na kuomba misaada na Serikali kuwasaidia Wazee, walemavu na watoto ninaomba ifahamike kwamba suala la kuwapeleka wazee na watoto yatima katika makazi huwa inatakiwa kuwa ni suluhisho la mwisho kabisa baada ya njia nyingine zote kushindikana.

Sisi kama wananchi na kama wanajamii na ninaliomba Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kwenda katika maeneo yetu ili tuweze kuwahamasisha wananchi waweze kutambua umuhimu wa kuwalea wazee, watoto yatima na walemavu kabla Serikali kwa sababu hili ni jukumu la jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wanajamii tunapaswa kuwasaidia wazee ambao walikuwa wametoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Na. 96

**Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya 2005/2006 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya - Makongorosi kwa kiwango cha lami na kwa kuwa, Wakala wa Barabara nchini *TANROADS* tayari imetangaza tenda ya mradi huo mwezi Nobemba 2005.

Je, Serikali inaweza kutamka ramsi kuwa ujenzi wa barabara hiyo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi kwa kiango cha lami na Wakala wa Barabara nchini yaani *TANROADS* ilitangaza zabuni ya ujenzi wa barabara hiyo mwezi Novemba, 2005.

Makandarasi wanne waliwasilisha zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo na uchambuzi wa zabuni hizo ulifanyika. Uchambuzi ulibaini kwamba bei zilizotolewa na makandarasi zilikuwa za juu sana zikilinganishwa na Bajeti iliyopo na makisio ya gharama za ujenzi wa barabara ya kiwango hicho cha lami. Kutokana na hali hiyo zabuni ilifutwa na mpango wa kuitisha zabuni upya ulifanyika.

Katika zabuni hii mpya, mradi utagawanywa katika sehemu mbali mbali na zabuni tofauti zitaitishwa kwa kila sehemu. Utaratibu huu utapunguza muda wa ujenzi wa barabara kwa kuwa makandarasi wawili watajenga barabara hiyo kwa wakati mmoja na pia itawezesha makandarasi wazalengo kushiriki kutokana na masharti kupunguzwa. Maandalizi hayo yanatarajiwa kukamilika za zabuni mpya kuitishwa mwezi Julai 2006.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba kuchukua zaidi ya miezi 8 kuonyesha kwamba kuna kasoro kiutendaji katika Mamlaka husika na kwamba atazirekebiesha kasoro hizo ili tusije tukasimama hapa kuulizana tena baada ya miezi 8?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR.MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli zabuni hiyo ilichelewe, lakini kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi suala la makandarasi ku-*tende*r bei ya juu kuliko *Engineers estimate* ndiyo lilikuwa tatizo, na hili si jambo la ajabu. Mara nyingi Serikali inatumia wataalam wake kujaribu kuangalia ni kiwango gani cha fedha zingetosha barabara hiyo. Sasa kama zinatofautiana na makandarasi wote walio-*tender* na Serikali ikaona kwamba haina bajeti kama hiyo, inarudi na kujipanga upya. Ni uchelewesho huo uliotokea na kuleta matatizo yaliyojitokeza. Lakini kama nilivyosema sasa hivi tumejipanga kugawa barabara hiyo katika sehemu mbili na kwa kweli barabara hiyo nina hakika sasa itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa Fedha tunaoanza kwa sababu fedha zipo. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda wa maswali umekwisha. Ninaomba mniwie radhi tuna orodha ndefu sana ya wachangiaji ambao wanataka kuchangia hoja maalum kabisa ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ninaomba tukubaliane kwamba muda wa maswali umeisha ili tuweze kutoa nafasi ya matangazo na wale Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia waweze kupata nafasi ya kuchangia. Hapa mezani kwangu ninayo matangazo machache kama ifuatavyo:-

Tangazo la kwanza, taarifa ya kikao, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati Uwekezaji na Biashara anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa leo tarehe 27 Juni, 2006 saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo, katika chumba namba 231 ghorofa ya pili.

Tangazo la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wabunge wa Lindi, anaomba Waheshimiwa Wabunge hao wakutane hapo nje saa 7.00 mara baada ya kuahirisha Bunge.

Napenda kuwatambua wageni wa Mheshimiwa Omar Kwaang'w Wakulima wa Kahawa kutoka Bonga Babati, ambao wako nasi leo hapa ndani. Ahsante.

Napenda kumtambua Mheshimiwa Aisha Kipangula Katibu wa CCM wa Wilaya ya Makete, ameambatana na Mweka Hazina wa CCM wa Mkoa wa Iringa ambaye ni Mume wa Mheshimiwa Monica Mbega. *(Makofi*)

Naomba kutambua kuwepo wa Mke wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambaye yupo pamoja nasi hapa leo. Waheshimiwa Wabunge, naomba kutambua kuwepo wa Mheshimiwa Remidius Kissassi, aliyekuwa Mbunge mwenzetu katika Bunge lililopita, lakini pia alikuwa Mbunge wa Bunge la Afrika. Huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan. *(Makofi)*

Napenda kuwatambua Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Zaynab Vulu kutoka Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Naomba kumtambua Mheshimiwa Esha Stima alikuwa Mbunge katika Bunge lililopita na ni mgeni wa Mheshimiwa Elizabeth Batenga. Naomba kumtambua Mchungaji wa Kanisa la Wasabato, Dodoma na mke wake ambao ni wageni wa Mheshimiwa Esther Nyawazwa. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu. Katibu tuendelee.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Kiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Kiti.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Kanuni kifungu namba 55(3).

**MWENYEKITI:** Ukurasa namba ngapi samahani Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Ukurasa namba 38.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi lazima niungame kwanza kwamba nilipokuwa shule Kiswahili sikufaulu kama alivyofaulu Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir. Na kama nilivyomsikia vizuri Mheshimiwa Dr. Zainab Gama alipokuwa akiuliza swali la nyongeza alitumia lugha kwamba Bunge lilizembea na kwa kuwa Bunge ni wewe, yeye na sisi na Waziri Mkuu. Sasa nataka tafsiri ya neno sahihi la Kiswahili inayotamka neno kuzembea na kama kuzembea limezembea nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ametumia kifungu hicho kuomba ufafanuzi wa neno hilo linamaanisha nini? Sasa ninamwomba Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama leo yuko tayari kutoa maelezo ya neno hilo anaweza kuyatoa na kama hayuko tayari basi anaweza kumpa taarifa Mheshimiwa Spika lini anaweza kutoa maelezo ama afute kauli ya neno lake hilo na kulibatilisha. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa maana ya neno kuzembea. Maana ya kuzembea ni kutofanya jambo ulilopewa

kulifanya. Kwa hiyo, ni kuzembea. Na Bunge lilipewa jukumu katika Mkakati wa Taifa. Kwanza, Wizara zote zilipewa majukumu kuweka mikakati yake na iko ndani ya Kitabu. Niko tayari nikipewa muda nilete kitabu jinsi Wizara zilivyoweka mikakati yake, Bunge halikuweka mikakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa maoni kuhusu kanuni aliyoisema Mheshimiwa Mbunge na Kanuni aliyoitumia 55 (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge ni chombo cha heshima, Bunge linaitwa Bunge Tukufu. Ukitumia neno kuzembea maana yake Bunge ni zembe. Haiwezekani Bunge likawa zembe na Wabunge wakawa wazembe. Namtaka Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kwa kuwa tunamheshimu afute kauli yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Bunge linakutaka ufute kauli yako kwa sababu wakati ukisema hoja ile hukutoa uthibitisho wa yale ambayo ulikuwa unayazungumza. Je, uko tayari kufuta kauli hiyo?

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wewe umethibitisha lugha hii si Kiswahili, naomba niifute. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Katibu endelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae. Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hebu samahani kidogo. Waheshimiwa Wabunge tafadhali naomba mnapotoka mtoke kwa utulivu kusudi tuendelee na Shughuli za Bunge. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ingawa ni ndefu, lakini ni hotuba nzuri. Nawashukuru pia watendaji wake wote, watalaam wake wote ambao wametayarisha hotuba hii kwa muda mrefu na baadaye jana ndiyo imewasilishwa hapa. Nawashukuru pia wanapiga kura wa Jimbo langu la Chambani kwa kunichagua kuja hapa kuleta matatizo yao ambayo ni mengi na mimi naahidi kwamba sitowaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi. Naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:- Kwanza, kuhusu hali ya chakula nchini. Kwa bahati mbaya nchi yetu imekuwa na matatizo ya ukame ambayo yamejirudia kwa miaka mingi na kwa hivyo, imesababisha matumizi yasiyo ya lazima kwa nchi yetu. Lakini nakumbuka hali mbaya zaidi ilikuwa katika mwaka 1998 ambako katika mwaka huo kwa bahati mbaya Wakuu wa Wilaya hawakueleza waziwazi au hawakutoa umuhimu waziwazi kueleza wananchi kuhusu uzito wa suala la njaa na matokeo yake ni kwamba watu wengi walikufa kwa sababu ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nilishiriki katika ugawaji wa chakula cha njaa katika Wilaya ya Kilosa na katika maeneo mbalimbali. Nilishuhudia jinsi wazee hadi vijana walikuwa wanakufa kwa ajili ya njaa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuwa na ushapavu na ujasiri wa kueleza waziwazi kuhusu hali halisi ya nchi na kuchukua hatua zifaazo kuhakikisha kwamba hakuna raia aliyekufa kwa njaa katika nchi hii. Nampongeza Waziri Mkuu binafsi kwa ujasiri wake, kwa ushapavu wake kwa kutembelea maeneo mbalimbali kuona hali halisi ya njaa na kwa kutafuta misaada ya ndani na ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hili kuna matatizo mengi sana yaliyojitokeza. Kulikuwa na upungufu wa chakula ambacho kilikuwa kinatakiwa kipelekwa kwa wananchi, *SGR* zilikuwa hazitoshi, kulikuwa na matatizo ya usafirishaji wa chakula na *SGR* zenyewe hazikuwa katika maeneo ambayo wananchi walikuwa na shida ya chakula. Lakini mapungufu ambayo yameonekana mwaka huu itakuwa ni kipimo cha kutayarisha kwa miaka inayofuata. Nafikiri tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imeshaandaa mikakati mbalimbali kuhakikisha kwamba kama kutakuwa na tatizo la njaa basi mambo ambayo yamekuwa na mapungufu katika kipindi hiki yatapatiwa ufumbuzi katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo ambalo ningependa kulizungumzia katika suala hili la njaa ni kuhusu *attitude* ya wafanyabiashara. Nafikiri Serikali kwa makusudi kabisa iliwapa nafasi wafanyabiashara hasa wa Dar es Salaam kuagiza chakula kwa ajili ya wananchi. Kwa bahati nzuri chakula kiliazigwa lakini bei badala ya kushuka ilipanda. Kipindi kile mahindi yalikuwa yanauzwa kwa kilo 300/= yakapanda mpaka shilingi 600, kwa kilo, mchele ambao ulikuwa unauzwa kwa kilo shilingi 500, ukapanda mpaka shilingi 1,000/= kwa kweli bei imeendelea kupanda hadi leo. Mfumuko wa bei ya mazao ya chakula kwa sasa hivi ni asilimia 10.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa ni kuwa hakukuwa na ufuatiliaji mzuri. Baada ya Serikali kwa nia nzuri kabisa kuwaeleza wafanyabiashara wa Dar es Salaam waagize chakula. Inawezekana wafanyabiashara wakubwa au wadogo lakini hakukuwa na ufuatiliaji kuona kwamba: Je, azma hii ya Serikali ya kuondoa tatizo la chakula inapatikana au haipatikani. Kwa hiyo, ni changamoto kwa Serikali kuona kwamba katika awamu yoyote inayofuata basi Serikali inapotoa tamko la kuagiza chakula basi ifuatilie. Je, wale walengwa wanafaidika au hawafaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo ningependa kuchangia ni juu ya bei ya mazao ya chakula. Tanzania imebahatika kuwa na mazao mengi ya biashara. Kwa mfano, katika Tanzania Bara, kuna mazao kama pamba, tumbaku, korosho, mkonge, chai, miwa au sukari na kadhalika Tanzania Visiwani kuna zao la karafuu. Zamani kulikuwa na nazi kama zao la biashara na viungo.

Naelewa kwamba Wizara ya Kilimo, Chakula na Masoko siyo Wizara ya Muungano. Lakini naelewa vilevile kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina majukumu ya kuwasaidia uchumi wa Zanzibar na hili limo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 23 ambayo ningependa ninukuu: "Katika nukuu aliyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Mheshimiwa Rais alipozindua Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005, ninanukuu: "Tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika maendelo ya uchumi na ya kijamii ya Zanzibar bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mambo ambayo si ya Muungano. Lakini naamini uchumi ambao ni mkubwa zaidi una wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar ambao ni mdogo." Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Muungano ina wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar. Katika msaada huo mimi ningetilia mkazo zaidi msaada wa kusaidia uchumi wa zao la biashara la Zanzibar yaani zao la karafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karafuu Zanzibar imekufa, kama utapanda ndege utembelee sasa hivi utaona ni kweupe tu kama mvi. Mikarafuu mingi ya Zanzibar imekufa.

Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali ya Muungano kwa makusudi kabisa kuisaidia Zanzibar katika kuimarisha zao lake la karafuu. Sisi tumekuwa tukiishauri Serikali ya Zanzibar kubinafsisha zao la karafuu kwa sababu hakuna maendeleo yoyote ya zao lile. Lakini kwa sababu ambazo Serikali yenyewe inazijua imekataa. Wakati huo tumependekeza kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama wanaendelea na kununua zao la Karafuu Zanzibar basi angalau wawaruhusu wafanyabiashara wengine wanunue vilevile karafuu Zanzibar. Wanaweza kuweka *indicative price* ambayo watasema kwamba bei hii Serikali inanunua na wengine vilevile wananunua, lakini hilo pia limeshindikana. Serikali bado inang'ang'ania kununua karafuu Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue Tanzania Bara kwa mfano, mazao yote ya biashara niliyoyataja Serikali haing'ang'anii yawe yanamilikiwa na wakulima wadogo

wadogo au wafanyabiashara, wawekezaji wadogo wadogo au wawekezaji wakubwa Serikali kazi yake ni kusaidia ukuaji wa mazao yale.

Lakini kwa kweli tunashangaa kuona kwamba kule Zanzibar zao ambalo ni tegemeo la kila Mzanzibari na zao ambalo linachangia asilimia 90 ya uchumi wa Zanzibar limekuwa kama halina mwenyewe. Mikarafuu inakufa, haishughulikiwa, hakuna utafiti unaofanywa, hakuna vitalu vinavyotosheleza kulisha mikarafuu, hakuna madawa na hakuna chochote. Nakumbuka katika miaka ya 90 Serikali iliwaita Waingereza kufanya utafiti kugundua maradhi mawili diabetes, satan death, ikaanza kuugua mikarafuu, lakini baada ya hapo mpaka leo hakuna kilichofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu hii ni Serikali ya Muungano na ni Serikali ya CCM kwa nini basi katika sera za CCM na Serikali ya Zanzibar inayosema:-

“Kuendeleza mazao yaliyopo ya biashara na kuongeza mengine.” Kwa nini Serikali ya Muungano isisaidie katika zao la karafuu, yale mengine hayapo tena, hakuna nazi na hakuna viungo, kwa sababu Zanzibar ilikuwa ni visiwa vya viungo, lakini viungo vimepotea.

Tulikuwa na pendekezo lingine tunasema basi angalau pawe na kilimo cha Mkataba, kilimo cha Mkataba ni makubaliano baina ya wakulima na wafanyabiashara na Serikali iwe mfanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kuna suala la soko, kuna suala la bei, kuna suala la huduma na kuna suala la pembejeo. Serikali ishauriane na wakulima juu ya bei, lakini Serikali inakaa inapanga bei haimhusishe mkulima wa aina yeyote. Basi itakuwa afadhali wakati wa Wakoloni kulikuwa na kitu kinaitwa CGA *Clove Growers Association* ambacho hiki chombo kiliwasaidia sana wakulima wa karafuu, lakini leo hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bei ambayo Serikali inatoa ni mdogo mno. Kwa sababu sasa hivi tani moja ya karafuu inauzwa 1,000/=, kwa bei ya Kimerikani ni *dollar* 3500, lakini wananchi wanapewa dollar 1250 ambayo ni asilimia 45.6 only bei ya soko je, hii ni halali? Ni halali hilyo!

Sasa wananchi wanatafuta njia za panya sasa wanaenda katika nchi za jirani kutafuta bei na ziko bei nzuri huko. Sasa Serikali badala ya kuongeza bei kwa wananchi inatumia fedha nyingi kununua vyombo vya kasi, kum-*mobilize* Askari wa KMKM ili kulinda Kisiwa ili karafuu zisitoke. Hayo si maajabu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nahisi hapo kuna mapungufu makubwa sana. Serikali ya Muungano lazima isaidie zao ambalo ni tegemeo la wananchi wote wa Zanzibar na Serikali yenyewe. Inaonyesha sasa Serikali imeshindwa haiwezi kuboresha

zao lile. Karibuni sisi Waheshimiwa Wabunge kutoka upande wa Pemba tumepata wazo la kuanzisha zao la korosho. Tukaongea na Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho akakubali, akapeleka mtaalamu wake Pemba kutafiti kama zao linastawi au halistawi, mtalaamu kasema zao linastawi. Akapelekwa mtaalamu kufundisha walikuma ambao wangependa kulima zao la korosho, wakulima wakajitokeza kwa wingi mno, wakapewa utaalamu ule na wakaanza kupanda kwa majaribio.

Baada ya muda mfupi tukasikia tangazo kutoka Radio Zanzibar ni kwamba ni marufuku kupanda korosho Zanzibar au Pemba. Tumeshangaa kwa sasa hii ni sera ya CCM kuboresha zao lililopo na kuongeza mengine ya biashara. Sasa mnaposema ni marufuku korosho Zanzibar sisi tunashangaa, na hii ni MKUKUTA na kule kuna MKUKUTA. Jamani tufanye nini sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri vyombo vinavyohusika visaidie zao la korosho liende Pemba, kwa sababu wananchi wamekubali. Tunafikiri ni aina nyingine ya mkombozi Pemba.

Suala hili tumelizungumza kwa Mheshimiwa Rais tulipokutane naye Kambi ya Upinzani, na mimi nimeishamwandikia barua Waziri wa Kilimo, Chakula na Masoko. Nafikiri Kiongozi wangu wa Upinzani atamwandikia barua Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hili. Tunataka yapatikane kweli mapinduzi ya kilimo na kweli wananchi wafaidike na kilimo. Kama hizo ni sera zenu basi tunaamini mtazifuatilia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuwa mimi nimefanya utafiti wa muda tu. Nilikuwa mkulima wa mpunga, nilikuwa mkulima wa mahindi na nyanya hapa hapa Tanzania Bara katika Mkoa wa Morogoro. Mimi nilikuwa nikilima mahindi kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Msemaji wetu wa pili ni Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Lakini naona hayupo humu ndani. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Jacob Shibiliti ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Vilevile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote japokuwa leo hawapo waliochaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika uongozi wa Chama chao. *(Makofi)*

Vilevile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji kwa Bajeti yake ya mwaka 2006/2007 kupitishwa bila kupingwa. *(Makofi)*

Vilevile napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake aliyoitoa jana ambayo inaonyesha mwelekeo mzuri. Na pongezi zangu za dhati pia ziende kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani TAMISEMI kwa hotuba yake inayojenga ambayo naamini ikizingatiwa tutasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa naomba nitoe angalizo. Jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba anathamini sana michango ya Waheshimiwa Wabunge na kweli mimi nime-*observer* katika kipindi kifupi nilichokaa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wanatoa maoni ambayo ni *productive*. Lakini unakuta Waheshimiwa Mawaziri wakiwa wanajibu hoja aidha, wanajibu kimzaha bila kuzingatia hayo maoni yao, kitu ambacho siyo kizuri.

Mfano mzuri tu, ni juzi Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa alivyokuwa akijibu hoja zilizohusu *COMESA* na *TANESCO.* Mheshimiwa Waziri alikuwa yuko tayari kabisa kutetea suala la *COMESA* na *TANESCO* wakati anajua kabisa kuondoka kwetu *COMESA* kumetuathiri kwa kiasi kikubwa. Na vilevile *TANESCO* iko katika hali mbaya sana.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Mawaziri wanapojibu wawe *serious* na wakijue kwamba wote tuko katika lengo moja la kujenga nchi yetu na wala siyo kubomoa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja katika hoja zangu. Hoja yangu ya kwanza, nitazungumzia barabara *especially* zile ambazo ziko chini ya TAMISEMI.

Ni kweli kabisa sote tunafahamu kwamba Wizara ya TAMISEMI ni nyeti na ni Wizara ambayo inagusa maslahi ya Watanzania moja kwa moja. Nikizungumzia hili ninamaanisha kwamba ni muhimu Wizara kama hii ikapatiwa Bajeti kubwa ambayo itatosheleza mahitaji kwa namna moja au nyingine.

Hivi sasa ninavyozungumza kila mtu anafahamu kwamba barabara za TAMISEMI ni barabara ambazo sasa hivi ziko katika hali mbaya sana na kwa hii mvua iliyomalizika juzi, nyingi ya hizo barabara ni mbovu. Mfano tu, ni barabara ya Makoka ambayo sasa hivi imekatika katikati hali iliyopelekea wananchi wa Makoka kutengwa kabisa na wananchi wengine wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Sasa nikija katika mafungu ya barabara. Katika Mkoa wa Dar es salaam tunaambiwa kwamba katika TAMISEMI zimetengwa milioni 460 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Sasa tunajiuliza hizi milioni 460 zitatosha vipi? Wakati juzi Mheshimiwa Waziri akinijibu swali la Shekilango aliniambia kwamba ile barabara ya kilomita 3 tu inagharimu karibu bilioni 2. Sasa hapa inabidi tujiulize hivi kweli tuko *serious* katika kutatua hili tatizo la barabara au tunakuwa tunafanya mzaha.

Vilevile ninakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alivyosema leo asubuhi kwamba kuna umuhimu wa wananchi kujitolea. Unakuta kweli wananchi wana nia ya kujitolea, lakini kuna vitu vingine ambavyo vinakuwa vinahitaji *support* ya Serikali. Nikitolea mfano, Wilaya ya Kinondoni, kuna greda moja tu na hilo greda sasa hivi ni mbovu.

Sasa unakuta wananchi kweli wana nia ya kutengeneza barabara, lakini wananchi hawezi ku-*afford* kununua greda, wao wanahitaji watoe mchango wao aidha wa mafuta au wa kokoto *then* greda lije liwasaidie. Lakini tunaambiwa Wilaya kama Kinondoni ambayo ni kubwa greda liko moja na ni bovu. Sasa katika mazingira kama hayo unategemea wananchi watakuwa na moyo kiasi gani wa kusaidiana na Serikali katika kutatua matatizo ambayo yanawasibu.

Vilevile nikizungumzia suala la barabara nitazungumzia barabara ya Kilwa najua hii iko chini ya *TANROAD.* Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa kama msimamizi wa Wizara zote na watendaji wote wa Serikali naamini atanisaidia katika hili. Hakuna ubishi kwamba sasa hivi wananchi ambao wanategemea barabara ya *Kilwa Road* wanatumia masaa karibu matatu kwa safari nusu saa kufika kazini, tatizo ni kwamba barabara ni mbovu. Sasa tunajiuliza hilo tatizo litatatuliwa lini na kuna mkakati gani wa dhati wa kuhakikisha kwamba hiyo kero ya barabara inaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kuhusiana na ujenzi mpya wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Juzi wakati Mwanasheria Mkuu akijibu hoja kuhusiana na utata wa juu ya nafasi ya Mkuu wa Mkoa alituambia dhahiri kwamba Mkuu wa Mkoa yeye ni mwakilishi wa kisiasa tofauti na ambavyo wengi wetu tunadhani kwamba labda ni msaidizi kiutendaji wa Rais Mkoani ambapo anakuwa anawakilisha *interests* za watu wote. Sasa ukituambia ni mwakilishi wa kisiasa *by implication* anatuambia kwamba anakuwa anawakilisha *interest* ya kile chama ambacho kimemweka pale. Sasa *that being the case* kwa nini Bajeti yake iingie Serikalini, basi itoke kwenye chama ambacho kimemweka pale. Lakini hiyo pia inatuonyesha jinsi ambavyo tumekuwa tukilalamika kwamba Wakuu wa Mikoa wanatubana sana kwenye kampeni na wanatubana sana masuala mengine. Ifikie kipindi kiongozi awe amechaguliwa na watu sio analetwa na mtu anabandikwa pale *at the end of day* anakuwa anatetea *interests* za mtu aliyemweka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija sasa kwenye hoja ya msingi tunaambiwa kwamba kuna fungu limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa watu ambao wamekwenda Dar es Salaam na wanafahamu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imefanyiwa ukarabati mkubwa na mamilioni yametumika na ripoti inaonyesha hivyo. Vile vile tumeambiwa kwamba kuna fedha nyingine ambazo zinafanya *extension* ya jengo lile lile. Sawa, japokuwa sikubaliani nalo kwa sababu yeye ni mtendaji wa kisiasa huyo hana haja ya kuwa na ofisi pale. Lakini iweje kuwe na fedha kwa ajili ya kujenga ofisi yake nyingine. Zinatengwa shilingi milioni 154 kwa ajili ya kufanya utafiti wa ujenzi wa Ofisi yake. Basi hizo shilingi 154m. *better* ziingizwe pia kwenye TAMISEMI ambao wana shughuli nyeti za barabara badala ya kwenda kujenga maofisi ambao mwisho wa siku yatakuwa matupu hayana mtu. Kwa sababu naamini

Mkuu wa Mkoa hana watendaji wengi kiasi hicho. Kwanza pale ofisi ipo ya kumtosha, pili haina haja ya yeye kuongezewa ofisi nyingine ambayo haina umuhimu kulingana na hali yetu ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuzungumzia kuhusiana na ofisi mpya ya Waziri Mkuu. Kwanza labda niseme sina pingamizi kuhusiana na ujenzi mpya wa Ofisi ya Waziri Mkuu inategemea itajengwa wapi. Serikali ya Awamu ya Nne ambayo tunaiita ya Ari Mpya ilituambia kwamba tutahamia Dodoma. Leo hii tunaambiwa kwamba Waziri Mkuu shilingi bilioni moja ni kwa ajili ya kujenga Ofisi tena Dar es Salaam. Ingekuwa Dodoma mimi ningeelewa. Tena nina *sympathies* sana na Waziri Mkuu kwa sababu kweli ofisi yake ya Dodoma iko katika hali mbaya sana, hilo halina ubishi. Lakini leo tunaambiwa kwamba shilingi bilioni moja imetengwa kwa ajili ya kujenga ofisi Dar es Salaam tena sio ujenzi rasmi ni katika utafiti sasa tuje tujiulize hilo jengo lenyewe litagharimu shilingi ngapi? Hiyo shilingi bilioni moja ingepelekwa mahali pengine tungeweza kufanya mambo makubwa au ofisi ijengwe Dodoma au basi tuambiwe kabisa jamani Makao Makuu ya Tanzania sasa hivi ni Dar es Salaam mambo ya Dodoma yamekwisha kieleweke kimoja. Hiyo nategemea Waziri Mkuu atanipa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hoja yangu nyingine ni kuhusiana na tatizo la chakula. Labda pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo walivyo-*deal* na tatizo la chakula kwa kuzunguka mikoani kuwapa moyo kwa waathirika na kutoa *alternative solution* nini kifanyike. Lakini kama ambavyo Mheshimiwa aliyetangulia kuzungumza alisema ni kwamba tulitaarifiwa kwamba wafanyabiashara watapewa misamaha ya kodi hivyo tutegemee chakula kitashuka bei. Sasa matokeo yake imekuwa vinginevyo misamaha imetolewa na vyakula vimepanda bei. Kila mtu anatoa *excuse* ya kupanda bei ya petroli kwamba ndio gharama ya kila kitu. Sasa sijui kama hiyo petroli imekuwa inaiathiri Tanzania peke yake kuliko nchi zingine. Nategemea kupata majibu. Ila mimi nilikuwa nafikiria kwamba tulikuwa tunaomba chakula lakini *at the same time* tunaambiwa mikoa mingine inazalisha chakula lakini kutokana na ubovu wa barabara wanashindwa kusafirisha chakula kutoka sehemu moja au nyingine. Sasa nadhani badala ya kuwaambia wananchi katika kila kaya waweke sijui gunia 5 za mpunga au mchele ili kuzuia njaa *it is better* basi tuboreshe miundo mbinu ili tuweze kujisaidia ndani ya nchi sio tunakwenda kuomba chakula nje wakati kuna mikoa mingine ambapo vyakula vinaoza. Kwa hiyo, ni vizuri kutafuta *alternative solution* ambayo inajenga zaidi kuliko *alternative solution* ambayo inabomoa.

Mwisho kabisa labda nimalizie kuhusiana na suala la mishahara na nitamalizia kidogo kuhusiana na ile shilingi milioni 500 ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu uliitangaza jana kwamba imetolewa. Mishahara niliuliza Wizara ya Menejimenti ya Utumishi katika Kamati zetu tukaambiwa kwamba kutokana na kuwa Kamati imeundwa na Rais kuhusiana na kuangalia mishahara ya watumishi wa umma. Kwa mwaka huu kutakuwa hakuna ongezeko la mishahara. Lakini *at the same time* tunaambiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba mishahara mwaka huu itaongezeka. Sasa hapa kunakuwa kuna *confusion* Je, mishahara kweli itaongezeka mwaka huu au mishahara inasubiri mwaka ujao wa fedha ili watu wajue kwamba kweli mwezi Julai

wasubiri kama fedha zimeongezeka au mambo yale yale. Isije ikawa tunafanya tu siasa mwezi wa Julai watu wanakwenda benki wanakuta mambo ni yale yale. Kwa hiyo ni vizuri kila kitu kuwa wazi. Wategemea nitapata pia *clarification* kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa hizo, shilingi milioni 500 za Mheshimiwa Waziri Mkuu alizozitangaza. Ni ndogo sana kwa mikoa lakini nikupongeze ni nzuri *for a start*. Sasa kumekuwa kuna mikopo mingi tumeambiwa kwamba misaada inatolewa lakini mwisho wa siku unakuta wanapewa watu wa aina fulani au labda wanapewa watu wa itikadi fulani. Sasa sijui kuna mikakati gani ambayo tumeandaa kuhakikisha kwamba hiki kidogo ambacho kinatolewa kinawafikia walengwa wote na kinakuwa kwa madhumuni ya mahitaji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kukushukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, na Spika mwenyewe kwa jinsi mnavyoweza kuliongoza vizuri Bunge hili, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge ni mwakilishi wa watu hivyo ukusanya mambo mbalimbali kutoka jimboni kwake na kuyaleta hapa kuja kuwasemea wenzake. Mimi Wana-Missungwi wamenipa mambo machache sana niombe tu kwamba hayo basi yapokelewe na Serikali yetu ya Awamu ya Nne. Cha kwanza kabisa nimetumwa nije niishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri waliyoifanya na niiombe Serikali isichoke kupokea shukrani katika suala zima la njaa.

Missungwi tulikuwa na matatizo makubwa sana lakini jinsi Serikali ya Awamu ya Nne ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete imefanya kazi ya maajabu kabisa kuwakomboa wananchi wa Tanzania nasema hongereni sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na unifikishie salamu kwa Mheshimiwa Rais Wana-Missungwi kwa kweli isingekuwa utaratibu wa Serikali wengi sana wangeweza kupata matatizo ya janga hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili waliloniagiza wamenituma nije cha kwanza nisiongeze maswali mengi katika hotuba ya Serikali hii, Rais ni mpya ndiyo kipindi chake cha kwanza kuomba fedha ili aweze kutekeleza majukumu mbalimbali.

Lakini pia Waziri Mkuu ni mpya katika nafasi hiyo. Mawaziri wote waliopo hapa ni wapya katika nafasi zao. Nikaombwa Bajeti yote kwa ujumla na Wizara zingine usiziwekee kikwazo. Sasa napenda nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu fedha ulizoomba wewe na walizoomba wengine Wizara zote mimi kwa niaba ya Wana-Missungwi nasema zote zipite kama zilivyoombwa bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe kwa jinsi ulivyoweza kuwasillisha hotuba yako vizuri. Kwa msaada wa Mawaziri wanaokusaidia lakini bila ya kuwasahau Makatibu Wakuu na

Wakurugenzi wengine. Hotuba imeandaliwa vizuri, umeisoma kwa umakini wa hali ya juu, haikuwa na mikwaruzo yoyote ile mpangilio umepanga vizuri hiyo ndiyo imefanya mambo yangu yawe rahisi zaidi katika kuchangia michango yangu. Nianze kukumbushia mambo machache sana ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe mwenyewe ni shahidi.

Ukiamua kuongea suala lolote kuhusu Missungwi usipogusa maji Wana-Missungwi hawakuelewi. Waziri Mkuu ulikuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, unafahamu vizuri zaidi matatizo ya maji ndani ya mji wa Missungwi. Missungwi ina matatizo makubwa sana ya maji. Kata ya Missungwi sasa hivi ina wakazi zaidi ya 15,000 kwa maana ya vijiji vya Mabuki, Lubuga, Iteja, Mwambola na Missungwi yenyewe. Vijiji vyote hivyo vina matatizo ya maji. Lakini Missungwi peke yake ina wakazi zaidi ya 8,000 na ina kaya 2,150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mji wa Missungwi maji yanauzwa shilingi 200/= kwa debe, shilingi 100/= wakati wa masika. Wakati wa kiangazi ni matatizo makubwa. Mipango mbalimbali imekuwepo. Katika jibu langu nililopewa na Wizara ya Maji mkutano uliopita nilihakikishiwa kwamba tungeingia katika ujenzi wa Musoma/Bukoba pamoja na Missungwi kwa kufadhiliwa na Wafaransa. Lakini katika Bajeti hii kidogo naona aidha kuna matatizo fulani. Sasa nikuombe Waziri Mkuu utakapopata nafasi ya ku-*wind up* ulizungumzie hilo. Uelezee kutakuwa na mkakati upi wa kuwanusuru Wana-Missungwi. Tafsiri mbalimbali zimekuwa zikisemwa, kila mmoja anatafsiri jinsi anavyoweza kutafsiri itakuwaje Missungwi iliyo karibu na maji isipate maji lakini yapelekwe kilomita zaidi ya 250. Tumeeleza mikakati iliyokuwa inaendelea lakini nina imani nawe Waziri Mkuu utalifanyia kazi na Missungwi itapata maji. Nina imani kubwa sana Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zimekuwa ni nyingi Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa John Samwel Malecela, aliahidi kama Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu aliahidi na mipango ndiyo iliyokuwa inaendelea lakini kwa bahati nzuri zaidi Mheshimiwa Rais aliyeko madarakani aliahidi na kwa urefu zaidi akasema yatafika mpaka Sumve maji yatakayopatikana. Upembuzi yakinifu tayari nina imani kubwa kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu utalifanyia kazi ili kero ya maji kwa Missungwi ifutike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie mradi wetu wa maji kupeleka Shinyanga na Kahama. Katika upembuzi yakinifu nadhani kuna makosa kidogo yaliyofanyika. Ilisemekana kwamba umbali wa kilomita 5 kutoka kwenye bomba kuu vijiji hivyo vitanufaika na mradi huo. Lakini cha ajabu kuna baadhi ya vijiji vimeachwa ambao umbali wake ni kilomita 4 kama Mahando. Kijiji kingine ni Mwamazengo tenki lipo ni umbali wa kilomita karibu 3 lakini hakihusishwa. Kijiji kingine ni Mwamagili ambacho kiko ndani ya Mwagiligili ni tawi tu la Mwamagili lakini ni kijiji cha Mwagiligili. Katika kata ya Irujamate yenye vijiji vitano ni kijiji kimoja tu kilichopata na wao ndio walinzi wakubwa wa mazingira katika eneo hilo. Ebu wataalamu wetu wafikirie basi vijiji hivyo viweze kuhusishwa katika *phase* inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la mifugo. Kwanza niunge mkono suala la uhifadhi wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji. Nakubaliana kabisa na wafugaji waliotolewa kule Ihefu. Nia ya Serikali ni nzuri tu ya kuwatoa kule kwenye vyanzo vya maji na iwatafutie mahali pengine. Lakini kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu wasitimuliwe basi waandaliwe mahali pa kuwapeleka. Limekuwepo tatizo kubwa yaani saa sita mchana unaambiwa ondoke uende zako, aende wapi. Lakini nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Mbeya jinsi hatua aliyoichukua yeye mwenyewe kwenda kuongea na hao wafugaji akatoa elimu ingawaje ni ya muda mfupi lakini walielewa na walisema kwamba hatutarudi tena kuingia kwenye eneo hili. Cha msingi sasa atafutiwe mahali pa kuwapeleka hawa watu kwamba baada ya kutoka hapa tunawapeleka mahali fulani. Mifugo iangaliwe. Nimpongeze sana Waziri wa Mifugo pamoja na Naibu Waziri. Wameliangalia suala la ruzuku kwenye madawa ya mifugo wakati tunazugumzia suala la mifugo kwenye Kamati kulikuwa kumetengwa shilingi 500 milioni, lakini baada ya kupiga kelele kule wameliona hilo na wameongeza limekuwa ni bilioni 2 nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji utakuja utuletee faida na tuuchukue kama mazao mengine tunavyoweza kuyachukua. Mheshimiwa Waziri Mkuu wafugaji waliomba upate nafasi ya kuwaita kama jinsi ulivyokuwa unawaita wadau wa mazao makuu kama pamba, kahawa, korosho na tumbaku, watengewe muda na wao uje uwasikilize jinsi watakavyoweza kutoa mchango wao na jinsi watakavyoweza kuchangia katika pato la Taifa. Nakuomba sana Waziri Mkuu ulifanye hilo ili angalau wafugaji waweze kujisikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ebu nigusie suala la barabara. Wenzangu wamezungumzia suala la barabara kuanzia Usagara kwenda Geita. Mimi naungana nao kabisa lakini hilo tuiachie Serikali. Serikali ni sikivu hakuna sababu ya kurudiarudia. Nizungumzie tu kipande cha kuanzia Usagara kwenda Fyela hadi Kisesa. Nimezungumza mara nyingi sana hapa Bungeni bado lipo tatizo kubwa, yaani mawasiliano hayapo. Nimwombe Waziri wa Miundombinu atenge hata kiasi kidogo kwa ajili ya kufungua wakati *designing* inaendelea ili angalau mawasiliano baina ya Bujingwa, Fyela mpaka Usagara yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya niipongeze Serikali kwa kukipa hadhi kituo cha afya cha Missungwi kuwa Hospitali ya Wilaya. Hatua kwa kweli ni nzuri wananchi wengi wanasaidiwa sana katika hospitali yetu hiyo. Lakini nimpongeze tu Waziri wetu wa Utumishi ambaye kwa kweli suala la watumishi analizingatia na katika maelezo yanayoendelea upatikanaji wa watumishi sasa hivi sio tena wa mlolongo wa mzungumko ni moja kwa moja anapata ajira anaelekezwa aende akafanye kazi mahali fulani. Nakupongeza sana Mama kwa uamuzi wako huo. (*Makofi)*

Lakini upande wa afya nizungumzie suala moja mimi ninalo kambi la wazee pale Bukumbi. Tuna zaidi ya watu 450 wana matatizo makubwa hawana gari, hawana Mganga pale isipokuwa kuna Manesi wawili tu. Chakula kinachelewa zaidi ya miezi mitatu matokeo yake wanaanza kuzagaa. Kuna wengine ni walemavu wanashindwa hata kutembea kutoka sehemu fulani kwenda sehemu nyingine. Wapewe gari, wapewe

Waganga pale ili wazee wangu niendelee kuwalea mtakapokumbuka kuja kuwachukua ninyi wazazi wenu karibuni, lakini mimi nawalea zaidi ya 400 ninao pale. Walemavu, wasioona wana kila aina ya matatizo. Nisaidieni sana nipate fedha niweze kuwalea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nigusie kwenye suala la elimu mimi ni maarufu sana kwa kuishi na walemavu. Ninayo Shule ya Msingi Mitindo ni ya Wasioona, lakini nina matatizo mengi kweli. Ebu iangaliwe kwa jicho la huruma basi sisi tusioona basi ninyi mnaoona mtuone ili angalau tuweze kupata huduma inayostahili katika shule yetu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nirudie tu kusema kwamba hotuba ya Waziri Mkuu ni nzuri lakini Waziri Mkuu atazingatia suala la maji katika mji wetu wa Missungwi. Naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kama wenzangu napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata wa zaidi ya asilimia 80. Ushindi alioupata Mheshimiwa Karume kule Zanzibar ambao umekifanya Chama cha Mapinduzi kiendelee kuongoza dola ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vile vile Waheshimiwa Wabunge wenzangu kurudi humu ndani ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza wote kwa kupata nafasi ya kurudi kuwawakillisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri aliyoianza ya utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Niishukuru kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu Serikali ya Awamu ya Nne ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwanusuru Watanzania katika janga la njaa. Anayekunusuru njaa anakunusuru kifo. Kwa niaba ya Watanzania wenzangu nchi nzima pamoja na wale wa Sikonge namshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete, Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa na watendaji wote walioshiriki kufanikisha chakula kuwafikia wananchi kwa wakati muafaka. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu Bajeti hii ni ya kwanza, sasa kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri lakini na mimi nina mambo machache niliyotumwa na wananchi wenzangu siwezi nikayasema haya yote ya jimbo langu la Sikonge, lakini nataka niseme mambo machache tu.

Kwanza suala la Utawala Bora. Zipo Wilaya ambazo zilianzishwa kwa mfano Wilaya mbili Sikonge, Missungwi na nyinginezo, zimepewa Wakuu wa Wilaya lakini yako mambo muhimu ambayo kwa kweli suala la Utawala Bora linakosa ule uzito. Toka tupewe Wilaya hizi wananchi wetu kwa kweli bado wanapata taabu sana ya suala la Mahakama. Hakuna Mahakama za Wilaya.

Kwa mfano kwangu mimi kuna Mahakama moja tu ya Mwanzo Wilaya nzima. Huwezi kutegemea hapo suala la kumhakikishia mtu anayekuwa na tatizo pengine la kuhitaji huduma ya Mahakama basi ahudumiwe vinginevyo kesi ikihamia Tabora Mjini kilomita 71 basi hata kama anayo haki huyu mtu anaweza akafika mahali akaacha kwa sababu ya umbali na gharama. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni suala la *OCD.* Wilaya ya Missungwi hakuna *OCD.* Wilaya ya Sikonge hakuna *OCD* wanasubiri nini hawa mbona Mkuu wa Wilaya amekuja. Hivi nani ambaye ana wasi wasi wa kukaa mahali. Mkurugenzi amekuja. Mimi nafikiri ni jambo muhimu sana watu hawa hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ya Awamu ya Nne inatilia mkazo suala la upambanaji wa ujambazi watu hawa ni muhimu sana wawepo katika maeneo ya Wilaya hizi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la barabara kutoka Tabora/Ipole hadi Rungwa. Hii ni mara yangu ya nne sasa nasimama kwenye Bunge hili nasema. Nimezungumza sana enzi za Mheshimiwa Magufuli mpaka ameondoka barabara iko pale pale. Sasa Mheshimiwa Mramba umeingia na bahati nzuri sana Mheshimiwa Mramba umekaa Mbeya unaielewa umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Makongoro nataka nikutaarifu barabara ina makorongo mengi sana. Niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri muiangalie barabara hiyo halafu ni aibu sana barabara, barabara inaitwa barabara kuu. Barabara kuu haipitiki. Ikifika masika tu mvua zikinyesha hakuna mawasiliano kati ya Wilaya yetu ya Sikonge katika maeneo ya tarafa hizi mbili, tarafa ya Kiwele na Sikonge. Hata utengenezaji wa barabara. Barabara hii bahati nzuri baada ya mvua za *el-nino* ilipata fedha kupitia Benki ya *ADB.* Serikali ikatoa tenda kwa Bwana mmoja anaita Badri *East Africa* lakini kwa bahati mbaya alirundikiwa tenda nyingi sana nchi nzima kashindwa kufanya kazi na mimi sioni kama kulikuwa na sababu gani ya msingi ya kumpa kazi nyingi sana.

Katika maeneo mengi akashindwa kufanya kazi, muda ule wa mkataba ukaisha *ADB* wakakatisha mkataba wa kuleta fedha. Sasa tumeleta tatizo kubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ulione hili kwamba kwa kweli hii barabara ni kero kubwa sana jimbo la Sikonge kwa kweli sisi tunahitaji tuwe na mawasiliano na wenzetu wa Mbeya sasa hatuna mawasiliano. Lakini hata sisi wenyewe hatuwezi tukatembeleana. Naiomba sana Serikali kwa kweli ilipe kipaumbele jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo suala la kilimo. Naiomba Serikali pamoja na kwamba wakulima wetu wanaweza wakalima vizuri, wakapanda vizuri na mvua zikanyesha vizuri. Lakini bila mbolea hasa ya chumvi chumvi ya viwandani bado tutaendelea kupata uhaba wa chakula.

Sasa hapa ingawa nasikia yapo maeneo machache yanalima bila mbolea lakini ninachopenda kusema tu ndugu zangu ni kujidanganya kuwa virutubisho vilivyopo kwenye mbolea ya chumvi chumvi kwa kweli vinaongeza mazao.

Sasa uzalishaji maeneo mengi sana kunakwamisha kutokana na wakulima wetu kutoweza kumudu gharama za pembejeo. Bado mbolea kwa kweli gharama yake ni kubwa sana. Wananchi wetu walioko kule vijijini kumudu gharama za mbolea ni tatizo kubwa. Sasa hivi mbolea ni biashara kubwa sana kwa wafanyabiashara.

Kwa hiyo, wanaofaidika sana ni wale wafanyabiashara, wanaochukua ile mbolea kuja kumuuzia mkulima. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali kuona umuhimu wa kuangalia bei ya mbolea. Hamuwezi mkawa na soko huria kwa masoko huru mpaka kwenye mbolea hili ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuita wadau wa mazao muhimu nchini, pamba, tumbaku, na kadhalika. Kwenye tumbaku Serikali inadhamiria kuongeza uzalishaji kutoka tani 48,900 hadi tani 100,000 ifikapo mwaka 2010. Sasa hii ni rahisi kusema, lakini wazalishaji wetu waangaliwe matatizo yao ndipo tutakapopata mafanikio. Tatizo la kwanza ni hilo la pembejeo kwamba bei ni kubwa kama nilivyolisema, lakini wakopeshaji vile vile wa pembejeo kwa maana ya mbolea na madawa kutojali matatizo ambayo yako juu ya uwezo wa wakulima. *(Makofi)*

Kwa mfano mkulima wa tumbaku akikopa mbolea anategemea alipe baada ya mavuno, lakini yapo matatizo mengine kama hayo ya ukame, mafuriko na kadhalika. Hakuna utaratibu wowote ambao ni muafaka unaoweza kumsaidia mkulima akipata tatizo la ukame, basi angalau sasa huyu anayemkopesha aone pengine umuhimu labda wa kumpa muda wa kulipa wa miaka miwili au aone umuhimu wa kumpunguzia angalau gharama za kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kutatokea tatizo la ukame, mkulima amepata kiasi fulani cha mauzo yake, yule anayemkopesha anaamua kukomba chote na kumuacha huyu mkulima masikini aanze upya tena. Hili ni tatizo kubwa sana.

Sasa naomba sana, pengine Serikali huko mbele ya safari ione uwezekano wa kuona umuhimu wa wakulima wetu angalau kuwa na bima. Wao wenyewe wanaweza wakafungua, basi wakawa na bima ili wanapopata matatizo, iwasaidie. Hasa huko tunakoelekea katika kipindi cha kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanawezeshwa katika suala zima la mikopo, kama hatutakuwa na utaratibu wa bima kwa wakulima wetu, vyombo hivi vya kuwakopesha kama mabenki vitawapeleka wengi sana Mahakamani. Kwa sababu mtu anaweza akalima tatizo la ukame likawepo na hakuna namna nyingine ya kulipa kwa sababu mradi ni uleule mmoja. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuliona hili hapo baadaye. Magari yana bima, watumishi wana bima, wakulima wetu nao ni muhimu baadaye wakawa na kitu hiki muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilikuwa naiomba sana Serikali, kwanza naishukuru sana kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo kutoka Shilingi bilioni saba mpaka Shilingi bilioni 21. Lakini kwa mazao ya biashara Mheshimiwa Waziri Mkuu, inawezekana likawa gumu katika kipindi hiki, lakini katika vipindi vijavyo, naomba sana

mazao ya biashara nayo yapewe ruzuku ya pembejeo kwa kuwa yanaongeza pato kubwa kwa Taifa. Sasa tukipeleka tu ruzuku yetu ya pembejeo kwa mazao ya chakula peke yake tunawanyima haki hawa wakulima wa mazao ya biashara. Maana kuna wakulima wengine wanalima sana mazao ya biashara halafu baadaye wanatumia mazao hayo ya biashara kununua mazao ya chakula. Sasa tuwape nafasi nao wapatiwe ruzuku ya pembejeo ili waweze kuzalisha zaidi kuongeza kipato chao na kuliongezea Taifa letu pato zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa na hayo machache, sipendi kengele nyingine inigongee, naomba tena niendelee kuishukuru sana Serikali ya Awamu hii ya Nne kwa kazi nzuri iliyoanza kuifanya na naendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, haya machache niliyoyasema Serikali iyazingatie na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tupo pamoja naye kumsaidia katika utekelezaji wa shughuli zake. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu wetu. Kwanza nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa kunipa heshima tena kwa mara nyingine ya kurudi katika Jengo lako hili Tukufu ili niwawakilishe katika shida zao nyingi walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Wabunge wenzangu kwanza kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwa jinsi ilivyoweza kuwasilisha Bajeti yenye mwelekeo ambayo Wazungu wanasema, *is a people centred budget*. Lakini lililonifurahisha mimi sio hilo tu, kwa mara ya kwanza ninaona jinsi Serikali yenye ufanisi, Serikali ya Uwezeshaji inavyojaribu kuoanisha itikadi ya Chama chake ambayo imeiweka Serikali na matendo yake kama utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii ni nzuri kwa sababu kwanza ni *replica* ya bendera ya Chama cha Mapinduzi, ya kijani kwa maana ya kuhifadhi mazingira. Katika bendera ile lipo jembe. Serikali hii makini imeamua kumkomboa mkulima kwa kuongeza ruzuku yake kutoka Shilingi bilioni saba mpaka Shilingi bilioni 21 kwa sasa. Inatafsiri bendera ya Chama iliyoiweka madarakani na nikakumbuka ule usemi uliosema, Chama imara kinazaa Serikali iliyo imara. *(Makofi)*

Tunashuhudia leo kwa vitendo na Bajeti hii haikuishia hapo, ikachukua nyundo iliyowakilisha wafanyakazi, ikasema na tutazame tuboreshe mazingira na mishahara ya wafanyakazi. Hongera sana Serikali ya Awamu ya Nne. Ni tafsiri nzuri na inatupa heshima sisi Wabunge tuliopitia Chama cha Mapinduzi kwamba sasa tunakwenda kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie jukwaa hili kuleta salamu za upendo kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Lowassa. Wamenituma nikushukuru sana kwa kuokoa zaidi ya nyoyo 3,000 za waliokuwa wameachwa kwenye uchaguzi wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbeya Mjini tumekuwa tukiongoza katika mitihani ya Darasa la Saba kwa miaka minne mfululizo na kufaulu kwetu ni asilimia 90 ya watoto wote. Lakini mwaka jana tuliweza kupeleka watoto asilimia 38. Lakini baada ya *intervention* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa imesimama kwenye asilimia 76.4. Wazazi wa Mbeya walifanya ibada maalum ya kumwombea Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yetu mpate afya mwendelee kututumikia na kutuhudumia Watanzania. Kama unavyojua, Mbeya tunaongoza kwa Makanisa mengi na mimi hapa Bungeni mnanijua kama Askofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa Mzee John Livingstone Mwakipesile, alifanya kazi nzuri sana ya kusimamia lile agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifuatilia na sio kufuatilia tu, ninakumbuka Jimboni kwangu kile kilichowezekana alisaidia kifedha. Ninamshukuru sana.

Lakini nitakuwa ni mtovu wa nidhamu nisipomshukuru sana Meya na Mkurugenzi pamoja na Waheshimiwa Madiwani, walifanya kazi nzuri kwa kipindi cha miezi mitatu tukafanikiwa kujenga Shule mpya tano, tena za kisasa zenye *standard*. Nasimama leo ndugu zangu, Wabunge wenzangu sio maneno yaliyonileta Bungeni, ni vitendo. Toka nimekuwa Mbunge ninajivunia kwa kuwa na Shule mpya 18 nilizozisimamia kama mimi. Watu wa Mbeya hawataki maneno, wanataka matendo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na tazama andiko limesema, ombeni mtapewa na sisi kama waumini, tunasema itiini mamlaka iliyoko katika nchi kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu. Sisi hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tumelitimiza. Leo hii kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba nitumie nafasi na wadhifa walionipa wenzangu kama Askofu, nikuombe.

Pale kwangu Mbeya Mjini Mheshimiwa Waziri Mkuu ninashamba la Iwambi. *Iwambi Dairy Farm*, ni kama hekari 1,500. Jiji la Mbeya ni Jiji linalokua na kupanuka. Nimepata Wawekezaji kutoka Hong Kong wanataka wajenge viwanda ambavyo vitakuwa na soko la *DRC*, soko la nchi za *SADC*. Nimeshindwa mahali pa kuwaweka.

Ninakumbuka kauli ya Rais wetu alisema kipindi hiki cha Awamu ya Nne ni kipindi ambacho lazima tuvumilie baadhi ya maamuzi yatakuwa makubwa, mimi ninaamini maamuzi haya ni *two way traffic*. Yapo maamuzi ambayo wananchi ni lazima tuyavumile kutoka Serikalini na vilevile Serikali nayo ikubali yapo mambo ambayo wananchi wakiomba mvumilie kutupatia, hii ni Serikali ya watu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba zile hekari 1500 za Iwambi ipewe Halmashauri ya Jiji la Mbeya ili iweze kujipangilia vizuri katika heshima na hadhi ya kuwa Jiji. Mheshimiwa Waziri Mkuu ninyi ndiyo walezi wetu hapa. *(Makofi)*

Mwenyekiti wangu hapa , Mheshimiwa Jenista Mhagama aliomba katika Bunge lililopita, alikuwa na shamba kama hilo la Hanga akaomba akapewa. Mimi nataka

nitumie maandiko hayo, ombeni nanyi mtapewa. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, barua yangu itafuata. Lakini hapa nimetumwa rasmi na wananchi wa Mbeya kwamba nikuombe ulione hili kwa jicho la huruma. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atakujalia. *(Makofi)*

Lingine ambalo naomba nizungumze linauwiana  na hilo la shamba. Zamani hili shamba kabla ya kuwa *Iwambi Diary Farm* lilikuwa ni eneo zuri sana kwa ajili ya maua, kabla halijawa shamba la ng'ombe. Lakini najaribu kujiuliza, tusipofanya *planning with convergence,* basi ule uwanja wa Songwe hautakuwa na kazi kama hatutaoanisha shughuli zetu. Mimi naamini uwanja ule tunapewa sio kama *monument* ya kuangalia, tunapewa uwanja ule utusaidie kuibua fursa za kiuchumi zilizoko Mbeya na moja ya furasa hiyo ni pamoja na hilo eneo la Iwambi.

Kaka yangu Nyaulawa alilizungumzia, lakini sasa na mimi naomba niongezee msumari wa inchi sita kwenye hilo. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu uwanja ule sasa uje ufanye kazi ambazo zinatakiwa. Wenzetu wa *DRC* wanaitamani sana Mbeya kufanya biashara, wanasema Dar es Salaam ni mbali. Wenzetu wa Malawi wenzetu wa Zambia wanaiona Mbeya kama *Hub* ya uchumi wa *SADC*.

Tukazane Watanzania sasa badala ya kuangalia misaada, tuangalie *trade* na *trade,* ni pamoja na kuangalia ku-*capitalize avenues* zote. Tuchukue masoko haya yaliyoko *SADC*. Jiji la Mbeya linakwenda kwa kasi! Tunaiomba Serikali ambayo ina nguvu na imara kama hii ya kwetu lazima iwe *facilitative* na hili najua mtatu-*facilitate*. Nitangulize shukrani za awali kwetu sisi waumini. Uwanja huu nilikuwa naomba tuu-*plan* kwa ajili ya kuangalia miaka 50 ijayo.

Jengo lile la kupokea na kuondokea abiria, mimi sidhani kama litakidhi haja. Tunajenga Uwanja wa Ndege ambao ni *International,* bila shaka ndege ambayo itakuwa na abiria mia moja, itaondoka na abiria wengine mia moja. Sasa unabaki unajiuliza jengo lile linaweza likawa-*accommodate* hao, kwa nini tusiangalie uwezekano wa kuweka, *let us think big*. Nafikiri itatusaidia kwa miaka 50, hatutakuwa na sababu tena ya kuhangaika na jengo la kupokea na kuwasafirisha wasafiri. Ninaomba sana nalo hili tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti lingine ni suala zima la Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Kwanza naomba nitangulize shukrani zangu za awali kwa kazi nzito inayofanywa na Madaktari na Wauguzi wa Hospitali ile. Tulikuwa na tatizo la msingi,  Mbeya ilikuwa haina Hospitali ya Mkoa. Kwa hiyo, utakuta shughuli ambazo zilipaswa kufanywa na hospitali ya Mkoa zote zikahamia kwenye Hospitali ya Rufaa. Kwa hiyo, utakuta Hospitali ile pamoja na kuihudumia Mikoa ya Rukwa, Iringa, Ruvuma na Mbeya yenyewe, lakini vilevile imekuwa na mzigo mkubwa kwa ajili ya kubeba shughuli za wananchi wa Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la uhaba wa Madaktari. Tuna upungufu wa Madaktari zaidi ya 35, sasa mtu ametoka Rukwa Kilometa zaidi ya 300, Iringa zaidi ya kilometa 350, anakuja pale anakuta Daktari anayetakiwa amshughulikie ugonjwa

wake hayupo na hii inapelekea kuonekana kwamba Hospitali ina huduma mbovu, kumbe ni kwa sababu ya kuelemewa na mzigo. Wenzangu wale mimi nawafahamu wanafanya kazi kubwa sana. Ni kazi ya wito na kujitolea. *(Makofi)*

Lakini lipo tatizo la hivi karibuni ambalo kidogo tulikuwa na Madaktari bingwa watano tuliletewa pale, hawakuchukua muda mrefu wakaondoka. Siwezi kuingilia taratibu za utumishi, lakini mimi nilikuwa nafikiri kama Daktari anaweza akaja akapewa pengine mafao yote ya uhamisho halafu akakaa kwenye Kituo *hardly* miezi miwili, mitatu anaondoka, mimi nafikiri ni matumizi mabaya ya *resources* za Umma. *(Makofi)*

Hakika kabisa ni matumizi mabaya ya umma. Naamini atakapoondoka tena, hata kama ataambiwa sasa kwa sababu umeomba ujisafirishe, lakini kwa kweli imetuletea matatizo sana na wale Madaktari watano kwa hakika walikuwa mabingwa kweli kweli hawakujali kwamba hawana Ofisi hata kwenye *corridor* waliwahudumia wananchi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili pamoja na Waziri wetu wa Afya mlipatie uzito. Hospitali ile iko ndani ya Jiji la Mbeya, lakini ni ya kwetu wote katika Mikoa minne, naomba mnisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru Serikali vilevile kwa kunikubalia kuitoa Mbeya *Technical College* na kuwa *Mbeya Institute of Science and Technology*. Lakini mimi kwangu, wanasema ombeni mtapewa. Kwangu mimi *MIST* bado tafsiri ya haraka haraka inanipa kama ukungu usoni. Hivi kwanini *MIST* isihame ikawa *MUST*? Neno *MUST* linapendeza *Mbeya University of Science and Technology*. Ndiyo ombi langu hili Mheshimiwa Waziri Mkuu. *Time frame* inaonekana *MIST* itaji *transform* kuwa *MUST* mwaka 2010. Ndugu zangu mbona nimeishi na ninyi kwa wema sana hapa Bungeni? Kwanini mnataka kuninyonga? Hebu kifanyeni kile kiwe Chuo Kikuu basi. *(Makofi)*

Naishukuru Serikali kwa kupeleka Walimu zaidi ya 42 kwenda kusoma nchi za nje, robo tatu ya Walimu hao sasa wamerudi. Ikama ile inatoshereza kabisa kuifanya, maana yake kasi mpya na ari mpya. Kwa hili mimi sina wasiwasi na Serikali hii. Umefika wakati na kwa kuanzia nilikuwa naomba ikiwezekana kiwe Chuo Kikuu cha kwanza cha kupeleka nusu kwa nusu, asilimia 50 wanawake na asilimia 50 wanaume. Tuanzie *Mbeya University of Science and Technology. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshimiwa sana ninaomba nimalizie hili la Madiwani. Mheshimiwa Waziri Mkuu agizo lako hili la kwamba lazima tuhakikishe watoto wanakwenda zaidi ya asilimia 50 mtekelezaji wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa Diwani. Hawa Madiwani Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa hivi wamebeba vyeo vyote vilivyopo ndani ya Kata, ni Mabwana Afya, ni Mabibi Afya, ndiyo Zahanati, wenyewe ndiyo magari ya *ambulance!* Asubuhi anaamka Mheshimiwa Diwani anakuta watu wanamsubiri pale nyumbani. Wanafanya kazi nzito sana! Ninakumbuka iliundwa Tume na Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Lubeleje, sasa kumekuwa kimya mno. Hawa ni wenzetu, ni wadau wetu katika kuleta maendeleo. Ninaomba kwa jicho la huruma, tena kwa kasi inayotakiwa ya Serikali kama hii ya Awamu ya Nne wafikiriwe Waheshimiwa

Madiwani wetu wanafanya kazi nzito wanalihudumia Taifa hili. Ninaomba maslahi yao yaboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na lugha pengine Halmashauri zao zitakaa na kuangalia, lakini zipo Halmashauri nyingine ambazo hata kujiendesha zenyewe haziwezi na ruzuku wanayopewa ni kidogo sana. Sasa nabaki najiuliza, hivi vyanzo vingine tumefuta hawa Halmashauri watawezaje kuwahudumia Madiwani wao? Mimi nilifikiri kwamba ni mgawanyo wa kazi, lakini *is a unitary state.* Hatuna Serikali mbili, ni Serikali moja. Diwani anapotekeleza, anatekeleza ni ya Waziri Mkuu, lakini tukisema Halmashauri zitajijua, Halmshauri nyingine ni hoi mno.

Ninaomba *intervention ya Central Government* katika kuhakikisha kwamba Madiwani nao wanacheza. Ile *quotation* yako Mheshimiwa Waziri Mkuu niliipenda sana. Mimi ni Mwalimu wa Fasihi, niliipenda sana. Basi hata kama huwezi kucheza, uko mbali, ile mirindimo yake ilie sasa na wimbo uwe basi katika huo huo na hawa Madiwani wacheze na mirindimo hii tunayocheza sisi huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangulize shukrani zangu za awali na kama Askofu, niwatakie baraka tele, mfanye kazi yenu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru sana. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hakika wanawake tunaweza, naona umetosha kabisa hapo na kazi ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, kwa ujumla wao, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mwenyekiti Mpya wa Chama Cha Mapinduzi pamoja na wale wote alioteuliwa nao. Mimi binafsi nimefurahishwa sana. Kwa nini nimefurahishwa? Mimi naamini katika mabadiliko. Nahisi mabadiliko yoyote yanaleta maendeleo. Kwa hiyo kwa kweli nimefurahi. *(Makofi)*

Aidha, nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuwashukuru Wanakilindi kwa mshikamano ambao wanaendelea kunipa siku hadi siku. Hakika wananchi wa Kilindi ni dhahabu kwangu. Kwa hiyo, ninawashukuruni sana na ninajua saa hizi wengi wananisikiliza, maana yake wana taarifa ya mchango wangu asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba pia nitoe pongezi na shukrani kwa Tume ya Huduma za Bunge pamoja na Spika, kwa huduma mbalimbali. Nadhani Wabunge mnaona mambo yanavyokwenda kwa kasi nyingine ya tofauti. Kwa hiyo, nimeona ni vyema nikawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayoifanya kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Aidha, namshukuru sana kwa hotuba yake. Kwa kweli kama Mwanachama wa Chama Cha

Mapinduzi ambaye anatoka kwenye Serikali ambayo iko chini ya Chama Tawala, mimi naongezea tu yale ambayo naona yanahitajika kuongezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tangu mwanzo, nitaongea kwa kasi mpya, kwani tofauti na msemaji mmoja aliyepita, mimi wananchi wangu wamenituma nifuatilie Bajeti zote moja hadi nyingine bila kukosa kwa sababu wanataka kuona Kilindi wanatazamwa vipi, na ndivyo nitakavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa haraka kidogo kwa kasi mpya kama nilivyosema. Kwanza kabisa nampongeza Waziri Mkuu kwa msemo mmoja aliousema jana. Hakika amenitia nguvu. Alim-*quote* katika ukurasa wa 10 Henry David Toure, ambaye alikuwa anazungumzia midundo ya ngoma. Hii imenipa nguvu sana. Lakini akahitimisha kwa kusema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne haitakubali mtu acheze mdundo wa tofauti na ule ambao unachezwa na Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nimefurahi sana kwa sababu kauli hii imekuja kwa wakati. Nilivyoanza kazi kama Mbunge pale Kilindi, kwa wasikilizaji msiojua Kilindi iko wapi, haiko Lindi, iko Tanga. Ninaomba niseme, kwa kweli Watendaji na uongozi wa Halmashauri haukunielewa kabisa. Ilifika mahali wakaona kama ninawasukuma sana, kumbe mwenzao ninacheza na mdundo wa Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimekuheshimu zaidi na hitimisho lako kwamba: “Ambaye anaona hawezi, atupishe.” Sasa nasema rasmi kwamba wale Viongozi ambao wananiona mimi ni kero kwa sababu nakwenda na mdundo, kama hawawezi basi kama alivyohitimisha Waziri Mkuu, sitaki kurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wanacheza kwa mdundo ambao ni wa Awamu ya Nne. Hiyo nadhani ni dhahiri, kila mtu anaona na kasi wanayokwenda nayo na wanavyotekeleza yale ambayo wanayasema. Sentensi hiyo ni muhimu sana, *walk your talk.* Kutekeleza yale unayoyasema. Kwa kweli naomba niwaombe sasa Mawaziri na Manaibu Mawaziri na Watendaji Wakuu wote Serikalini, twende na mdundo. Nasema hivyo kwa maana gani? Wengine tutakuwa tunacheza ngoma halafu ikakolea ikaanza kunoga, tukaanza kucheza kwa kasi zaidi, tukaanza kutofautiana. Nina maana gani? Tunapouliza maswali hapa Bungeni hasa yale ya nyongeza siyo kwamba tunataka kukomoana au kufanya nini. Ni kwamba tumetumwa na wananchi tuje tuulize. Sasa msituangalie kwa jicho la tofauti ndugu zangu. Chezeni ngoma inavyotakiwa ili twende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwezi uliopita nilikwenda kwenye Ofisi ya Waziri mmoja nikamwambia Sekretari wake sina *appointment*, lakini nina shida ya haraka sana, naomba kumwona Waziri. Akaniambia kwa kweli kwa leo hawezi kukuona. Nikamsihi utadhani Mbinguni, hata kuingia mbinguni nadhani ni nafuu. Akaniambia haiwezekani kabisa. *Pressure* imempanda. Nikasema anangoja nini Ofisini, si aende

nyumbani!  Sasa nimeelewa mdundo wa ngoma unakwenda kwa kasi kidogo, anashindwa ku-*cope.*

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nikuhakikishie wapo Mawaziri ambao kwa kweli niseme wanaanza kucheza mdundo vizuri. Nimseme tu mmoja, kwa kweli nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomtaja, lakini Mheshimiwa Hawa Ghasia, yeye wala hatufahamiani vizuri ila tu alikuwa ananisikia hapa Bungeni ninavyolalama kuhusu mahitaji ya wananchi wa Kilindi, basi yeye akaja akanipigia simu akaniambia mdogo wangu kuna hiki, hiki na hiki nenda kafuatilie.  Nimefuatilia na nafurahi kusema tayari nimepata Dola 600. Ninaomba na wengine mcheze mchezo huo, msingoje tuwafuate jamani.  Tuko pamoja hatuwapigi vita wala nini, tunataka twende pamoja kwa manufaa ya Watanzania. Kuna baadhi ya Wabunge wanakuwa waoga, wakati mwingine huwa naambiwa na wewe nawe na Kilindi yako! Ndiyo iliyonileta humu ndani. Sasa wengine wanakuwa wanaogopa kwamba watamchukia. *(Makofi)*

Nakumbuka mzee mmoja nilivyoingia kwenye Bunge la Afrika Mashariki nikawa nalalamika, mbona sasa napigwa madongo? Mbona nasemwa hivi?  Akaniambia mwanangu, (sasa hivi amefariki yule mzee sitakaa nimsahau). Akaniambia mwanasiasa kama huna maadui watafute. Fanya kitu uwe na maadui.  Usipokuwa na maadui, kila mtu ni rafiki yako, basi jua hapo kuna dosari. Kwa hiyo, ndugu yangu msiogope, tuseme kweli na tuwe na ushahidi kwa kuzingatia kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye masuala ya Wanakilindi.  Awali ya yote wamenituma niwahsukuru sana Mawaziri ambao wamekuja Kilindi. Kwanza Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kweli huyu alikuja mara tu baada ya kuapishwa kuona hali ilivyo.  Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Luka Siyame.

Naibu Waziri wa Maji - Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kweli alinitia majaribuni. Aliniambia anakuja, tukaandaa kila kitu na mimi nilijua barabara hazipitiki hali ni mbovu, lakini nikataka aje aone. Watendaji wangu kule wakamuarifu barabara ni mbovu Mheshimiwa Waziri huwezi kupita, mimi nikasikitika sana.  Dakika ya mwisho akaniambia siji. Ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri, njooni mpite ndiyo hivyo mtajua jinsi ya kufanya maamuzi mwone yale tunayoyafanya.  Tulimwandalia trekta, tulimwandalia pikipiki, vitu ambavyo mimi napanda kufika kwenye maeneo. Lakini bahati mbaya hakuweza kuja. Kwa hiyo, nawashauri sana Waheshimiwa Mawaziri, njooni msiogope mazingira, ndiyo hali yenyewe, tutaboresha. *(Makofi)*

La pili niishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kweli hususan Mheshimiwa Akukweti, kwa msaada wa chakula wakati wa njaa. Nadhani sakata la Kilindi wengi mliliona. Mkuu wa Wilaya anasema hakuna njaa, mimi napita nakuta wananchi wanakula mizizi, wengine wamedondoka. Lakini nawashukuru sana kwa busara zenu, Serikali iliweza kuleta chakula. *(Makofi)*

Aidha, nichukue fursa hii kuishukuru Kampuni ya *Tanga Cement* kwa msaada wa chakula walichotupa na Bwana *Venon Fernandes* wa *Agape Television* ambaye alileta

chakula kwa ajili ya mashule yote. Katika ukurasa wa 12 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba kila kaya ihamasishe kuweka akiba ya chakula. Ninaomba wataalam waje kule kwangu kwa sababu kwa kweli Maafisa Elimu nilionao ni wachache mno. Naomba sana waje tusaidiane. Hata mimi nilikuwa nafikiria jinsi ya kuweka Benki ya Chakula kwa sababu Kilindi tunalima sana. Kwa hiyo, nitaomba sana huo msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, kwa kweli nasikia uchungu kuzungumzia barabara. Wilaya ya Kilindi hata ukiangalia kwenye Bajeti, sijui kama utaona mahali kuna barabara yoyote, na tunaishi kule tuko watu wengi na tuna barabara nyingi. Barabara ya *TANROADS* ni kaeneo kadogo tu kutoka Handeni mpaka Kibirashi, hata hiyo nayo hawaiangalii. Lakini hatuna barabara nyingine yoyote inayogharamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyowaambia, wakati wa Masika hii wanaanchi walikuwa hawana basi, hakuna gari inayotembea kwenda kule. Kwa kweli inasikitisha. Barabara zinatengenezwa hata zile za Halmashauri kwa kiwango cha chini mno. Wale Mawaziri, akina Mheshimiwa Pinda waliokuja, wanaelewa nasema nini. Kiwango cha chini kabisa! Sasa mimi sielewi kwanini unakuta barabara tatu, nne zinatengenezwa kwa wakati mmoja, halafu zote ni kwa kiwango cha chini. Sasa hivi ukifika hazina maana. Badala ya kusema tuchukue barabara moja, tu-*concentrate* nayo kutokana na fedha tulizonazo, wanajenga barabara nne kwa kiwango cha chini kabisa. Kwa hiyo, hili suala naomba liangaliwe. Tumepeleka maombi Wizarani tangu mwaka 2003 kuomba *upgrading* ya barabara, mpaka leo bado. Kwa kasi mpya naamini litawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumzie kuhusu wafugaji. Asilimia 40 na zaidi ya wakazi wa Kilindi ni wafugaji. Kwa kweli wakati wa kiangazi ndio utajua hawa watu wana shida kiasi gani. Wanahama kabisa. Fikiria wazee, akina mama wajawazito na watoto watoto wadogo, lakini inabidi wahame kwa ajili ya makazi au mifugo yao na hata wao wenyewe kwa sababu maji yanakuwa hayapo. Ninaomba Serikali jamani mtuangalie kwa jicho la huruma muweze kutupa msukumo zaidi. Siyo yote ambayo ninayajua au wao wanayajua ambapo tunaweza tukafuatilia, lakini mnaweza mkatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji, tunashukuru. Lakini jamani, tumepewa eti Mkandarasi mmoja kwa miradi zaidi ya 10 ya Vijiji. Mkandarasi mmoja huyo huyo anapita, eti naambiwa yupo na Wilaya nyingine anafanya kazi. Halafu huyu huyu mmoja ajengee visima vyote hivyo! Kweli inawezekana! Naona haiwezekani. Kwingine nako utapeli, hakuna usimamizi. Mambo yamekuwa magumu, unashangaa unakuta mabomba ya zamani yanang'olewa kwenye njia ya zamani ndiyo yanaunganishwa yanakuwa mapya. Juzi amekamatwa mtu mmoja amepigwa, amefanywa nini, lakini ninaomba Serikali iingilie kati. Ninakwenda haraka kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ardhi. Jamani, kuna neno "Kilindi bwerere"! Watu waende jamani, ardhi tunayo, lakini hebu kwanza wale mnaohamasisha watu kuhamia Kilindi, njooni mwangalie, ardhi inawatosha hawa watu? Muelewe hizi jamii zinakua, wale watoto watakuwa na Miji yao hasa mnavyoleta watu wengi wanalundikana, iweje? Ndiyo maana tunakuwa na migogoro mingi sana ya ardhi kule.

Aidha, ninaomba mipaka yetu ijulikane ya Wilaya. Mpaka sasa hivi hatuelewi mipaka ni ipi kwa sababu mipaka ambayo tunayo kwenye *GN* tunaona ni tofauti kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hospitali. Hatuna Hospitali. Lakini tunaomba *Ambulance* kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi tuna Kituo cha Afya kidogo tu kimoja kiko Songe, hicho ndiyo kinachohudumia wote. Tunguli kuna Kituo kingine cha Afya lakini hata jana waliopita pale wanasema kwa kweli unafika Hospitali unajua tunakaribia Hospitali unafikiri unafika *Mortuary* jinsi kulivyokuwa hovyo, kunanuka, kuchafu hakuna huduma.

Aidha, katika Zahanati zetu zote watumishi ni *Nursing Assistants*, nadhani mnaelewa nasema nini. Hao ndiyo, Madaktari na ndiyo Waganga wenyewe, nimekuta mtoto ameandikiwa *Fansida*, vidonge viwili kutwa mara tatu. Mganga huyo kaandika, lakini ni kwa sababu hatuna *man power* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye suala la Watendaji, maana hili ni muhimu. Kweli kabisa mimi naomba niseme na niungane mkono na wengine, jana Mheshimiwa Malecela amesema kwamba twende kwenye Vikao. Sasa vikao hujui ni lini, kwangu mimi Vikao vinaahirishwa kila siku nikaona kwamba labda nitoe taratibu yangu ya kazi ile siku ambayo ninaondoka ndiyo kesho yake kinaitishwa Kikao, lakini kwa sababu Madiwani tupo pamoja, unakuwa unaarifiwa. Ukifika kwenye Kikao, nakumbuka, nitoe tu mfano halisi, tunaambiwa tupitishe Bajeti. Kamati ya Fedha milioni 303 Januari – Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasimama pale nikasema kama Mbunge. “Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua matumizi yakoje.” Unajibiwa na Mtendaji Mkuu, anakwambia tafadhali Mwenyekiti, huyo anataka kuyumbisha Kikao. Kazi ya kusema matumizi ni kazi ya *Internal Auditor.* Sasa, kwa sababu mara nyingi Madiwani wengine wanatishika na zile jeuri na kauli za Watendaji Wakuu, basi unakuta kwa kweli wanashindwa kuuliza kitu kingine. Ninaomba sana jamani, Kilindi tutazamwe. Mambo siyo kama mnavyoyaona, mtaendelea ninyi kucheza ngoma Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi wenzenu tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suala la madini, nashukuru juzi nilipata majibu, tayari tumeandaa mkakati, tumeweka Wakili na sasa hivi mtasikia Viongozi fulani Watendaji Wakuu wanakwenda Mahakamani. Lakini hilo tunashukuru Serikali imetupa mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu jamani viongozi wa kwenye Wilaya waache vitisho. Jamii nyingine hazijui haki zao. Kwa hiyo, tunawaomba waache vitisho. Halafu kazi ya Afisa Usalama ni kazi kama kazi nyingine, isiwe sababu ya kuwatisha wananchi. Kwa hiyo, hilo nalo nimeona niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, naomba niseme, tuna Mbuga ya Wanyamapori ambayo kwa kweli ina wanyama wengi, watu wanaingia na kuvuna kama vile haina mwenyewe. Hii inafuatana na ile Mbuga kutoka Simanjiro ya Kabojo, lakini kwa sababu mpaka uko mbali sana, upande wetu wanaingia wanawinda wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana yake muda sina, uwezeshaji kwa wananchi wangu. Kwa kweli wananchi wa Kilindi wanahitaji kuwezeshwa hasa akina mama na vijana wapewe elimu ya biashara. Nilikutana na mama mmoja anauza mahindi, nikawambia hebu naomba haya mahindi yote, utauzaje? Akaniambia mwanangu, mbona huo ubinafsi? Nikikuuzia yote, watu wengine nitawauzia nini? Ina maana hawaelewi hata mbinu za biashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, naomba jamani Wizara husika ziweze kutusaidia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, nimepata taarifa tunapewa Kituo cha Polisi, tuna *Police Post* tu ndiyo ya Wilaya. Naomba jamani Usalama wa Raia mtuangalie na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkutano wako mmoja na Mawaziri wako naomba mje mfanyie Kilindi itawasaidia kufanya maamuzi sahihi, maana yake maamuzi mnayoyafanyia Dar es salaam na Dodoma, hayazingatii hali halisi ya kule tuliko sisi. Wananchi wa Kilindi wanaona kama mnaongelea nchi nyingine, siyo kwao. Kwa hiyo, ninaomba sisi tutagharamia chakula na malazi, msijali, lakini mtalala wapi? Lakini mtalala na mtaamka na chakula mtakula, lakini muweze kuona hali halisi na upande wa pili wa Tanzania jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kama mtumishi wa Serikali wa muda mrefu, naomba niseme, mara nyingi tumekuwa tukisema Watendaji na watumishi wa Serikali wabovu, hakuna watumishi wa Serikali wabovu. Ila wakati mwingine Viongozi ndiyo wanatuyumbisha na taratibu zenyewe zilizopo. Fedha hazitoshi na wakati mwingine Viongozi wengine wamekuwa tishio. Nimekuwa Mtumishi wa Serikali miaka 23, ninaelewa ninasema nini na nadhani wao wanaelewa nasema nini. Sisi wa chini ni kwamba tunakwenda na upepo unavyoenda na uoga wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema yote hayo, niseme tena, ahsanteni sana. Kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nawashukuru sana. Niseme tu mambo ya Sekondari, naomba Walimu waje, nyumba zimejengwa kwa viwango vya chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nashukuru, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID SINANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo nami nipate kuchangia katika hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nami nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Nampongeza sana pamoja na timu yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ningependa kutoa shukrani kwa Serikali kwanza, ya Awamu ya Tatu na pili; kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Shukrani hizi ni

kwa sababu sisi wananchi wa Mtwara tulikuwa na matatizo makubwa ya barabara ya kutoka Kibiti – Lindi na matatizo ya daraja. Lakini kwa hivi sasa Daraja la Mkapa limejengwa. Tunashukuru sana na barabara ya Kibiti – Lindi inaendelea vizuri. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali kwa kutuletea Mradi wa Umeme wa *Mnazi Bay*. Sasa hivi wananchi wa Kusini Mtwara na Lindi tuna uhakika wa kupata umeme. Kwa hiyo, nalo natoa shukrani. Pia, nisingependa kumsahau Mheshimiwa Shirima ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara kwa kusimama kidete katika utekelezaji wa mradi huu na nadhani yuko hapa, naomba apokee shukrani zetu kwa niaba ya wananchi wa Mtwara. Pia, Mheshimiwa Saddiq naye alikuwa pamoja wakati huo alikuwa *DC* wa Mtwara naye alishirikiana naye katika kufuatilia mradi huu wa umeme na nadhani ndiyo maana amepandishwa cheo sasa kuwa Mkuu wa Mkoa. Pengine hiyo ni moja ya sababu. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Mtwara Mjini kwa kunichagua ili niwawakilishe katika Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, sisi wa Mkoa wa Mtwara tuna matatizo makubwa. Tukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, inatutia moyo hasa hiki kipengele ambacho msemaji aliyepita amekigusia. Naomba kunukuu: “Serikali ya Awamu ya Nne haiwezi kumwachia kila Kiongozi wake au kila Mtendaji kusikiliza na kucheza ngoma anayoipenda. Tumeahidi maisha bora kwa kila Mtanzania, tutatekeleza ahadi hiyo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Asiyeweza kucheza ngoma hiyo kwa midundo inayopigwa na Serikali itabidi atupishe.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kauli hii ingekuwa nje kabisa katika jalada la Kitabu hiki. Ni kauli ambayo kwa kweli itasaidia sana. Nadhani watu itabidi waeleweshwe na waielewe. Kauli hii ndiyo nadhani itakuwa ni dira ambayo itatupeleka mbele zaidi. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, watu wa Mkoa wa Mtwara wamekaa nyuma sana kwa muda mrefu kimaendeleo. Hii sio siri, nchi nzima inafahamu, Serikali inafahamu. Sasa hivi imepata faraja kwa kauli ya Serikali iliyosema kwamba Mikoa ya pembezoni sasa hivi itapewa kipaumbele ukiwemo Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, wananchi wa Mtwara wamepokea kauli hii kwa mikono miwili na kwamba wana imani kubwa kwamba kauli hii itatekelezwa ili tuondokane na matatizo ambayo tunayo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara ina miundombinu na maliasili ya kutosha ya kuweza kutupeleka sisi katika maendeleo makubwa. Mkoa wa Mtwara una Bandari nzuri kupita zote katika nchi hii kwa maana ya kina kirefu. Bandari hii ina kina cha mita kumi. Inaweza ikapokea meli tatu zikafunga gati za kimataifa na meli sita zikawa katika Ghuba, katika *Bay* ile ya Mtwara pale Bandarini. Ina *facilities* zote, ina *container handling facilities*, ina ma-*shade* makubwa manne ya kuhifadhi bidhaa.

Hivi majuzi imefanyiwa *heavy duty paving* ya *container terminal*. Inaweza ikaweka *container* 1000. Lakini hivi sasa, hivi ninavyozungumza ukienda katika Bandari ile hamna hata *boat*, acha meli, hakuna kitu, hakuna kinachofanyika. Bandari hii imekaa kwa muda mrefu haina kazi. Inafanya kazi wakati wa msimu wa korosho. Meli ikija inapakia korosho na wiki tatu zimepita meli imeleta tani 2000 za *sulphur*. Sasa hivi unaweza ukatandika jamvi pale ukasoma *Maulid*. Bandari hii yenye hadhi na heshima kiasi hiki haina kazi. Bandari hii ingeweza kuchangia kipato cha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nishauri kitu kimoja kwamba badala ya watu wa Ruvuma kusafiri Kilomita 1000 kuifuata Bandari ya Dar es salaam, ingekuwa ni busara kwamba wangesafiri kutoka Songea kwenda Mtwara Kilomita 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari hii iko Kilomita 600 kutoka Ruvuma. Iwapo Serikali itatilia maanani barabara hii kutoka Songea – Tunduru – Masasi – Mtwara, basi Serikali pia itaeupukana na gharama kubwa ambazo sio za lazima za usafiri. Wataalam wa uchumi wakifanya mahesabu, naona watakuta kwamba Serikali itakuwa imeokoka kwa gharama za mafuta ambayo yananunuliwa kwa fedha za kigeni na uchakavu wa magari *(wear and tear)*. Bandari hii inaweza ikachukua mazao ambayo yanapatikana katika Mkoa wa Ruvuma. Kwa hiyo, Bandari hii ingekuwa ina kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna mambo mawili, wananchi wangepata ajira, Bandari ingekuwa inafanya wajibu wake na pia kupunguza gharama za kusafirisha mazao kutoka Mkoa wa Ruvuma na Wilaya zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba sasa hivi pamoja na miundombinu tuliyokuwa nayo, umeme wa kuaminika naamini kwa muda mfupi utapatikana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwashawishi Wawekezaji waje waweke viwanda Mtwara ili Bandari itumike kikamilifu. Hatuna viwanda, kuna kiwanda kimoja cha korosho, vingine navyo vinakarabatiwa, lakini havitoshi. Tunaomba Serikali sasa ipige *about turn*, itutazame na sisi huku Kusini. Tumepiga kelele kwa muda mrefu, tunaomba Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, baada ya hii Bandari, kuna Uwanja wa Ndege. Uwanja huu ulijengwa na Wakoloni. Mwaka 1965 ukapanuliwa na sasa hivi una mita 2258. Uwanja huu sasa hivi hautumiki kikamilifu.

Tunashukuru Kampuni ya *Precision* kwamba hivi sasa nao wameanza safari za kwenda *Mozambique*, kwa hiyo utatumika kidogo. Uwanja huu ulikuwa na taa, sasa hivi taa zimeng'olewa. Tunaiomba Serikali, Uwanja huu ufanyiwe ukarabati ili nao uweze kukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uvuvi. Tunawataja hapa wakulima, ni jambo zuri, lakini wavuvi nao naona hawajapewa uzito wao. Wavuvi hawa mpaka sasa hivi wanatumia zana za kizamani, mitumbwi ya kizamani. Mtwara kumetengenezwa *Marine Parks*, Sasa hivi inabidi waende wakavue mbali. Bila *boat*, wavuvi hawa hawawezi kufanya kazi vizuri. Hawawezi kuvua na kuinua hali zao za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Mikindani ambacho kilikuwa kinatengeneza maboti kimekufa, tunaomba Serikali ifufue kile kiwanda. Kulikuwa pia na kiwanda cha kutengeneza vinoo vya barafu nacho kimekufa. Tunaomba nacho kifufuliwe. Kwa hiyo, wavuvi hawa tunaomba wasaidiwe kwa sababu maeneo mengi yametengwa kwa ajili ya *Marine Parks*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara pia ingeweza kuchangia pato la Taifa kwa utalii. Mtwara kuna fukwe nzuri kama zilizoko katika sehemu nyingine za nchi hii. Lakini hatuna Hoteli ya Kitalii. Tunaweza kusema hatuna hoteli kabisa. Lakini, kuna fukwe nzuri, kuna *Marine Parks*, kuna hifadhi za wanyama, kuna vivutio vya kila aina. Kuna Miji ya kizamani kama Mikindani ya kihistoria.

Tunaomba Serikali nayo itilie mkazo katika suala la utalii. Kwa sababu mtalii anaweza kuja akatumia Bandari, anaweza akatumia ndege, anaweza akatumia gari kwa njia zote mtalii anafika Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninaiomba Serikali pia itilie maanani juu ya mahusiano kati ya Tanzania na Msumbiji. Kutoka Mtwara Mjini mpaka Mto Ruvuma ambao ni mpaka, ni kilomita 40 tu, sio mbali sana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itilie maanani hilo.

Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Benjamini William Mkapa alipokuwa akiweka Jiwe la Msingi wa Daraja la Umoja, alitoa kauli na mwenzake Mheshimiwa Gebuza, Rais wa Msumbiji wakakubaliana kwamba hapatakuwa na *Visa*, lakini bado *Visa* inaendelea, kwamba wananchi wa nchi mbili hizi watasafiri bila ya *Visa*. Tunaomba hili nalo Serikali walifuatilie. Kwa kufanya mahusianao kati ya Tanzania na Msumbiji, biashara ikiwepo, wananchi nao watapata manufaa na sisi kidogo tunaweza tukasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mtwara ni watu masikini sana. Tunashindwa hata kuchangia maendeleo yetu. Tunaomba Serikali itusaidie kuhimiza wawekezaji waje kuwekeza, vinginevyo umeme huu ukishakuwa tayari, utakuwa hauna kazi kama ilivyokuwa Bandari sasa hivi haina kazi, Uwanja wa Ndege hauna kazi. Umeme tutagandisha *Ice cream* tu badala ya kufanya mambo ya maana na barabara hii hata ikiisha, watakuja Mtwara watarudisha chupa tupu za soda na chupa tupu za bia. Itakuwa haina maana. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itusaidie kututafutia Wawekezaji muwaelekeze waje kule vile vile. Tuna miundombinu yote, tuna Uwanja wa Ndege, tuna Bandari, tuna umeme, lakini, Mtwara hakuna viwanda, kumezorota!

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kilimo, tuna kituo kizuri na kikubwa cha Naliendele, Kituo cha Utafiti wa Kilimo. Kituo hiki kuna wataalam kadhaa na wanakwenda katika nchi mbalimbali. Sasa hivi ninavyozungumza kuna Mtaalam mmoja amekwenda Ghana kuwasaidia. Wanatoka Kituo cha Naliendele cha Mtwara. Lakini kilimo kiko nyuma kabisa. Wananchi wanalima kwa jembe la mkono. Tunaomba Serikali itusaidie, vile vile itutafutie matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa kuanza kabisa, napenda kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kushinda kwa kura nyingi sana za kihistoria kuwa Rais wa nchi yetu. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushinda na kuchaguliwa kwa kura nyingi kutoka ndani ya Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Nampongeza sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge hili ukiwemo wewe mwenyewe, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Kiongozi wetu ndani ya Bunge hili.

Lakini pia nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwa heshima kubwa walizonipa mimi mwenyewe na heshima kubwa walizokipa Chama Cha Mapinduzi ili tuweze kuwa Viongozi ndani ya Bunge hili kwa miaka mitano ijayo. Kwa maana hiyo, namwomba Mungu awabariki, awape mvua za kutosha na wapate kuvuna mazao mengi na uchumi wao ukapate kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kutambua ugumu wa maisha ya wafanyakazi wake, kwa maana hiyo kuamua kuongeza mishahara. Mishahara ya Serikali kutokana na hotuba ya Bajeti, itaongezwa. Naamini itasaidia sana kupunguza makali ya maisha ya wananchi na wafanyakazi wa Taifa hili. Lakini pia nimefurahishwa sana na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais, juu ya upandishaji wa mishahara ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Askari Polisi ni kazi ngumu, ni kazi za hatari. Lakini, Rais wetu baada ya kutambua hili, alieleza kwamba katika Bajeti ya mwaka huu atahakikisha kwamba mishahara ya Askari Polisi inapanda. Kwa maana hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza na pia nina kila sababu ya kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa namna walivyolishughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hili ni ombi. Ningependa Serikali itafakari kwa makini sana namna ya kusaidia Wanajeshi walioko mipakani. Wanaishi katika mahandaki kwa miezi sita, lakini hawana posho yoyote ambayo inawasaidia kuishi katika mazingira hayo magumu. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iangalie jambo hili kwa makini sana. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, najua matatizo yao wanayoyapata huko mipakani. Kwa hiyo, hapa nawasemea kwamba hawana posho yoyote wakati wanakaa huko katika mahandaki. Naiomba Serikali ijaribu kuona ni kwa namna gani itawasaidia Askari Jeshi hawa ili wajikimu huko waliko. Mshahara wa Askari huyu sio mkubwa sana, agawe, autumie yeye huko porini, sehemu nyingine atumie kwa familia yake, ni kweli kwamba maisha yao ni magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niongee mambo ya Jimbo langu la Mufindi Kusini. Mimi kama Mbunge, katika miaka 10 iliyopita nimekuwa nikiiomba Serikali ichukue Barabara ya Nyigo – Mgololo, barabara ya Kilomita 60 tu. Ni barabara inayokwenda katika kiwanda kikubwa kabisa cha *SPM* Mgololo. Bodi ya Barabara ya Mkoa katika kipindi cha miaka 10 imekuwa ikiiomba Serikali ichuke barabara hii. Barabara hii inapita Wilaya ya Mufindi - Njombe - Mufindi – Njombe, haina mwenyewe! Haina mwenyewe kabisa! Lakini kwa miaka yote imekuwa ikihudumiwa na Wilaya ya Mufindi.

Sasa namwomba sana Waziri wa Miundombinu aliangalie jambo hili. Nimeambiwa kwamba iko Kamati imeundwa ya kuchunguza barabara zote za kitaifa. Nawaombeni sana muichukue barabara hii. Umekuwa ni mzigo mkubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Mufindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinazotolewa katika Wilaya hazitoshi. Barabara hii ni muhimu sana. Wanasema sijui kuna barabara nyingine, sijui ile barabara inayopita kule milimani, ile milima ni mikali sana, inahatarisha maisha ya madereva, ina hatarisha maisha ya magari. Kuna wakati waliandika kibao pale, magari yaliyodondoka, magari makubwa yalikuwa ni zaidi ya 13. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali itilie umuhimu sana barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni umeme. Ninavyo Vijiji viwili pale, kimoja kinaitwa Mninga, kimoja kinaitwa Kihanga. Vijiji hivi viko kiwanda cha kutengeneza nguzo ambazo zinatumika Tanzania nzima. Lakini wale wananchi wa Vijiji vile hawana umeme. Sasa, wakaanza kusema Mheshimiwa unaona, sisi tumeanza kupinda migongo. Nikauliza, kwa nini? Wakasema hatuangalii huko juu, maanake tunapata uchungu, nyaya zimepita pale kwa miaka kumi iliyopita, lakini wenyewe hawana umeme. Sasa, mimi kule siwezi kwenda kufanya Mkutano leo wa hadhara. Mpaka wananiambia, hivi wewe Mheshimiwa, huko Bungeni wewe unaongea nini? Kwa nini hawakusikii? Labda ukatoe machozi mle ndani ya Bunge labda watakusikia. Mheshimiwa Msabaha Sijui kama yupo. Lakini nashukuru ameniandikia *note* sasa hivi, anasema Mheshimiwa Malangalila baada ya Kikao hiki twende tukaongee ofisini kwake. Labda atanisikia. Lakini nitamwomba Mungu, kabla sijakwenda kule, nasali kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nataka kulizungumzia sasa hivi ni kuhusu Kiwanda cha *MPM*. Hapo mwanzo kilikuwa kinaitwa *SPM*, sasa hivi kinaitwa *MPM (Mufundi Paper Mills)*. Mimi kama Mbunge, katika kipindi cha miaka kumi nimekuwa nikizungumzia sana Kiwanda hiki, nimekuwa nikiiomba sana Serikali itafute mwekezaji katika Kiwanda hiki. Siku niliposikia mwekezaji amepatikana, nilifurahi sana kwamba Mungu amesikia kilio chetu. Wasiwasi wangu mkubwa haikuwa kwamba Kiwanda kile kinasaidia uchumi wa nchi tu, bali ilikuwa ni hifadhi ya mazingira katika kiwanda kile kwa sababu Kiwanda kile kinatumia madawa yenye sumu kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposikia mwekezaji amefika, nikafurahi. Sasa mwekezaji mwenyewe huyu sasa ameanza mambo ambayo mimi na wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini tumeshindwa kuelewa na naamini kabisa na ninyi mtakaposikia hapa

hamtamwelewa. Mwekezaji huyu ana *General Manager* wake anaitwa Sichodili, ni Mhindi. Anatumia madawa makali, zile takataka za uzalishaji anazitupa ovyo. Pale kuna mto mkubwa sana unaopita unakwenda Kilombero na Rufiji huko. Wakati wa mvua zile takataka zinavuja zinaingia kule mtoni. Sasa ndugu zangu wa Kilombero na Rufiji, nawapeni pole tena sana. Amekuwa akishauriwa, bwana eeh, zamani kulikuwa na *treatment plan,* tumia *treatment plan* kutibu hayo madawa ya sumu ili yasilete madhara kwa wananchi, haelewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine pia ambalo ningezungumzia hapa, huyu Mhindi huyu ni mbaguzi. Kwa sababu gani nasema ni mbaguzi? Akishauriwa na watu weusi anawaita mbwa, halafu akishauriwa zaidi anasema mimi Serikali yenu hainifanyi chochote kwa sababu Viongozi wote wa Serikali wako mikononi mwangu. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, uko hapa na wewe uko mikononi mwa huyo Mhindi. Nakupa pole Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa mimi ningependekeza iundwe Tume. (*Makofi*/*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, kanuni gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Kifungu cha 50.

**MWENYEKITI:** Naomba Mheshimiwa Mbunge ukae chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Kifungu cha 50. Ningependa tu kumwomba Mheshimiwa Mbunge, haya aliyoyasema ni mazito na ni vizuri akayathibitisha. Tunachomtaka athibitishe; moja, kauli hiyo kama huyo Mhindi ameyasema, maana kama aliyasema na una ushahidi, basi kayasema yeye. Lakini kama hakuyasema na huna ushahidi, basi tunakuomba ama ufute ama utuletee uthibitisho, maana ni maneno mazito ambayo yanataka uthibitisho.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hicho kweli kinatoa maelezo haya kama yalivyobainishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri (Mheshimiwa Juma J. Akukweti). Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, kutokana na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri athibitishe kauli hiyo hapa ndani ya Bunge ama aifute kama hana uhakika nayo. Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. BENITO B. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa ushahidi baadaye.

**MWENYEKITI:** Endelea na tunasubiri ukabidhi ushahidi wako kwenye Meza ya Spika ukiwa kamilifu, vinginevyo hatua zitachukuliwa dhidi yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hii pia inakutaka Kiongozi wetu umpe muda, maana hivyo ulivyoacha anaweza kuchukua miaka mitatu kutafuta ushahidi. Sasa apewe muda wa kutoa ushahidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kukumbusha hilo. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge, ndani ya siku saba uwe umeshakamilisha ushahidi wako na kuuweka Mezani kwa Spika na vinginevyo kama ushahidi huo hautakuwa na ukweli, basi Kanuni na taratibu za Bunge zitafuata utaratibu wake. Naomba uendelee na maelezo yako. *(Makofi)*

**MHE. BENITO B. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba maneno niliyoyasema ni ya kweli na kwa sababu yatanichukua muda mrefu, naomba kufuta haya niliyoyasema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa wakati ukitoa maelezo hayo ulikuwa umeshafanya utafiti na kuwa na uhakika wa kitu unachokisema, sipendi kurudia taratibu za Bunge. Ndani ya siku saba tunaomba ukamilishe ushahidi wako na kama unaendelea na hotuba naomba uendelee. Kama umeshamaliza hotuba yako, naomba niendelee na ratiba yangu.

**MHE. BENITO B. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge amefuta hoja yake. Mheshimiwa Waziri naomba tuendelee na ratiba. Mheshimiwa Mbunge tuendelee, kama bado unaendelea na kuchangia hoja hii.

**MHE. BENITO B. MALANGALILA:** Mheshimiwa mwenyekiti, nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Basi, tuendelee. Anayefuata ni Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ajiandae.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bismillah Rahman Rahim. Ahsante sana kwa kunipa muda mchana huu nami niwe mmoja katika wachangiaji wa hoja iliyokuwepo mbele yetu. Kabla sijaendelea na kuchangia, naomba kwanza niunge mkono hoja hii kwa asilimia zote na kuiafiki.

Baada ya hapo, kama walivyotangulia Wasemaji waliopita, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne kwa kura zote isipokuwa moja tu kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa uchaguzi uliofanyika juzi hapa Dodoma. Vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na mapema kabisa kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais, pamoja na Viongozi wengine katika kuliendesha gurudumu la uongozi katika Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaishia hapo, bali nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti ambao wanachukua nafasi hii kuongoza Baraza hili kwa ufanisi kabisa bila ya upendeleo na bila ya kujali. Inadhihirisha jinsi gani hapo Mwenyekiti ulivyokuwa na msimamo. Nakupongeza sana kwa jinsi unavyoendesha Kikao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila ikiwa sikuchukua nafasi hii kuwapongeza Wapiga Kura wa Mkoa wa Kusini Zanzibar, hususan Wapiga kura wa Jimbo langu la Muyuni kwa ushindi wa kishindo waliokiletea Chama Cha Mapinduzi hadi kufikia kuzoa hati tano za utendaji mzuri katika Chama cha Mapinduzi kuanzia siku ya uchaguzi mpaka katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambacho ndiyo Chama Tawala kwa Tanzania kwa muda huu. Nawapa hongera sana Watendaji pamoja na wananchi wa Mkoa Kusini Unguja na Jimbo la Muyuni kwa kazi yao nzuri wanayoitekeleza katika Awamu hii ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, naomba nizungumzie masuala machache kuhusiana na Bajeti yetu hii ambayo kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba ambayo kwa kweli tungesema haina cha kuongezea, lakini siyo binadamu. Binadamu ni lazima anapopata kitu palipo pazuri asifu, palipokuwa siyo aongezee ili kufikia lengo na madhumuni yaliyokusudiwa.

Naamini kabisa kwamba hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukilinganisha na hotuba ya Bajeti ambayo tumeipitisha juzi, zinakwenda sambamba. Kwa uzoefu wangu na kwa jinsi ninavyoona, naamini kabisa kwamba haya yaliyozungumzwa katika hotuba hii yamechujwa ipasavyo, ni ya uhakika na yataendelezwa kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo, nizungumzie kuhusu suala la Muungano. Kama ilivyozungumzwa katika ukurasa wa 22 na 23, ingawa kuna Msemaji hapa mmoja aliyepita wakati alipokuwa ananukuu alifupishafupisha, hakuinukuu kikamilifu kama ilivyoandikwa. Kwa hiyo, ningeomba kwa ruhusa yako ninukuu maneno ambayo aliyazungumza Mheshimiwa Rais na yamerudiwa tena kwa kunukuliwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusema: “Tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya uchumi na jamii ya Zanzibar, bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo siyo ya Muungano, lakini naamini uchumi ambao ni mkubwa zaidi una wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar ambao ni mdogo.”

Hii ni kauli ya Serikali na mara zote Serikali inapotoa kauli haitoi kauli kwa kutania, inatoa kauli kwa nia na madhumuni hasa ya kuendeleza lile ambalo liko mbele yetu. Kwa hiyo, labda niwasaidie wale wenzetu ambao wana wasiwasi.

Sisi Chama Cha Mapinduzi, Chama Tawala, ambao ndio waumini wa sera pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tunaamini wazi kwamba usemi huu uliotolewa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, ni usemi ambao ni sahihi, ni wa kweli na sisi tunaungojea kwa hamu tukiwa kama ni Viongozi kwa kushirikiana na Serikali hii ili

kuona kwamba azma na lengo hili linatekelezwa ipasavyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuhakikishia sisi Wana-CCM, Chama Tawala, kwamba tuko pamoja na tunakuhakikishia kwamba tutashirikiana kuona kwamba lengo hili na madhumuni haya yanatekelezwa ipasavyo bila ya wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba nizungumzie kuhusu ajira na uwekezaji ambayo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia katika ukurasa wa 40 na 41, ninaomba ninukuu kidogo. Amezungumza kwamba: "Serikali katika mwaka 2006/2007 imetenga wastani wa Shilingi milioni mia mitano kwa kila Mkoa kupitia Benki zilizopo kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira nchini. Fedha hizo zinatolewa kwa mtu mmoja mmoja au vikundi kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu kwa kutumia taratibu za kibenki kulingana na uwezo wa kibiashara wa mwombaji." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hii ndiyo azma na lengo, jambo la kusikitisha ni kuona kwamba moja katika suala ambalo linaweza likasaidia katika suala la mikopo, tunapozungumza tukasema mikopo nafuu kwa mtu mmoja mmoja, lakini tukiunganisha na hotuba ya Bajeti kulikuwa na masikitiko ya kuona kwamba Benki zetu wakati tunapowekeza huwa tunapata riba ya asilimia mbili au tatu. Lakini tunapokopa, ikiwa haya ndiyo kielelezo cha kuonyesha kwamba walau na sisi tuondokane na umasikini unachukua riba zaidi ya asilimia 19 mpaka 20, 22 sasa ikiwa kama hii ndiyo hali; je, lengo hili litafikiwa? Kama litafikiwa, Serikali itafanya nini kuona kwamba katika njia hii tukiachilia mbali hizi za Mikoa ya Shilingi milioni 500, lakini kuna wengine ambao hawatazifikia hizi za Mikoa kama watu binafsi, kutakuwa na utaratibu gani? Tungeiomba hapa Serikali iweze kuwa makini na kuona kwamba inalipitia upya suala hili na kuwaona kwamba hawa watu wa mabenki na wao wanakuwa na utaratibu wa kuona kwamba wanakuwa na hali inayostahili ili kuondoa huu umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala lingine ambalo ningependa niongelee leo hapa ni kuhusu ujenzi wa Ofisi za Wabunge. Tukiangalia Ofisi yetu hii ya Bunge Dodoma, Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na Ofisi ya Bunge Zanzibar ni Ofisi ambazo kwa kweli zinakwenda na wakati katika ari mpya, nguvu na kasi mpya. *(Makofi)*

Lakini kitu cha ajabu ni kwamba katika Ofisi zetu za Wabunge, leo kama unapata mgeni anakuja katika Ofisi yako ya Bunge na baada ya kuona hali hii yote ya Ofisi zetu zilivyo, kweli zinakwenda *standard* na *speed* ya Bunge letu? Ningeshauri sana Serikali na Bunge kuona kwamba inachukua kila juhudi ya kuona kwamba ile nia na madhumuni ya kuzijenga Ofisi zetu za Wabunge safari hii zifikiriwe. Kwa kule Zanzibar ambapo itakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi, tungependelea sana, ni vizuri kuwa chini ya Waziri Kiongozi, lakini na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Ofisi ya Bunge ihakikishe kwamba inapitia na kuona kwamba hatua hizi zinakamilishwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda, lakini ningependa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Rais Kikwete kwa jinsi alivyokuwa na juhudi mapema ya kuona kwamba tunaondoa kero za Muungano. Tuna tamaa, tunaamini na tuna uhakika

kwamba kero za Muungano zitakwisha haraka iwezekanavyo. Lakini juu ya yote hayo, kuna mengi hayatasubiri.

Kwa hiyo, tungeomba sana, kwa yale ambayo hayatangojea Tume ilete ripoti kwa mfano suala la *VAT* na bugudha inayotokea kwa wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar wanapokuja Bara, nadhani juu ya kwamba taratibu zipo, tungeomba mapema iwezekanavyo suala hili liweze kufikiriwa ili tuondokane na bugudha hizi. Pia tuondokane na bughudha ya jamaa ambao wanapendelea kuja na magari yao hapa kwamba *registration* ambayo nakumbuka katika hotuba iliyopita, walizungumzia suala hili na kuiomba Serikali kulitazama upya ingawa kweli sheria za magari za Zanzibar, hazihusiani na Sheria za Magari ya Bara lakini *VAT* ni ile ile moja. Kwa hiyo, tungeomba suala hili litazamwe upya ili kuona kwamba bugudha hii inapunguzwa kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli zetu za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niliuliza swali hapa tarehe 20 Juni, 2006 kuhusiana na sarafu zetu. Ningeomba sana Serikali iziangalie sarafu zetu za Shilingi mia moja ambazo zinaonyesha sura za Viongozi wetu. Sarafu hizi jamani mbali ya kwamba ni kuukuu, ni nzuri, lakini tuangalie zinatengenezwa kwa madini gani. Kwa nini hazichukui muda mpaka inafika unaangalia sura za Viongozi humtambui huyu ni Kiongozi gani, kufikia hadi mpaka madukani watu wanazikataa kwamba haitambui kwamba ina sura ya nani.

Kwa hiyo, ningeomba sana hadhi ya Serikali yetu, hadhi ya nchi yetu kimataifa iende sambamba na hadhi na hadhi ya sura za viongozi wetu ambao tunasema kwamba tunawaenzi, zionekane kwamba zinalingana na hali ile kama zilivyo sarafu za wenzetu Kenya hata ikiwa imefukiwa siku mbili, tatu utaikuta vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa dhati yangu nikupongeze kwa jinsi ulivyokimudu Kiti. Umeendesha kipindi cha Maswali na Majibu kwa wakati, lakini ulipotokea msukosuko hapa kidogo umeweza kuutuliza. Nafikiri ni mwanzo mwema, Mwenyezi Mungu akuzidishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sababu zinazonipelekea kuunga mkono hoja hii, moja imelenga ahadi ndani ya Ilani yetu. Lakini pili, imani niliyonayo kwamba kutokana na sifa na ufuatiliaji, usimamizi na kutoa maelekezo aliyonayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina uhakika Bajeti hii kitaifa itakamilika. *(Makofi)*

Lakini nina uhakika na hotuba hii ya Waziri Mkuu kwamba Mkoani kwetu Lindi itafanikiwa kwa sababu tunaye Kiongozi mwenye sifa hizi, Mkuu wetu wa Mkoa, tungeomba mtuachie kwa muda kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo sita ya kuzungumza. La kwanza, barabara ya Kibiti – Lindi. Tunaipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa sisi watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara kuwa na barabara ya lami. Tunawapongeza wale Wachina waliojenga kutoka Somanga mpaka Matandu. Tunawapongeza pia Wachina hawa wanaoanza Nangurukulu kuelekea Mbwemkulu, lakini kwa kweli hatuna raha wala hatuna uhakika na kazi inayofanywa na Kampuni ya Karafu ambaye anatokea Mnazimmoja mpaka Mbwemkulu. *Speed* yake ni ndogo na hatuamini kama kweli anaweza akamaliza katika muda ambao ameongezewa kufikia mwezi wa kumi mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikuja Lindi akatamka kwamba haridhishwi na kazi inayofanya Karafu, akaitwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu Bwana Dr. Makongoro Mahanga na kupewa maagizo mbele ya Mkutano wa Hadhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu naye alifika Lindi na yeye akatamka hilo la kutoridhishwa akamwita Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Mramba. Kilichozungumzwa kwenye Mkutano wa Hadhara na Waziri wa Miundombinu ni kwamba huyu Bwana hashikiki! Kiburi! Sisi watu wa Lindi tumefurahia hiyo kauli, lakini ndio basi hapo hapo, baada ya kwamba hashikiki ana kiburi; kinafuata nini? Lakini kipande cha kutoka Nyamwage mpaka Somanga ni kero kubwa kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Wiki mbili zilizopita, magari 80 yalinasa pale yakiwa na abiria. Wakati haijapata mkandarasi au fedha hazijapatikana, basi utaratibu wa kuzifanyia matengenezo uwepo ili barabara iweze kupitika muda wote. Sisi Wabunge wa Mikoa ya Lindi na Mtwara tunaopita njia ile, tukifika kipande kile tunakuwa hatuna nguo, tuko uchi, maana tunatukanwa matusi ya kila aina na Wapigakura wetu, utafikiria sisi tunafurahia hali ile.

Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali moja imsimamie Karafu, lakini pili kipande hiki cha Nyamwage mpaka Somanga wakati kinasubiri fedha, matengenezo ya kawaida yafanywe ili wananchi wasilale njiani bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni maji katika Mji wa Lindi. Mimi ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, ninapozungumza na mambo ya jumla nina haki. Mji wa Lindi una matatizo sana ya maji. Lakini Mheshimiwa Rais alipofika Lindi alitamka neno zuri sana. Matatizo ya maji Mji wa Lindi suluhisho lake liko Kijiji cha Chipwapwa Jimboni kwangu. Nina uhakika jambo hili litatekelezwa, maana sio rahisi Bajeti hii ya kwanza kuanza kulishughulikia suala lile. Nina hakika Bajeti inayokuja litawekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili likiwekwa kwenye Bajeti, ningeomba vile Vijiji vyote ambavyo maji yatapita kutoka Chipwapwa na hivyo navyo vinufaike na maji haya. Namna nyingine, bomba lile haliwezi likawa salama hata kidogo. Kwa hiyo, ningeomba Vijiji vya Kata za Ng'apa, Kata ya Tanangongolo, Kata ya Lutamba na Kata ya Melola vyote vinufaike na maji haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni Wilaya ya Lindi kutokuwa na Hospitali toka Uhuru. Serikali ya Awamu ya Tatu iliamua kujenga Hospitali ya Wilaya ya Lindi Kitomango. Tukapangiwa Shilingi milioni 300 kwa mwaka 2004/2005. Shilingi milioni 100 zililetwa, kazi ikafanyika. Mwaka 2005/2006 Shilingi milioni 100 nyingine zililetwa kazi imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006/2007 hii Bajeti tunayosoma sasa hivi, nimeangalia vitabu vyote Shilingi milioni 100 siioni ya kumalizia. Sasa tungependa tuelezwe tu kwamba, ndiyo mradi umekwisha kabisa au labda tulizidiwa na mambo, Bajeti inayokuja fedha hizi zitawekwa tena! Tungependa tulifahamu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni umeme. Ndugu yangu Mheshimiwa Sinani - Mbunge wa Mtwara Mjini, amezungumzia. Naomba nitumie nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Dr. Msabaha, ameamua kufika eneo la *Mnazi Bay* kwa miguu yake mwenyewe, siyo kwa nyaraka. Aliamua kukaa na Wabunge wa Lindi na Mtwara na wadau wengine kwa siku mbili kujadili jambo hili na wiki zilizopita tumefikia maafikiano kati ya Serikali, Kampuni ya *ATUMASI*, *TANESCO* na *TPDC*. Ningeiomba Serikali sasa ifikie mahali pa kutoa maamuzi ili gesi ile iweze kuwa umeme na sisi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara angalau tujisikie kwamba tunafaidika na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara na umeme ni chachu ya maendeleo. Vitu hivi vikikamilika, nina uhakika hii habari ya kusema, “kule Lindi!” Hawasemi, Lindi, yaani kama vile mbali sana. Vitu hivi vikikamilika kama azma ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ilivyo, nina uhakika watu wa Lindi tutakuwa katika hali nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu mimi kwa miaka minne mfululizo, wakati ule nilikuwa Naibu Waziri nilikuwa nashindwa kusema, nilikuwa naandika, Dr. Msabaha shahidi yangu, miaka minne nilikuwa naomba umeme kwa Vijiji vyangu vya Ng’apa na Mchinga. Mwaka huu naweza nikapumua hapa, nitaomba kwa kweli Wizara ya Nishati na Madini ivikumbuke Vijiji vya Mchinga na Ng’apa tena Mchinga zote mbili, moja na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano, nataka kuzungumzia habari ya uendeshaji wa Vijiji. Bajeti ya wakati ule, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alitoa tamko kwamba anasimamisha uandikishaji wa Vijiji mpaka baadaye itakapotolewa taarifa tena. Suala hili la Vijiji ni kero kweli kweli, tena ni siasa. Tungeomba hatua sasa zichukuliwe na Serikali ieleze basi wananchi wajue na sisi tujue tukawaambie wananchi, tuendelee kusubiri mpaka lini?

Leo mimi nina Kijiji kama Chilala pale Rutamba, kina Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, kina Shule ya Msingi, Chuo kinachotegemewa na watu wa Wilaya yote ya Lindi Vijijini yenye Majimbo mawili eti bado ni Kitongoji. Nina Kijiji kipo Ruvu Kilomita 15 kutoka Kijiji cha Mamba kinaitwa Kitongoji na kina Shule. Tungeomba suala hili kwa kweli sasa litamkwe ni lini litatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi nazijua aina kuu mbili za uongozi. Aina ya kwanza, kuichukua kasoro kama fursa ya kutafuta njia mbadala kufikia dhamira mliyokusudia, aina ya pili ya uongozi ni kusubiri kasoro, ulalamike na kusahau mengine yote mazuri. Huu ni ulalamikaji. Lakini jana kaka yangu Msemaji wa Upinzani, alitumia lugha nzuri zaidi, sio kulalamika, kupiga kelele. Kupiga kelele kwa Kiswahili cha kawaida, ni kuzungumza maneno yasiyokuwa na maana. Ni *shouting*, sio *arguing.* Hii si sifa ya mtu kuringia kwamba tutapiga kelele, tutapiga kelele.

Mimi nimeangalia huu mgogoro unauzungumziwa huu wa Wakuu wa Mikoa kuwa Wabunge, akaitaja ibara ya 63 ya Katiba, hapana 67 kwamba Wakuu wa Mikoa kujiunga kuingizwa humu Bungeni, ni ukiukwaji wa Sheria Na. 66(3), ndiyo ambayo alikuwa ameitaja wakati ule. Ibara hii lazima isomwe kwa umakini zaidi ili utambue kwamba ibara ya 66 inazungumza akili ya Wabunge, kabla ya mabadiliko ya nne katika Toleo la 80, ibara hii ambayo ilikuwa ibara ya 24 ilikuwa inawatambua Wakuu wa Mikoa kwa wadhifa wao kama Wabunge. Baada ya mabadiliko yale, Mkuu wa Mkoa kwa nafasi, siyo Mbunge. Lakini ibara hii haimzuii Mkuu wa Mkoa kuwa Mbunge. Maana inazungumzia hivyo.

Lakini kwa kujua vile vile kuwa watu wanaweza wakapata matatizo, ibara ya 67(ii)(g) inasema: “Ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi....” Afisa. Mkuu wa Mkoa kwenye Katiba hii haambiwi kama ni Afisa. Ibara ya 61, naambiwa, atakuwa Kiongozi katika Serikali. Huhitaji kuchukua Kamusi kupata tofauti ya Kiongozi na Afisa.

Afisa ni Mtumishi wa Serikali, Katiba inasema Mkuu wa Mkoa ni Kiongozi wa Serikali, anaweza kuteuliwa leo, kesho akaondoka zake. *Terms of Office* ya Afisa wa Serikali sio hivyo, hateuliwi namna hiyo. Kama Waziri ni Kiongozi wa Serikali anakuja Bungeni watu hawashangai. Naibu Waziri ni Kiongozi wa Serikali, anakuja Bungeni watu hawashangai. Mkuu wa Mkoa anayeteuliwa na Rais, yule akija Bungeni nongwa! Anapeperusha bendera! Ndiyo Kiongozi huyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa wa Serikali hapeperushi bendera. Hii tofauti ya kwanza. Lakini ya pili, ukitaka kuisoma Katiba hii uelewe vizuri fungu hilo, ungekwenda vile vile kwenye ibara ya 72(ii). Afisa huyo akitaka kugombea uongozi kwenye Chama cha Siasa, inabidi aache kazi. Wakuu wa Mikoa hawa ni Viongozi wa Siasa tayari, ni Makatibu wa Siasa hawa wa Mikoa, wengine Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taaifa.

Afisa Mwandamizi hawezi kwenda kugombea nafasi hiyo, ukiisoma hii ibara, naomba ninukuu: “(a) Iwapo mtu yeyote mwenye madaraka katika utumishi wa Serikali, madaraka ya aina iliyotajwa katika ibara ya 67(2)(g) ataamua kuwa Mgombea Uchaguzi wa Rais au wa nafasi yoyote chini ya Katiba hii. (b) Kugombea uongozi wa ngazi yoyote katika Chama cha Siasa, kinyume na masharti ya ajira, mtu huyo atahesabiwa kuwa utumishi wake umekoma.” Sio uongozi wake umekoma, “utumishi wake umekoma.”

Hivi kweli Tanzania hapa tulipofikia leo tunashindwa kupata tofauti ya utumishi na uongozi! Kweli tunahitaji kupata *degree* kujua tofauti hiyo! Ni mabadiliko yale yaliyofanywa ya Nne ndiyo yaliyomtoa sasa yule Bwana asiwe Mbunge, lakini hayamzuii Rais kumteua kuwa Mbunge, wala Mbunge hazuiwi kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa. Naomba jambo hili, mazungumzo ya jana, leo, mtu mwingine asije akalizungumza tena. Mimi ningependa niliweke sawa kwa namna hii.

Lakini likazungumzwa lingine jana la ajabu kwamba eti hii habari ya rushwa ni mazungumzo tu ya CCM, hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka Rais wa Awamu ya Tatu aliunda Tume ya Jaji Warioba na akapewa Hadidu za Rejea atafute mianya ya rushwa. Tulikuwa tunakusanya mapato ya Serikali Shilingi bilioni 25 kwa mwezi kabla ya Tume hii haijaundwa, baada ya mianya kugundulika, hatua zilichukuliwa kuziba mianya ile na Rais yule ameondoka anakusanya wastani wa Shilingi bilioni 190 kwa mwezi. *(Makofi)*

Wenzetu hawakuamini kwamba rushwa inachukuliwa hatua, wanataka waone watu wako Mahakamani wameshitakiwa. Jamani na hili kuliona nalo linahitaji *degree*! Lakini kwa sababu wamesema tutapiga kelele, basi kelele tunajua maana waendelee kupiga kelele lakini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ya Awamu ya Nne msikubali kuwa *derailed* watu wanapiga kelele. Nyinyi semeni tu, kelele za mlango hazimzuii mwenye nyumba kufanya nini, kulala. *(Makofi/Kicheko)*

Tungependa kwa kweli tuwe na uongozi wa kusifia jambo jema linapotokea na kukosoa jambo ovu linapotokea ili tuweze kurekebisha. Lakini mimi simlaumu yeyote kwa sababu ukiwa huna la kusema mtu ameku-*tight* kila mahali, lolote unaweza ukasema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu kwa kupewa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwangu mimi kwanza kabisa ningependa kuwapongeza wale wote ambao wamechaguliwa na hususan kwa kumtaja nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa Ndugu Jaka Mwambi kwa kuchaguliwa kuwa Kaimu Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Katika mchango wangu nitaanza na kuchangia na janga la UKIMWI ambalo kwa Wilaya yangu ndiyo linapunguza nguvukazi kwa kiasi kikubwa sana. Lakini kipengele cha kwanza, nipende kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali katika juhudi zake zote za kuwasaidia wananchi wangu wa Makete katika tatizo hili kubwa la UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaje wafutao pia katika kuwashukuru sana kwa michango yao mikubwa ingawa sitaweza kutaja wote. Kwanza, nawashukuru sana *Global Funds* ambao wanatoa michango yao kupitia TAMISEMI. Nawashukuru

*UNAIDS*, *TACAIDS*, *TAHEA*, ambao kwa bahati nzuri Kiongozi wao ninaye hapa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

Pia, nawashukuru *UNECEF*, *NGOs* zote ambazo kwa namna moja au nyingine zimekuwa zikiisaidia Wilaya yangu katika kujinasua tatizo la UKIMWI na hususan zile *NGOs* ambazo Makao yake yako Makete ambazo ningeweza kutaja lakini chache ni mfano *SUMASESU*, *MSF* na nyingine nyingi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo bado lipo, nguvu bado inapungua na tunashukuru kwa hii misaada lakini ukiangalia tatizo kubwa liko kwenye uwiano wa vitu vitatu ambapo tumeainisha wakati wote kwamba ni kupiga vita ujinga, maradhi na umaskini. Kwa hiyo, utakuta kwamba tatizo la UKIMWI Makete ni kama *function* ya tatizo la ujinga na umaskini. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ni kwamba umefika wakati sasa tutoe msaada ambao wananchi wa Makete wataushukuru milele hasa kwa kuwapelekea maendeleo ili waondokane na umasikini kwa kupiga vita ujinga ili waweze wao wenyewe kujinasua na matatizo hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na mkakati sambamba na ile ya kutupatia misaada ambayo bado naishukuru sana, lakini kuwe na mkakati wa kupeleka maendeleo Makete. Kwa mfano mpaka leo hii barabara zetu za Makete hazipitiki. Naomba nimshukuru Naibu Waziri ambaye amefika mwenyewe Wilaya ya Makete na kuona na hususan mwezi wa nne wakati wa mvua karibu siku tatu wananchi wa Makate hawakupata mafuta yakiwa kwenye magari kwa sababu hayakuweza kufika magari kutoka Njombe, kupeleka mafuta Makete kwa sababu barabara iliharibika. Vile vile, katika elimu na sehemu nyingine uwe ndiyo mkakati ambao nadhani hawa ndugu zangu watawashukuru sana Watanzania kwamba wamewakwamua katika tatizo hili sugu la UKIMWI.

Lakini kipengele cha pili, napende pia kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye amewaahidi kuwahudumia watoto yatima. Lakini ukiangalia katika Bajeti ya Waziri wa Fedha, ukiangalia katika hotuba ya Waziri Mkuu hakuna mkakati maalum unaoonyesha kabisa kwamba huu ni mkakati na hii ni Bajeti ya kusaidia watoto yatima huko Makete na mahali pengine Tanzania.

Nadhani ipo haja ya kuwa na Bajeti, isiwe sasa hivi kama ilivyo imekwenda tu kwenye Wizara inadandia dandia tu, ambayo unaweza ukakuta kwamba matokeo yake baadaye huwezi kujua ni kiasi gani hili limeweza kufanikiwa. Kwa hiyo, naomba Serikali iandae mkakati.

Ninazo taarifa kwamba huko nyuma Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilifika Makete ikaainisha programu na mikakati mbalimbali ambayo nadhani sasa ni muafaka ipitiwe ili katika Bajeti ijayo watenge fungu kabisa la kuhakikisha kwamba watoto yatima wanahudumiwa hasa wanawezeshwa katika fani za elimu ili waweze kujiajiri wao wenyewe. Huu utakuwa ni msaada mkubwa sana kwa watoto yatima walioko Makete na nadhani na mahali pengine kujua wako wapi, wanafanya nini na wana matatizo yapi.

Tujue idadi yao na ni programu zipi ziweze kufanyika ili ziweze kuwasaidia watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, napenda kuishukuru Serikali na hasa Ofisi ya Makamu wa Rais katika juhudi zake za kuhakikisha kuwa mazingira yanalindwa. Hili limewakumba ndugu zangu wa Kijiji cha Kikondo kilichopo Wilayani Makere ambao wao mwaka 1978 Kijiji chao kilisajiliwa na baadaye ikaonekana kwamba lile eneo kwa kweli lina uharibifu mkubwa wa mazingira. Naunga mkono kabisa kwamba wale wananchi wanatakiwa wahamishwe ili kunusuru vile vyanzo vya maji vilivyopo Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Serikali, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Nne hasa ukizingatia kwamba ni ya Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi ambacho kinawapenda watu wake, nilikuwa nadhani kuwe na upendo kuona ni namna gani, kwa sababu wale wananchi wako 2,800 na kwa sababu walisajiliwa, basi kuna Shule ya wanafunzi 425, basi huko watakakohamia Serikali ione umuhimu wa kuwasaidia angalau kuwajengea Shule ili waweze kuanza kufundisha watoto wao. *(Makofi)*

Lakini pili, Makete hasa eneo la Kitulo huko Kikondwe ndiyo sehemu pekee ya juu ambayo mwanadamu wa Tanzania anaishi tu katika milima. Kwa hiyo, pale ni baridi sana. Sasa hao wananchi ukiwaambia mwezi wa saba wawe tayari wamepata mahali pa kukaa watajenga saa ngapi? Miezi mitatu, watajenga nyumba za makuti! Kama ni matofali nyumba nzuri, inahitaji muda. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwafikirie kuwapa muda mzuri ili waweze kujenga na ukizingatia kwamba kuna watoto wachanga wanaozaliwa siku hadi siku kule ni baridi waweze kutimiza nia nzuri ya Serikali ya kulinda mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kuchangia kuhusu tatizo sugu la umeme. Mimi nadhani leo tunaweka hoja ya kwamba tupitie Mikataba yote. Nadhani ipo haja vile vile ya kupitia maamuzi yetu ya ndani ambayo yamekuwa yakifanywa huko nyuma. Mojawapo ni kama lile ambalo limefanywa na Serikali kupitia maamuzi ya kuuza nyumba za Serikali, ambayo nawapongeza sana kwa maamuzi hayo waliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la umeme, angalia, bwawa la Mtera liko huku Dodoma maji yanategemewa kutoka milima ya Makete yapite Usangu, kwenye jua kali, yapite kwenye bonde hili lenye *friction* , haya maji hayawezi kuwepo. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani tujaribu kuainisha mipango tuiangalie Tanzania yote na pembe zake zote kuona ni wapi ambapo huu mpango ungeweza kuwa stahimilivu zaidi.

Natoa mfano, Makete kuna vyanzo vingi vya maji ambayo yanakwenda kwenye bonde la Kyela na baadaye kufika kwenye Ziwa Nyasa. Hayo yangeweza kutumika kama tungefanya vizuri, kwa sababu stadi zimeonyesha kwamba Mtera inatoa MW 80, Kihansi MW60 na stadi ambazo zimefanyika nyuma zinaonyesha kwamba ule mto wa Maalya ambao unaingiza maji Ziwa Nyasa ungetoa MW 222 kubwa kuliko zile za sehemu zozote zile. *(Makofi)*

Sasa nilidhani kwamba suala la kukwepa maji, tunakwepa kwa sababu sisi ndiyo tumesababisha ukame wa nchi. Wenzetu wa Zambia wametumia maji kwa kuzalisha umeme kwa asilimia 99. Nchi zilizoendelea kama Urusi watu wanatumia asilimia *19 hydro power* na wakati huo huo wanatumia nyuklia asilimia 15. Marekani wanatumia nyuklia asilimia 20, lakini asilimia saba wanatumia maji. Tusiuache huu mkakati wa maji, pamoja na mikakati mingine, uende sambamba na kuona kwamba bado *source* ya maji ni muhimu sana na hasa ukizingatia kwamba maji ni rahisi kuliko s*ource* nyingine. *(Makofi)*

Lakini vile vile mngeuchukua huu mto ambao unamwaga maji Ziwa Nyasa kwa watu wa Makete, ungewawezesha kuweka mabwawa ya samaki. Lakini ukiteremka kule chini kwenye bonde la ndugu yangu jirani Mheshimiwa Profesa Mwandosya na Mheshimiwa Mwakyembe, wale wangeweza kufanya kilimo cha umwagiliaji. Wenzetu wa Malawi, ule mto wana-*regulate* kutoka kule. Kwa hiyo, maji yanajaa kwa sababu wale wanayatumia kwenye kumwagilia. Yakirudi yanachukua ardhi yetu ya *Matema Beach* na Ipinda inaliwa kwa sababu maji ni mengi. Sasa sisi tu-*regulate* kwenye kuingia tupeleke kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, unapojenga nyumba kama ni ya kuta nne, huwezi ukajivunia kujenga kuta mbili wakati kuta mbili nyingine bado. Lingine ambalo napenda kuchangia ni suala zima hili la viwanja ambavyo Serikali imesema kwamba wale ambao hawakujenga inabidi wavirudishe. Mimi nadhani hiyo siyo *permanent solution.* Wale watu uwezo wao ni mdogo. Kwa hiyo, wamejikuta wanatafuta hela kwa miaka mitatu miezi 36 na leo imeonekana kwamba hajavi-*develop,* wananyang'anywa.

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza Serikali iongee na Mashirika ya hifadhi za jamii kama *NSSF, PPF, LAPF* na mengine, ambayo yana wanachama. Wafanye kama wanavyofanya *SACCOS* kuwakopesha wafanyakazi, pesa za kujengea nyumba na hivyo itakuwa imetatua tatizo kama hili. Lakini vile vile, bado Serikali ihamasishe *Financial Institutions* kuwakopesha wananchi wengine ambao wanaweza wakakidhi zile sheria, wakopeshwe waweze kujenga nyumba na hivyo azma ya Serikali itakuwa imetimilika kwa sababu lengo lilikuwa ni kuhakikisha kila Mtanzania ambaye anaomba kiwanja anapata bila kubagua. Leo unapomnyang'anya atakwenda kupewa mwenye pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niongelee suala la maendeleo. Suala la msingi nimesema ni kuondokana na uchumi ambao ni tegemezi. Lakini vile vile tumesema kwamba ni kujenga uchumi ambao unawashirikisha Watanzania wote. Lakini ukiangalia hotuba ya Waziri wa Fedha inasema wazi kabisa kwamba baadhi ya malengo hayakutekelezwa kwa sababu wale wanaotupa pesa walikuwa wametingwa na vitu vingine. Maana yake nini? Ni kwamba hatuwezi kutegemea kujenga uchumi wetu kwa kutumia wafadhili kwa sababu siku wakitingwa, basi sisi tunabaki tuko nje.

Kwa hiyo, napendekeza kwamba kuwe na mkakati madhubuti kwa Serikali wa kuwawezesha wawekezaji wa ndani wa Tanzania ikiwezekana hata wapewe ruzuku. Ili kujenga uwezo wao wa miradi mbalimbali, Mfano naweza kutoa kwa jengo hili ambalo

tumo humu ndani. Jengo hili limejengwa na ndugu zetu wa China wametoa bilioni 29. Lakini ukipiga mahesabu vizuri, asilimia kama ilivyosemwa vizuri, asilimia 70 zimerudi China kwa njia ya mishahara na kwa njia ya *materials* mbalimbali. Kwa hiyo, sisi tumebaki na jengo.

Lakini hakuna watu wengine ambao wamefaidi zaidi ya hili jengo. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali ili kweli tufike tunakotaka. Lazima..

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Taarifa, Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakubali kupokea hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae chini tupokee kwanza taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Maelezo ambayo anayatoa Mheshimiwa Mbunge sasa hivi, inaonyesha kwamba hili jengo limejengwa kwa msaada kutoka China. Hili limejengwa na pesa za Serikali za nchi hii. Yule ni Mkandarasi tu ndiyo aliyejenga. Kwa hiyo, ni vizuri akalifahamu hilo. Alivyosema kwamba pesa nyingine zimerudi huko hazikurudi. Hii ni pesa ya Serikali ya Tanzania, imetoa kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mbunge naomba utakapoendelea kuchangia, upokee taarifa ya Serikali inayosema kwamba ujenzi wa jengo hili umetokana na fedha za Serikali na siyo msaada kutoka China. Naomba uendelee. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hiyo taarifa na naifuta hoja yangu.

Nilichotaka kusema, mfano huo kwenye Mashirika mengine ambayo tunatoa tenda kwa Mashirika ya nje, basi ielekeze dhana nzima kuwawezesha Watanzania ili wapate zile kazi pale wanapoweza na hasa kwenye miradi ambayo fedha zake zilikuwa ni zetu Watanzania kama ilivyokuwa kwa jengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ya kutoa majadiliano haya. Nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake hii nzuri ambayo karibu inakidhi maeneo mengi na mimi nasema naunga hoja mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia muda, kabla sijasitisha Kikao hiki, ningeomba tu Waheshimiwa Wabunge tufahamu kwamba michango yote tunayoitoa ndani ya Bunge ni michango muhimu na Watanzania wote wanafuatilia nini tunachokiendesha. Kwa hiyo, naomba kusema, mtu yeyote

anapochangia kama ana hoja ya msingi na yenye uthibitisho, ni vyema akawa na uthibitisho katika mkono wake ili Mheshimiwa Spika anapoomba uthibitisho, basi inakuwa ni rahisi kupeleka uthibitisho huo Mezani kwa Spika. Vinginevyo tunaweza tukawa tunapata taabu sana kuthibitisha ama kutokuthibitisha na huenda ikawa kinachosemwa na Mheshimiwa Mbunge labda kiko sahihi au hakiko sahihi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu kutoa taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwataje kabisa Wasemaji wa mwanzo, kwa kuwa ilikuwa Mheshimiwa Severina aseme baada ya Mheshimiwa Dr. Mahenge na hajapata muda, basi atakuwa msemaji wetu wa kwanza na atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga.

Baada ya hayo, naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa 11.00 jioni. Ahsante. *(Makofi)*

*(Saa 06.52 Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate kuchangia hoja hii.

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu kwa kunichagua kati ya wale wachache walioweza kuingia katika Bunge la Jamhuri Muungano wa Tanzania. Napenda kutoa shukrani kwa Chama changu cha CHADEMA, kwa kuwa na imani na mimi, kunichagua kuweza kuwakilisha Mkoa wangu wa Kigoma. Naahidi nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na nitatetea maslahi ya Watanzania bila uwoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kutoa hongera nyingi kwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na ninawapongeza wote waliopata nyadhifa mbalimbali siku hiyo ya tarehe 25 katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hii, nilikuwa napenda pia kutoa shukrani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri waliyofanya. Tumeshirikiana pamoja kwa kipindi cha wiki mbili kutatua tatizo la uraia la Mtanzania mmoja anayeishi Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma kumekuwa na tatizo kubwa la masuala ya uraia. Sijui kama ni Mikoa yote ambayo ipo mipakani wanapata tatizo hili au ni Kigoma tu. Wananchi wamekuwa wakifukuzwa nchini kwa kuambiwa sio raia halali. Hilo ni tatizo ambalo limeanza siku nyingi. Sasa huyo ambaye tumemsaidia katika hizi wiki mbili ameteseka kwa muda wa mwaka mmoja na nusu akiambiwa kwamba sio Mtanzania. Alifukuzwa akapelekwa Ubalozi mdogo wa Burundi, Ubalozi mdogo wa

Burundi wakamkataa na akarudishwa tena Tanzania. Kwa hiyo, sasa hivi ni *stateless,* ila Wizara ya Mambo ya Ndani inaendelea na kazi hiyo. Kwa hiyo, naamini kabisa tatizo lake litatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye hoja, lakini mimi nitarudi nyuma kwenye historia ya nchi yetu katika mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali kwa ajili ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa Mtanzania. Napenda kuzipa pongezi awamu zote nne kwa sababu zilifanya kazi nzuri kwa kuhakikisha kwamba umaskini kwa Mtanzania unaondoka. Tangu mwaka 1961 tulipopata uhuru, kumekuwa na mikakati mbalimbali. Tulianza na Azimio la Arusha, mali ya wananchi ilikuwa mikononi mwa wananchi wenyewe na Serikali ndio ilikuwa mdhamini mkuu au msimamizi mkuu wa mali hizo. *(Makofi)*

Katika miaka ya 1980 tunaona pia kulikuwa kuna sera nzuri za Sekta za Maji, huduma za afya, elimu na huduma za kijamii kwa ujumla. Lakini kwa bahati mbaya hatukuweza kufanikiwa vizuri kwa sababu uchumi wa nchi ulikuwa umetetereka kutokana na vita dhidi ya Iddi Amini, kutokana na Shilingi kushuka thamani kutokana na mafuta ya petroli kupanda bei duniani na *East African Cooperation* ilivuponjika. Kwa hiyo, kidogo uchumi wetu ulitetereka. Lakini Serikali haikuacha kufanya kazi nzuri kwa kuhakikisha kwamba inaleta njia nyingine mbadala mwaka 1980, tukaanzisha *National Economic Survival Program* (1981) na *Economic Recovery Program (1986)* kuhakikisha kwamba uchumi unafufuka. Pia kulikuwa na mikakati mingine kama S*tructure Adjustment Program* na hizi zote zinaonekana ni kazi ambazo Serikali ilikuwa ikifanya kuhakikisha kwamba tunajikomboa, tunamkomboa Mtanzania kutoka katika umasikini, maradhi na ujinga. *(Makofi)*

Katika miaka ya 1990 tumeona Sekta Binafsi zikiwa kama injini kuu ya kuhakikisha kwamba uchumi unakua kwa mtu mmoja mmoja. Lakini kwa sasa hivi tunayo *vision 2025*. Katika hiyo *vision 2025* au Dira ya Maendeleo ya Taifa, tunaona kwamba kuna MKUKUTA, MKURABITA, na MKUMBITA. Lakini hizi zote zinaonekana lengo lake ni lile lile moja kuondoa umasikini kwa Mtanzania. Sasa tujiulize: Je, tunahitaji kuendelea kutafuta misamiati mingine? Kwa nini hatufanikiwi na juhudi hizi zote za Serikali? Juhudi ni kubwa lakini mafanikio ni kidogo! Tujiulize, tatizo liko wapi?

Kwa hiyo, ni maswali ya kujiuliza pamoja na kwamba tuna matatizo mengine mengi kwamba labda Bajeti yetu inakuwa ni kidogo katika kutekeleza mipango ya Serikali, labda wataalam wetu hawana *capacity* ya kutosha au hatuna wataalam wa kutosha. Lakini mimi pia naona tuna tatizo lingine na wana-*sociology*. Tunasema unapotaka kutatua tatizo lolote, hakikisha unaangalia chanzo cha lile tatizo, usiende moja kwa moja kwenye tatizo lenyewe kwa sababu linaweza likajirudia tena.

Mimi naona Tanzania tuna tatizo moja la kukosa maadili. Maadili yako aina mbili. Kuna *professional ethics* na kuna maadili ya mtu binafsi. Sasa vitu vyote viwili vinakwenda pamoja. Wachangiaji wengi wamekuwa wakilalamika kwamba Halmashauri zetu zinapata hati chafu, wengine wanasema kwamba rushwa bado imekithiri katika

Sekta ya Umma, lakini tujiulize, kwa nini vitu vyote hivi vinatokea? Kweli tunakuwa labda ni kile kidogo ambacho kimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi fulani, lakini mipango mingi unakuta haitekelezeki, haifanikiwi. Tujiulize, ni kwa nini? Kama tungekuwa tunatumia kile kidogo ambacho tunacho katika kuhakikisha kwamba kweli tunamkomboa Mtanzania katika huu umaskini, naamini tungepinga hatua zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea suala la maadili, naamini kabisa maadili binafsi au nidhamu binafsi na maadili ya kazi yanakwenda pamoja. Warsha nyingi zinatolewa kuhusu huu utawala bora. Kuna Semina nyingi kuhusu utawala bora, lakini mimi naona kama bado hatujafanikiwa. Serikali sasa hivi inatakiwa kupigania maadili binafsi, kupigania nidhamu kwa mtu mmoja mmoja ili kutekeleza majukumu yetu. Kwa mfano, unakuta katika Wizara zetu zote, sasa hivi katika Bajeti nimeona kuna kifungu ambacho kimetengwa kwa ajili ya utawala bora na suala la UKIMWI. Tutaendelea kutoa hizi pesa mpaka lini? Pesa hizi zingeweza kufanya kazi nyingine, mimi naona tayari watu wangeshapata ujuzi wa kutosha kuelewa maana ya utawala bora ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mtu akiwajibika katika sehemu yake akashirikisha watu kama inavyotakiwa katika kazi yake, naamini tutapata matunda mazuri tu pamoja ni kwamba tunacho kidogo ambacho tunakitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutokuwa na nidhamu binafsi, linasabisha tusiweze kutekeleza maadili ya kazi ambayo tunayo. Unakuta katika Ofisi wameandika kibao, hatutoi wala kupokea rushwa, lakini vyote hivyo vinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutokuwa na hayo maadili binafsi yanasababisha watu wasiweze kufanya kazi zao vizuri kwa sababu kwanza anafanya tu wala hajali. Muda wa kazi umeandikwa lazima wafanye kazi labda masaa manane anapokuwa Ofisini, lakini muda mwingi anautumia kupiga makelele au kufanya shughuli nyingine yoyote ambayo anahisi yeye inamsaidia na hiyo inatusababishia watu kuwa hawana uzalendo na kuwa wabinafsi. Mtu yupo tayari kufanya chochote kuhakikisha kwamba anajipatia kipato ambacho ni cha zaidi hata kwa kumwumiza Mtanzania mwenzake.

Kwa hiyo, nafikiri Serikali sasa hivi inatakiwa ipiganie nidhamu binafsi, maadili binafsi ili watu waweze kutekeleza maadili yao ya kazi, hivi vitu vinakwenda pamoja. Ndivyo ninavyoona mimi tatizo lililopo. Pamoja na kwamba tunacho kweli hicho kidogo, tukiwa na maadili binafsi tutaweza kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri na kuhakikisha kwamba uchumi unakuwa endelevu na usemi wa Waziri Mkuu unaosema kwamba tucheze ngoma kwa mdundo mmoja, naona utawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea na suala hilo, naona kwamba kukosekana maadili binafsi kunasabisha kutokuwa na uzalendo. Tumesikia watu wengi wakilalamika hapa wakisema kwamba *TRA* kuna watu wana majibu mabaya, Wananchi na Wabunge wamejibiwa vibaya, huku ni kukosa uzalendo. Mtu anaona kabisa kwamba ile ni kazi ya kumhudumia Mtanzania, lakini anafanya anavyotaka yeye.

Kwa hiyo, mimi nitaendelea kusisitiza maadili binafsi na maadili katika kazi zetu tunazozifanya ili kuhakikisha kwamba tunafanikisha ile mipango yetu tuliyojiwekea, haina haja tena kuendelea kuweka misamiati mipya au mikakati mipya. Tuwafundishe Watanzania waweze kuelewa kitu gani kinachoendelea kwa sasa hivi kuhusu MKUKUTA, MKURABITA na kadhalika. Lakini tuhakikishe kwamba hawa Watendaji wote kila mmoja katika nafasi yake anafanya kazi ambayo amekusudiwa kuifanya ili malengo yaliyowekwa yaweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, napenda niwashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Kwimba ambao kwa imani kubwa waliyokuwa nayo walinipatia kura nyingi sana asilimia karibu ya 80, kuja kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kuwapongeza kwa sababu wao ndio walionileta hapa kwanza, hivyo ni lazima niwapongeze wao. Lakini kikubwa walichonituma kwa niaba , nimpongeze Mheshimiwa Rais kwanza kupata kura nyingi sana katika Uchaguzi Mkuu kuwa Rais wa nchi hii. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Chaguzi hizi mbili zimeonesha kwamba makabila yote yanafanana na yanalingana. Tanzania hapa hakuna kabila dogo wala hakuna kabila kubwa. Sasa hivi hapa ninavyoongea mimi, naamini kwamba Wakwere sasa hivi wanajivunia sana na sio ajabu Wazaramo na Wazigua wanaozunguka kabila la Wakwere wanajiita Wakwere wanapokuwa nje ya maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile niitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Wakuu. Nina shukrani zake za dhati baadaye, lakini nampongeza kwanza kwa kupata kura nyingi sana za Wabunge hapa kumthibitisha uchaguzi wake. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuteuliwa katika Bunge letu Tukufu kuwa Spika. Lakini vilevile nampongeza Naibu Spika, ambaye ndio wewe mwenyewe hapo, mwanamke wa kwanza kuwa Naibu Spika. Hongera sana.

Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri. Kwanza niwapongeze, lakini niwape pole sana kwa sababu nafahamu wana kazi kubwa sana hasa katika Awamu hii ya Nne. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana na kuwapa pole nyingi na kazi kubwa imeanza kuonekana. Pongezi za mwisho, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge. Nafahamu mlikopitia hadi kufika mpaka hapa. Mmepita katika kazi kubwa sana, nawapongeza sana. Pongezi zangu za mwisho ni kwa Serikali kwa ujumla jinsi

inavyoshughulikia mambo mbalimbali tangu ilipoanza shughuli zake za Awamu ya Nne. Tumeona wote ilivyoshughulikia suala la njaa, jinsi ilivyoshughulikia masuala ya mafuriko, ajali mbalimbali inaonesha kwamba Serikali kweli iko makini na mimi naamini kwamba inawezekana, ndio sababu hata Bajeti ya Serikali ilipokuja mbele ya Bunge lako Tukufu ilipita bila upinzani kwa sababu Serikali inaonekana ipo makini. Tuna imani nayo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tahadhari moja, kwamba wananchi wana mategemeo makubwa sana kwa Serikali yetu. Lakini naomba niseme wazi kwamba naomba Wabunge tukubaliane tuwaambie wananchi ukweli kwamba maisha sio rahisi, maisha ni magumu. Mwenyezi Mungu anaelekea kuwapenda sana ndege. Ndege hawana mashamba, ndege hawafanyi biashara, ndege wanapata chakula, lakini Mwenyezi Mungu hajawahi kuwapelekea vyakula kwenye viota. Ndege lazima afuate vyakula, pamoja na kuwepo kwa vyakula. Kwa hiyo, lazima tuwaambie kuwa lazima tufanye kazi kwa nguvu zote ili kuisaidia Serikali iweze kutufikisha kwenye malengo yake. Lazima tufanye kazi kwa nguvu sana. Baada ya kusema hayo, sasa naomba niendelee na michango yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaweza kuongea maneno mengi sana, lakini nitajitahidi kwenda haraka haraka. Ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu unaongelea juu ya kujitosheleza kwa chakula. Naipongeza sana Serikali kwa kutoa maelezo haya mazuri sana. Lakini ombi langu ni kuomba Serikali ijaribu kutupatia maelezo waziwazi kwamba familia, kwa mfano familia ya watu kadhaa inatakiwa angalau wawe na chakula kiasi gani kwa mwaka kwa sababu kuna sehemu nyingine watu wanapata vyakula vya kutosha, wanauza vyakula vyote wanakuwa na njaa. Tuwe na vigezo, tuwe angalau na maelekezo fulani, kwamba angalau kila familia ijiwekee chakula cha kutosha kwa mwaka mzima. Kama familia ya watu watano au kama ni familia ya watu kumi, hata angalau tu kwa wastani, kuwapatia wananchi angalau mwanga, kwa sababu watu wengine hata makadirio ya vyakula wanachohitaji kwa mwaka mzima hawajui. Nilikuwa nafikiri kwamba Serikali sio vibaya angalu tu ikatoa maelezo fulani ili watu wakae wakijua Serikali inategemea nini kutoka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi wetu. Ukifuatilia, tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza, ya Pili, ya Tatu na hii ya Nne, Serikali daima ina malengo mazuri sana kwa wananchi wake. Kila wakati imekuwa ikitoa maelekezo lakini hatusogei sana. Kulikuwa na maelekezo kama chakula ni uhai, kilimo cha kufa na kupona, mazuri tu. Lakini je, ujumbe unawafikia wananchi wetu? Hivi sasa tunaongelea juu ya kuondoa maradhi, umaskini na ujinga. Je, wananchi wetu wanapata ule ujumbe tunaouelewa sisi?

Unaposema juu ya umaskini, umaskini tunaouongelea hapa ndio umasikini wanaouelewa wananchi wetu, kwa sababu inaweza kuwa tunaongea lugha tofauti, mtu anaweza kulima shamba lake la pamba, akalima shamba lake la zao lolote, lakini amelenga kununua ng’ombe. Akishapata ng’ombe kwake ameshakuwa tajiri. Nadhani hatuongelei juu ya utajiri huo. Mtu anaweza kuamua kufanya kazi fulani ajenge nyumba, akishapata nyumba kwake yeye huo ndio utajiri. Ndio lugha yetu hiyo. Naomba sana

tujaribu kuangalia utaratibu wa kuwasiliana vizuri na wananchi wetu waweze kuelewa lengo letu ni nini hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa shukrani na pongezi, napenda nitumie nafasi hii kwa niaba ya watu wa Jimbo la Kwimba kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wakati akiwa Waziri wa Maji alitushughulikia mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Shinyanga. Alikubali maji hayo yafikie katika Wilaya ya Kwimba katika tarafa ya Mwamashimba. Inawezakana watu wengi hawafahamu hata Kwimba ni wapi, kwa hiyo wanafikiri ni Wilaya. Ni kweli, iko Mkoa wa Mwanza, lakini ni Wilaya ambayo haipakani na Ziwa hata kidogo, ni kame. Tulishapata mradi mwaka 1974/1975 kulikuwa na mradi wa maji wa kupeleka tarafa ya Mwamashimba, haukufanikiwa, ikaja *HESAWA* ikajaribu kuchimba angalau kila Kijiji kisima, kimoja lakini hivi sasa tunavyoongea kuna visima vinne tu katika Vijiji vyote vilivyochimbwa na *HESAWA*. Mradi huu ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu alikubali uje mpaka Tarafa hii ya Mwamashimba, ni muhimu sana kwa watu wa Tarafa ya Mwamashimba na watu wa Kwimba kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani, kama taratibu zingeweza kuruhusu, mradi huo uweze kufika hata kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba, nafahamu Ngudu kuna utaratibu wake wa kupelekewa maji, lakini ingefaa ule mradi ambao unakwenda mpaka Mwamashimba usogezwe mpaka Ngudu ambao ni Mji unaokua haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika suala moja ambalo nilitaka kuongea, nalo ni wazee na walemavu. Suala la wazee na walemavu, labda nisiongelee sana. Kwanza niongelee juu ya walemavu. Ndugu zangu mimi sikuwa hivi. Wale waliokuwa wananifahamu, nilikuwa natembea haraka haraka kuliko hata wengi mnavyotembea. Hali ya maisha inabadilika. Unaweza kupata ulemavu wakati wowote! Napenda niseme wazi hapa, siombei mtu yeyote hapa apate udhaifu kama wangu, mimi natosha kuwapatia mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata uzoefu kwa niaba yenu, ninatosha. Lakini, naomba Serikali iangalie juu ya *physiotherapists* ndio ambao watatusaidia sana kupunguza walemavu katika nchi hii. *Physiotherapists* wanakuja baada ya Daktari. Mimi nilipolazwa nilipewa dawa mpaka *BP* ika-*stabilize,* sikuwa tena na la kufanya na Daktari. Lakini nilikuwa bado kitandani, sana sana ningeweza kuwa ni mtu *wheel chair. Physiotherapist* ndio ambao wamenifanya leo niweze kusimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Afya, angalia maslahi yao, angalia uwezekano wa kuwafikisha *physiotherapists* kama sio katika ngazi ya Vijiji angalau hadi katika ngazi ya Wilaya. Mimi natoka Mwanza. Kama ningehitaji *physiotherapist,* ningetoka Mwanza kwenda Bugando au Muhimbili Moi, la sivyo nakwenda India. Gharama ni kubwa sana, kwanza kwa mlemavu mwenyewe, kwa mgonjwa mwenyewe, au kwa familia yake. Lakini naamini kwamba kama tukiwapatia uwezo sana *physiotherapists,* naamini kabisa kwamba tutapunguza walemavu, tutaongeza watu wa kuweza kusaidia kuongeza pato la Serikali hata katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mimi huwezi kuniita kama ni mlemavu. Mimi sio mlemavu, mimi hivi sasa ni kama mtu ambaye alikuwa anaumwa Malaria, huwezi kuumwa Malaria leo ukapona mara moja. Mimi napona pole pole. Nina uwezo wa kuzalisha mali, lakini kama ningeweza kuachwa Bugando nimelala tu, baada ya *BP* ku-*stabilize,* ningekuwa tegemezi. Lakini *physiotherapists* ndio walionisaidia.

Naomba kama haiwezekani kuwaongezea kipato chao, angalau basi waruhusiwe wafungue Kliniki binafsi. Hawa hawatoi dawa, hawa wanafanya kazi bila kugawa dawa. Masharti ya kufanya kwao, ni lazima tu wafungue Kliniki zao wakiwa au Daktari na Mganga, sidhani kama ni lazima sana. Hao wanapewa wagonjwa na Daktari baada ya Daktari kumaliza kazi yake. Hawa ndio wanakabidhiwa mgonjwa. Sasa unataka mganga afanye na *physiotherapist* wa nini? Naomba waruhusiwe wafungue Kliniki zao kama hawawezi kupewa mafao yao mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu nimepigiwa kengele, lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu hujafika Kwimba, tarafa ya Mwamashimba, kabla ya mradi wako kufika. Kupata thamani ya mradi huu ilikuwa inafaa ufike kwanza uone watu wanavyohangaika, ujiridhishe wewe mwenyewe kwamba kazi uliyofanya sio ndogo, ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

La mwisho, kabla ya kengele, lakini kama italia mapema, nimeunga mkono hoja. Mwisho ni suala la mazingira. Ninamheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mwandosya. Kwimba tulikuwa na mradi wa *KRP*, tulipanda miti, mikaratusi mingi sana na watu waliitikia sana wito wa kupanda miti na hata sasa hivi wako tayari kupanda miti. Lakini mikaratusi tunaambiwa inanyonya maji. Kwimba ni kavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Sikuweka vitu vyangu sawa sawa, lakini ngoja niziweke, zitakubali tu. Kwanza kabisa, nawapongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutoa hotuba yake ya Bajeti nzuri sana na inatoa mwelekeo mzuri. Vilevile nawapongeza na Mawaziri ambao wako chini yake. Kuna Mheshimiwa Juma Akukweti ambaye ni Waziri wa Nchi, ambaye anashughulikia Bunge na utaratibu, nimesema sana kwa sababu amefanya utaratibu mzuri sana katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Vilevile, nawapongeza na wengine, Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Peter Pinda na Manaibu wake Mheshimiwa Siyame na Mheshimiwa Celina Kombani. Wote nawapongeza sana kwa kazi nzuri. Mimi naiona pamoja na wataalam, pamoja na Makatibu Wakuu, wamefanya kazi nzuri sana. Mimi naona kabisa kwamba Bajeti hii ya Wizara hii chini ya Waziri Mkuu ndio kiini cha maendeleo katika nchi hii na ndipo kama Wizara hii chini ya Waziri Mkuu ikifanya kazi kama inavyopasa ndio inajibu kabisa suala la Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya na Wizara zote za nchi hii zinakutana katika shughuli hii. *(Makofi)*

Hii ni mantiki kubwa sana kwamba, kama Wizara hii ikifeli kufanya kazi kama ipasavyo, Wizara nyingine hazina nafasi ya kutekeleza Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Huo ndio ukweli wenyewe! Kwani ndio wanabeba Tawala za Mikoa zote, Serikali za Mitaa zote katika nchi hii, Halmashauri zote. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kama kuna watu ambao ni goigoi katika Wizara hii, kama hawawezi kwenda katika Kasi Mpya, basi waondolewe. Usije ukaweka gari mbovu *engine* mpya, halafu ukaendesha halafu chesesi imekatika, huwezi kufika Morogoro. Kwa hiyo, hii naomba kabisa tujaribu kuangalia, tunawapa kazi ili waweze kuchekecha tuweze kufikia hizi azma. *(Makofi)*

Pili, nataka nitoe shukrani sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Katika Mkutano wa tatu, nilizungumza katika Bunge hili mambo mawili makubwa na yamefanyiwa kazi. La kwanza nililalamika sana juu ya elimu katika Wilaya ya Kiteto kwamba imeshuka, wala hakuna! Naomba Serikali ishughulikie kikamilifu. Wilaya iko nyuma kielimu, kuna tatizo gani Kiteto? Tukifananisha na Wilaya za Wafugaji Ngorongoro, Monduli, Simanjiro, kwanini Kiteto iko nyuma kielimu kuliko Wilaya nyingine zote? Kwa kweli Wizara imefanya kazi. Namshukuru sana Mkuu wangu wa Mkoa, pamoja na Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kutuma Tume kwenda kuchunguza kuna nini Kiteto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarajika kabisa kwamba unapozungumza hapa, Serikali inakukubali, imefanya kazi nzuri sana na hakika sasa kwamba watu wa Kiteto wanasubiri kwa hamu sana Wizara ya Elimu na Mafunzo itoe majibu ili Kiteto nayo ifananefanane na Wilaya nyingine zote katika nchi hii. Hilo la kwanza.

La pili, nililalamika. Sio kulalamika, nimeongea juu ya uharibifu wa Mazingira katika Wilaya ya Kiteto mpaka Tume ikaja kutoka Kiteto, wananchi wameandamana wakapokelewa na Mawaziri, Waziri wa Mazingira na Waziri wa TAMISEMI hapa Bungeni hiyo Tume ya Kiteto, nao wakaunda Tume, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa pamoja na Taifa wameunda Tume, imekwenda Kiteto kushughulikia masuala ya matatizo yaliyoko Kiteto juu ya uharibifu wa mazingira. Nawashukuru sana. Mkuu wa Mkoa ameunda timu kwa maelekezo mazuri tu, hiyo timu ikiongozwa na *RC*, timu ambayo ni nzuri, imefanya kazi nzuri katika Wilaya Kiteto, ninaamini kabisa ripoti yake imeshafika mpaka Ofisi ya Waziri Mkuu na imeshafika kwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kiteto wanasubiri kwa hamu sana matunda ya hiyo Tume, kwa ajili ya maendeleo ya Kiteto. Wamejua, wamekuja kuhakikisha na wameongea na Tume, kwa hiyo, wanasubiri. Ninapoongea hivi, wananituma kila siku, majibu ya Tume yatakuja lini? Kwa sababu kuna watu ambao ni waharibifu, ni viongozi, wanataka kuelewa Serikali hii kwa kweli inatimiza wajibu wake ama haitimizi!

Kwa hiyo, tunaomba Tume baada ya kufanya hii kazi, nina hakika na Mkuu wangu wa Mkoa pamoja na Mawaziri wote. Ninaomba isiachiwe hii kazi Wilaya. Wilaya haiwezi. Tuko ndani ya migogoro ya hiyo Tume, Wilayani wananchi

wamelalamika, Wilayani sisi wote ni wabovu, kwa hiyo, tunangojea maamuzi ya Tume ifanye kazi. Huwezi kumwambia mtu wa Wilaya amuweke ndani mtu ambaye yeye amemuuzia ardhi. Sasa yeye atamshitaki! Haiwezekani. Ndio maana Tume imekwenda kule. Kwa hiyo, tunaomba sana kazi ya hii Tume ije.

La mwisho ambalo ni la jumla ni suala la wafugaji. Suala hili limezungumzwa sana. Kwanza tuelewe kabisa kwamba, tatizo la wafugaji sio ng'ombe. Ng'ombe anachungwa na binadamu, mtu anasingizia ng'ombe ndio mharibifu wa mazingira. Sio ng'ombe, mwenye ng'ombe ndio mharibifu wa mazingira. Wewe ng'ombe unapeleka kwenye kunywa maji, kama kuna kisima pale wewe ndiye binadamu anayempeleka ng'ombe akaharibu hicho kisima.

Hakuna, usiwalaumu ng'ombe hata siku moja, ng'ombe ni chakula, ng'ombe ni mali kama mahindi au kahawa, tatizo ni binadamu kuwatafutia mahali pazuri, ng'ombe hawawezi kuruka tu wakaenda kuharibu mazingira, hata haiwezekani. (*Makofi*)

Mipango ya binadamu ndiyo inayotufanya sisi tuseme kwamba, ng'ombe ndiyo wanaharibu mazingira. Kwa hiyo, naombeni sana, wafugaji ndiyo watu ambao sasa hivi kwa kweli wamekuwa wakimbizi katika nchi hii. Wote tunaelewa wafugaji, kwa nini hamzungumzii ng'ombe? Mimi ni mfugaji na kila mtu ni mfugaji. Sasa hivi mfugaji ameiokoa nchi hii kwa gharama kubwa sana. Mnafahamu kilo moja ya nyama ya ng'ombe ni sawasawa na lita moja ya *petrol*? Leo nchi hii kama nyama hakuna, mnaweza kuagiza nyama kutoka nje? Mnajua ni ghali zaidi kuliko mafuta mnayotumia katika magari? Mnaiona thamani ya maziwa na kuku, hamuwezi kuangalia mambo haya?

Kwa hiyo, nawaomba twendeni sasa tukawapangie matumizi bora ya ardhi, tupate maeneo ya wafugaji na tupate na maeneo ya wakulima. Hiki kitu tusikionee haya, yametamkwa na Rais wetu siku nyingi, hata Wizara kuundwa ili tuweze kufuga mifugo vizuri, lakini inaelekea Serikali inalionea haya suala hili na katika jumba hili, inaelekea kuwa mkulima ni lazima nawe uwe mfugaji. Mimi ni mkulima na ni mfugaji sijaumia kitu chochote. Kwa hiyo, nawaomba sana.

La mwisho, Halmashauri zetu za Wilaya kuna kitu kinachoitwa *Local Government Support Program*, eti Wilaya haipati fedha mpaka imepata Hati Safi. Jamani unaniletea Mkurugenzi mbovu, anayekula pesa, kwa nini uwaadhibu watu wangu? Badala ya kumwadhibu huyu Mkurugenzi, ambaye anakula pesa, mahesabu yake machafu, sasa unasema Wilaya ya Kiteto au Wilaya nyingine, zisipate pesa, tujisahihishe kwa hapo. Halafu inawezekana hizi fedha ni mkopo, nitakuja kuzilipa kwa wananchi ambao hawajapata huo mkopo kwa ajili ya uzembe wa mtu. Hebu kila mtu achukue mzigo wake kabisa, kama Wataalamu hawawezi kupata Hati Safi ni shauri lao, hilo la mwisho. Naomba tugawane kabisa fedha, kuna wilaya sasa hivi wanapata shilingi milioni 500, nyingine shilingi milioni 700 na nyingine shilingi milioni 800 kwa sababu ya kupata Hati Safi. Mimi ni Mjumbe wa *LAAC*, tumekwenda kuangalia *value for money,* wale waliopata Hati Safi hamna kitu, wamehonga wakapata Hati Safi, unakuta jengo liko hivi basi ngoja nifanye hivi Juma asije akasimama pale.

Sasa la mwisho ambalo nataka nizungumzie ni kwamba, sisi Wilaya ya Kiteto, kuna Kata ambazo zina kilometa 80 mpaka 70, huo Ukuu wa Wilaya utafanywa namna gani? Tunaomba Kata na tulileta *application* siku nyingi, tangu mwaka 2000 Rais akatamka hilo, basi Kata sita. Sisi tumeshawahi, haya mambo sisi tulikuwa tumechelewa, sasa tunataka kufanya hivi unasikia mlango umefungwa, jamani mtufungulie mlango na sisi tuone. Nina vijiji 54 katika Wilaya nzima na vitongoji 600, sasa unapeleka wapi, nchi yenye vitongoji tupu? Vitongoji umati wa watu uko ndani ya vitongoji, jamani ziwe vijiji, hapana, hakuna makisio. Basi tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba kabisa ndugu yangu, hili ni suala ambalo ni la kimaendeleo kabisa. Jirani yangu Mheshimiwa Job Ndugai, amezungumza, kwa kweli hili jambo la vijiji wala tusingojee uchaguzi, hapana! Sasa tutajengaje sisi Sekondari? Tuna kata 10, wenzetu wanajenga Sekondari kwa Kata. Tukiomba sisi Kata tunaambiwa hapana, yaani Sekondari zetu ziwe 10 tu? Hali yetu yote ni vitongoji? Nina shule kama 90 sasa hivi, lakini tumeanza kufungua kwa vitongoji. Kwa hiyo, naombeni sana jamani, suala hili la vijiji lipo katika ofisi ya TAMISEMI, tuangalieni sana.

La mwisho, kuna watu ambao walitupinga katika suala la Uchaguzi Mkuu, sasa kama mnawapenda basi wahamisheni, wamekuwa kero katika maeneo yetu na sisi tumeshika mpini. Wakati ule walikuwa nao wameshika mpini, sasa tumerudia tumeshika mpini, sasa waondoke, kama unawapenda basi wapeleke katika ofisi yako, nenda kawabebe. Wananchi tumeshindwa hata kwenda kutoa shukrani, kwa sababu bado wanatukodolea macho pale, waache waondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba mfanye haraka. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Siku nyingine utakapokuwa unaomba mambo yako, upitie kwa Spika, ndiyo utaratibu.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mohamed Missanga ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Meryce Emmanuel.

**MHE. SUSAN A J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja safi sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Awali ya yote, naomba nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwani amekuwa ni Rais wa kwanza toka vyama vya upinzani vimeanza, kuweza kukaa na Kambi ya Upinzani na kuongea nao. Hivyo basi, nadhani Rais kama Kiongozi Mkuu na Viongozi wenzake pia watamfuata na kuona umuhimu wa Wapinzani hapa Bungeni. Pili, naomba nichukue nafasi hii kukishukuru chama changu cha CHADEMA, kwa kuniteua na ninawaahidi kwamba, nitafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu na ari ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe pongezi kwako wewe binafsi, kama Mama ambaye kwa kweli umetupenda na hukujali itikadi zetu, umeweza kutuonyesha njia, tunakushukuru sana. (*Makofi*)

Baada ya pongezi hizo, naomba sasa nianze kuchangia katika hoja hii. Katika mchango wangu wa bajeti niliunga mkono hoja ile mia kwa mia kwa sababu kuu mbili: Kwanza, kwa sababu bajeti ile ilikuwa ina mwelekeo wa kumwinua maskini, ambaye ni raia wa nchi hii lakini pia kwa sababu ni mpinzani na upinzani haumaanishi kupinga kila jambo hata kama lina tija kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie na nitaanzia Wizara ya Afya, kwa sababu mimi pia ni mwanakamati katika Kamati ya Huduma za Jamii, ambapo Wizara ya Afya ni mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, katika bajeti ya mwaka huu, Wizara ya Afya imepata nakisi ya asilimia 42. Kwa maana ya kwamba, mwaka 2005, Wizara ya Afya ilipata zaidi ya shilingi bilioni 278, lakini kwa mwaka huu tunaona imepata shilingi bilioni 195 tu. Sasa tunajiuliza, hivi magonjwa hapa nchini Tanzania yamepungua au yanazidi? Lakini pia tukiangalia katika vyombo vya habari na tunavyojua ni kwamba, sasa hivi akina Mama 24 hufariki kila siku kutokana na matatizo ya uzazi, hii inamaanisha kwamba, kwa mwaka mzima, wanawake zaidi ya 8,600, yaani karibu wanawake 9,000 tunawapoteza hapa Tanzania, lakini hapohapo bajeti imepungua kwa asilimia 42. Sasa naomba kuuliza, kwa sababu Waziri Mkuu ameongelea masuala ya afya, tujue ni kwa nini Wizara hii bajeti yake imepungua kwa kiasi kikubwa namna hiyo, wakati magonjwa yanazidi kuendelea na wananchi wanazidi kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, naomba tuelekee kwenye ukurasa wa 14 kuhusu bei za mafuta. Ieleweke kwamba, mafuta kwa kweli katika nchi yoyote, ndiyo chanzo cha maendeleo ya uchumi, kwa sababu ni mafuta hayohayo ndiyo yanayotumika katika viwanda, magari na sehemu nyinginezo. Kwa hiyo, hapa Tanzania tunaona bei ya mafuta inapanda kila siku, tunajiuliza ni kwa nini, pamoja na kwamba, mafuta yamepanda katika soko la dunia, lakini najiuliza ni kwa nini tusiwe tunachukua yale mafuta ambayo ni *raw* ili yafike hapa yaweze kuprosesiwa na katika kuprosesiwa tunaweza pia tukapata lami ambayo tumekuwa tunaagiza kutoka nchi za nje? Tukileta mafuta ghafi kwa vyovyote vile bei itapungua. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, tuna kile kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi cha *TIPER*, kwa nini tusiwe tunaleta mafuta ghafi ili tuweze kupata pia lami ambayo ni *by-product* ya mafuta hayo? Hii pia itapunguza sana gharama za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nijielekeze katika ukurasa wa 40. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameelezea kwa kina, suala zima la ajira na uwezeshaji kwa wananchi kiuchumi na ameeleza kwamba: "Katika kutekeleza Sera, Mikakati na *Program* hizo, napenda kusisitiza kuwa eneo la kujiajiri binafsi ndilo lenye nafasi nyingi za ajira". Nakubaliana kabisa na Waziri Mkuu lakini kinachoshangaza ni kwamba, tuchukulie mfano wa Dar es Salaam pale Kariakoo, sasa hivi tumekuwa na Wamachinga wa Kichina, ambao kwa kiasi kikubwa sana, wamechukua ajira za watu wetu. Sasa naomba kuwauliza hasa wale ambao wameshakuwa Mabalozi kwenye nchi mbalimbali, hivi kuna nchi duniani inayokubali raia wa nchi nyingine, kwenda kufanya umachinga kwenye nchi zao? Nilikuwa naomba Waziri wa Mambo ya Ndani, atueleze hawa watu wana *status* gain, kwa sababu wanaoonekana kule ni watoto. Kwa hiyo, tunataka kujua

hawa watu kweli wana vibali vya kufanya hizo kazi? Kama hawana kwa nini wapo, hata kama wanazo basi kwa nini wasipewe watu wengine? Hizi kazi ni kwa ajili ya wananchi wetu, wakati huo huo Ilani ya CCM inasema kwamba, inataka kuongeza ajira, sasa najiuliza hizi ajira zinatoka wapi kama watu wa kutoka nchi za nje wanakuja kufanya ajira hizi ndogo ndogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, tuwe tunajua kabisa sera ya uwekezaji ikoje ili tuweze na sisi kama tunaweza kuwapeleka vijana wetu China wakafanye umachinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye suala zima la UKIMWI, ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelielezea. Ni kweli Tanzania ilishatangaza kwamba, tuna janga la UKIMWI hilo kila mtu analielewa lakini katika *figures* alizotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, anasema kwamba, tuna idadi ya watu karibu milioni 2.5, ambao wameathirika lakini hapohapo anasema kati ya hao ni 27,000 ambao wanapata hizo dawa. Kwa mahesabu ya haraka haraka ni asilimia 1.08 tu, sasa najiuliza hao wengine wote wanatagemea dawa kutoka wapi? Serikali ina vigezo gani kuwapa hao watu madawa hayo na ni kwa nini wawe wachache kiasi hicho na madawa yapo? Lakini pamoja na hayo, tunaona kwamba, hizi *ARVs* ziko kwenye mahospitali ya rufaa tu, labda sasa tunajiuliza wale wagonjwa wengi ambao wako vijijini wanapataje hizi huduma za *ARVs?* Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba wakati Waziri Mkuu, akifanya majumuisho, atusaidie kutueleza inakuwaje namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hoja zangu. Awali ya yote, wakati Mheshimiwa Rais anaongea, alisema kwamba na ninanukuu: “Serikali yake itahakikisha inaendeshwa kwa sheria, kwa maana ya kuwa Serikali itataka kuona hakuna mtu anayekuwa juu ya Sheria na kuhakikisha kuwa, haki za msingi za raia zinaheshimiwa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo ni hapa karibuni tu tumeona mambo ya ajabu sana yanatokea, tumeona ghorofa pale Chang’ombe likiporomoka, lakini naomba nichukue fursa hii, kumshukuru sana Waziri Mkuu, kwa ule utayari aliokuwa nao na uharaka wa kuweza kutatua lile tatizo. Tumeona Tume imeundwa ya ukaguzi, lakini tunajua pia inatumia pesa za mlipa kodi. (*Makofi*)

Pia tumeona kule Mererani ajali mbaya sana iliyoua zaidi ya watu 50, tunajiuliza hivi haya magari mpaka yanabeba abiria zaidi ya uwezo wake, Askari wa Barabarani hawakuwepo au haya magari yalikuwa yanapita hewani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuhusu kuporomoka kwa ghorofa na sasa hivi Tume kuanza kufanya kazi zake, tunajiuliza hivi hakuna Baraza la Kukagua majengo? Kama lipo basi lilikuwa wapi mpaka maafa makubwa kama haya yanatokea? Kwa hiyo, tunadhani tutapata majibu baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo ajali ya juzi niliisoma kwenye gazeti kwamba, baada ya kuua nadhani karibu watu 80, amepewa ya shilingi 40,000, hivi

najiuliza ni kweli roho za watu hawa 50 na zaidi mtu anapata faini ya shilingi 40,000 tu au hii ni *advance payment*? Kwa hiyo, ninadhani tutahitaji maelezo ni kwa nini inakuwa hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niongelee suala zima la usafiri wa daladala. Mimi natokea Dar es Salaam, kwa hiyo, nilikuwa naomba nielezee adha wanazopata wasafiri hasa kutokana na kufungwa kwa kituo cha Mwenge na hivyo sasa hivi kutumia kituo cha Makumbusho. Haimwingii mtu akilini, kuona ni kwa nini watu wanaotoka Posta au Kariakoo kuelekea Mwenge, washushwe pale Makumbusho, halafu waanze kutembea kwa miguu. Ni kwa nini basi yale mabasi yasiondoke yaende mpaka Mwenge, yawashushe abiria wa Mwenge, halafu yachukue safari ya kupitia Afrikasana ili kuchukua hii barabara ya Shekilango na kurudi Posta/Kariakoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona kwa kweli wananchi wanateswa bila sababu yoyote ile, kwa sababu kama tunajua kituo cha daladala, yaani *Bus Terminal* pale Dar es Salaam, kinahitaji kiwe na vigezo vya namna gani. Sasa hivi ile *Bus Terminal* ya Makumbusho, haifai na ninadhani wahusika wa Manispaa ya Kinondoni, hawakutumia kigezo cha aina yoyote zaidi ya kuwadhalilisha wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielekee kwenye suala zima la Elimu na Mafunzo. Ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo, aliongelea kuhusu suala zima la upungufu wa Walimu. Tunajua kwamba, tuna upungufu wa walimu 5,793, lakini mimi binafsi na labda na wenzangu, sioni ni kwa kiasi gani mwanafunzi anayemaliza kidato cha sita, apewe kozi ya mwezi mmoja aende akafundishe wanafunzi wenzake wa sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba turudi nyuma katika historia yetu ya suala zima la *Universal Primary Education (UPE)*, ambapo kwa kiasi kikubwa kweli Tanzania ilipata tuzo ya *UNESCO*, kwa sababu kwa kiwango kikubwa, wananchi waliweza kujua kuandika na kusoma. Watu wazima wote waliweza kujua kuandika na kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ieleweke kwamba, *program* ile ilikuwa na matatizo makubwa na tatizo kubwa lilikuwa ni kuchukua wanafunzi waliomaliza darasa la saba kuwafanya wawe walimu wa shule hizo hizo za msingi. Kwa hiyo, naona Wizara inachotaka kukifanya ni kuturudisha kulekule kwamba, tumeshaona makosa yaliyotokana na *UPE* lakini sasa hivi tunataka tena tuchukue walimu waliomaliza Kidato cha Sita na mwanafunzi huyo hatujui amefaulu kiasi gain, hata kama amepata *Division One*, bado sasa hivi wanafunzi wetu tunaelewa kwamba, hawasomi kwa ajili ya kuelimika, bali wanasoma kwa ajili ya kufaulu mitihani tu. Sasa wanafunzi hao wakitoka wakaenda kufundisha wanafunzi wenzao, sioni kama tutapata *product* nzuri ya wanafunzi hao kuweza labda kujiunga na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee kusema kwamba, ni kwa mlolongo huohuo basi kwa sababu sasa hivi tunaendelea kuongeza vyuo vya elimu ya juu na kwa kuwa wanafunzi wengi watakwenda kule na sijasikia hata mara moja ni vipi *lecturers* nao wanaongezwa? Kwa hiyo, ninaamini itafika mahali pia wanafunzi wanaomaliza Chuo

Kikuu na kupata *First Degree,* wataambiwa wawe wanapewa *program* ya mwezi mmoja au wiki moja waweze kufundisha wanafunzi wenzao wa Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo naomba nitoe ushauri, kwa sababu wale wanaosoma *Education,* vyuo vingi vikuu siku za nyuma ilikuwa ni miaka mitatu, sasa hivi wameongeza mwaka wa nne ambao kwa mantiki ya kawaida, sioni ule mwaka wa nne yule mwanafunzi anafanya kitu gain, kwa sababu unakuta anarudia zile programu za *first year, second year* na *third year*. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Wizara iangalie ni jinsi gani inaweza kukutana na wanataaluma ambao nina hakika, Wizara hiyo inao wengi, wakae waangalie ni jinsi gani wanaweza kusaidia ili kupata walimu wa vyuo vikuu, hasa wale ambao wamesoma Ualimu. Pia wale ambao wame-*graduate* lakini hawakusoma Ualimu, walau hawa wapewe *program* ya mwezi mmoja au miezi miwili, waweze kwenda kufundisha wanafunzi wa sekondari. Kwa kweli sikubaliani kabisa na suala la mwanafunzi aliyehitimu *form six, whether* amepata *division one* au *two* kwenda kufundisha mwenzake wa *form one* au *form three,* kwa sababu ualimu una *ethics* zake. Ni lazima mtu awe amepitia *methodologies,* kwa hiyo, kumtoa mwanafunzi wa *form six* kwenda kufundisha sekondari, naona hilo ni ni kujiongezea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee suala zima la miundombinu. Itakumbukwa kwamba, siku za nyuma wakati Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Augustine Mrema, alipokuwa hapa Bungeni, alifanya jitihada kubwa na akaweza kuwahamasisha wananchi wa Marangu na Kilema, kujenga barabara. Wananchi wale wamekata kahawa zao na mimea yao mingine ili kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami. Inasikitisha kuona kwamba, Serikali imegharamia lami mapipa kama mia na ushee hivi yalikuwa pale Marangu lakini barabara ile mpaka leo haikujengwa, lami ile imeharibikia pale. Sasa sielewi kwamba, ni kwa sababu zipi nadhani ama ni sababu za kisiasa au za kiuchumi, hilo silielewi. Naomba Serikali ilifafanue hili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kweli ile barabara iangaliwe upya ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, kwani barabara ile si tu kwamba ni kwa ajili ya wananchi wale, lakini ile barabara ikumbukwe kwamba, inakwenda kwenye hospitali ya Kilema, ambayo inasaidia sana wagonjwa wengi kutoka sehemu mbalimbali za Mkoa wa Kilimanjaro na nje ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee pia suala zima la walemavu, Mheshimiwa Bujiku Sakila ameliongelea lakini na mimi naomba niliongelee kidogo. Nilipokuwa pale Chuo Kikuu, nilikuwa mlezi wa walemavu. Kwa kweli kundi hili la walemavu limesahaulika kabisa katika nchi yetu ya Tanzania na imekuwa sasa ni kazi ya watu binafsi kuwasaidia na mara nyingi tumeona kwenye vyombo vya habari, Ndugu Reginald Mengi, akiwahudumia wale walemavu, lakini Serikali sijaona kwa kiasi gani imewasaidia. Hata wale wachache ambao wamepata bahati ya kwenda mpaka vyuo vikuu, wameachwa solemba wanateseka, hawana huduma za aina yoyote, inakuwaje Serikali ishindwe kuwahudumia wanafunzi zaidi ya 10 waliopo Chuo Kikuu kwa kuwanunulia magari *(motor tricycle).*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataala*, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu, lakini pia uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura asilimia 99.9 kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Niwapongeze sana wote wale ambao waliteuliwa juzi na Halmashauri Kuu, kuanzia Mheshimiwa Yusuph Makamba, kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kuwa Katibu Mwenezi, Mheshimiwa Rostam Azizi, kuwa Mweka Hazina, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, kuwa Katibu-*Organisation*, Mheshimiwa Jaka Mwambi, kuwa Naibu Katibu Mkuu na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kuwa Katibu wa Siasa wa Mambo ya Nchi za Nje. Nawapongeza sana, nawatakia kila la kheri, ni matumaini yetu kwamba, watatuongoza sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha pamoja na wasaidizi wake wote, Mawaziri wote walioko chini yake na Mheshimiwa Katibu Mkuu, ndugu yangu Vicent Mrisho, kwa kazi nzuri na bajeti nzuri waliyotuletelea. Nawatakia kila la kheri na mafanikio katika utekelezaji wa bajeti hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Ndugu yangu, Mbunge mwezetu wa zamani Mheshimiwa Ole-Kone kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida. Sisi watu wa Singida tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa uteuzi huo, lakini tunamshukuru zaidi kwa kuamua kumleta Singida badala ya kumpeleka mahali pengine na tunaamini kwamba, tutanufaika sana kwa uteuzi huo. Kwa kufanya kazi naye Mheshimiwa Ole-Kone, kwa sababu tunajua sisi kama Wabunge na yeye alikuwa Mbunge, anajua matatizo yetu na nina hakika atatusaidia sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Lakini nampongeza vilevile kwa sababu baada ya kufika tu amefanya kazi nzuri kwa kipindi kifupi, amelishughulikia vizuri suala la njaa kiasi kwamba, watu wote waliostahili wamepata chakula na ameshughulikia sana agizo la Waziri Mkuu, kuhusu mambo ya Elimu kiasi kwamba, tumejenga sekondari mpya 34. Nampongeza sana Mheshimiwa Ole-Kone. (*Makofi*)

Lakini sitamtendea haki Mheshimiwa *DC* wangu, *Capt.* James Lyamungu, amefanya kazi nzuri na anaendelea kufanya kazi nzuri, anaweza asinielewe. Nasema katika hii panga pangua inayokuja, tuachieni Lyamungu Singida, kama hamumpi cheo, kama akipata *promotion* maana ziko nafasi mbili za Wakuu wa Mikoa, inawezekana zikatokea basi mpeni *promotion*, lakini kama ni *DC* hebu tuachieni Singida aendelee kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niipongeze Serikali ya CCM kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi walivyosaidia na kutatua tatizo la njaa Mkoani Singida. Sisi ni miongoni mwa mikoa na wilaya, zilizokuwa zimeathirika sana, lakini kwa juhudi kubwa ya Serikali yetu, ahadi ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji tumefanikiwa sana katika kupata chakula cha njaa. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nipelekee salamu kwa Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri mliyoifanya na Mawaziri wako waliokusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizo, nataka nibainishe matatizo mawili: Moja nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu, ujue kwamba, bado kuna maeneo hivi sasa yana matatizo ya njaa. Tarafa ya Sipuka ni miongoni mwa Tarafa ambazo zimeathirika kwa sababu wenzetu kule ambao tunapakana nao wa Tabora, wanapata mvua nzuri lakini mwaka huu mvua haikuwa nzuri kwao, watakuwa na tatizo la njaa. Katika Tarafa ya Ikungi nao watakuwa na tatizo la njaa.

Kwa hiyo, naomba ku-*register* tatizo hilo ili Serikali ianze kujipanga, kwa sababu pamoja na jitihada zote ambazo wamefanya, wakulima wa Mkoa wa Singida, wamejituma kweli kweli, kwa sababu ya ukosefu wa mvua kutakuwa na njaa nitaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na viongozi wetu ya kugawa chakula, lakini yapo malalamiko kwenye eneo moja. Katika vigezo vile ambavyo tumejiwekea vya kugawa chakula kulikuwepo na kigezo kimetumika hasa katika Jimbo langu kwamba, wazee na vikongwe, ambao watoto wao wako Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Moshi, kwa kudhaniwa kwamba, wanafanya kazi, basi wazee wale na vikongwe wale hawakupewa chakula.

Kwa kweli ni bahati mbaya sana, kwa sababu mtoto kuwa Dar es Salaam, wewe unajua na Waziri Mkuu anajua, siyo maana ya kwamba, kwa sababu yupo Dar es Salaam basi ana kazi, eti kwa sababu yupo Arusha ana kazi, ataweza kumsaidia mzazi wake, kwa hiyo, hili kwa kweli limezua malalamiko makubwa. Naomba kigezo hiki kiondolewe.

Kama ushahidi upo kwamba, yupo mtoto Dar es Salaam anaitwa Missanga, anafanya kazi analipwa mshahara, nasema sawa lakini isichukuliwe tu kwamba, maadamu yupo Arusha au yupo nje ya Singida, basi mtoto wake anatakiwa amletee. Sawa lakini yeye mwenyewe anangojea chakula cha mgao, leo atampelekea baba yake na mama yake?

Ningeomba sana katika utaratibu ujao, kigezo hiki cha kuwanyima wazee na vikongwe chakula eti kwa sababu watoto wao wako Dar es Salaam, kiondolew, lakini wakati wa chakula unasema hapana, wewe mtoto wako yuko Dar es Salaam, mbona kwenye kura hamkumwambia akapige kura Dar es Salaam? Ningeomba sana hilo liangaliwe na liondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kulielezea ni suala zima la ugawaji wa Wilaya. Mkoa wa Singida kama unavyofahamu, unatokana na Mkoa wa

Kati *(Central Province)*, ambao uligawanywa mwaka 1963 na kutoa Mkoa wa Singida, Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Iramba. Lakini Wilaya hizi ni za kikoloni za mwaka 1940 na 1950 siyo kwamba ni Wilaya mpya ambazo zilianzishwa baada ya kuundwa huu Mkoa wa Singida, la hasha. Ni Wilaya ambazo zimekutwa toka enzi ya ukoloni au maboma, kwa lugha ya kiutu uzima. Maboma ya ukoloni yamekuwepo hapo hadi hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachonisikitisha ni kwamba, pamoja na kwamba viongozi wa Mkoa walionitangulia wamejitahidi sana kutaka Wilaya hizi zigawanywe (Wilaya ya Singida, Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Iramba), lakini hakuna mtu aliyesikia, kiasi kwamba, Wilaya hizi hazijagawanywa ingawa ni za kikoloni. Lakini zipo Wilaya ambazo zimeanzishwa baada ya uhuru zimeshagawanywa. Hizi ambazo zimekutwa toka enzi za ukoloni hazijagawanywa. Mambo chungu nzima yamefanyika na viongozi chungu nzima wameenda mara kwa mara kuuona uongozi wa juu, lakini hakuna chochote kile ambacho kimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mkoa huu unaanzishwa ulikuwa na wakazi 220,000 tu. Sasa hivi Mkoa wa Singida una wakazi 1,400,000, bado Mkoa ni huo huo na Wilaya hizo hizo. Sasa linganisha kutoka wakazi 220,000 mpaka wakazi 1,400,000. Nadhani si vibaya nikasema kwamba, Singida hatutendewi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya utafiti na kuona kwamba, zipo Wilaya kama nilivyosema, zimegawanywa mara kadhaa tu. Nyingine ilikuwa Wilaya moja zimekuwa Wilaya tano, nyingine Wilaya moja zimekuwa Wilaya tatu na kadhalika. Sasa kwa nini isiwe Singida? Kwa mfano, nisamehe nataka nitoe mfano ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu anaujua. Ningeweza nikaeleza mengine lakini mfano mzuri utakuwa ni ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu anaufahamu wa Wilaya ya Masai. Wilaya ya Masai imegawanywa ikatoka pale Wilaya ya Monduli, Wilaya ya Ngorongoro, Wilaya ya Longido, Wilaya ya Simanjiro na ikatoka Wilaya ya Kiteto. Wilaya tano ndani ya Wilaya moja; sisi Singida tumekosa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya nyingine ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anaijua ni Wilaya ya Mbulu, imetoka Wilaya ya Babati, Wilaya ya Karatu na imetoka Wilaya ya Hanang, zote hizi zimegawanywa. Hivi sisi Singida tuna matatizo gani Wilaya zetu hazigawanywi? Kama ni idadi ya watu, nimeeleza kutoka wakazi 220,000 kwa Mkoa mpaka wakazi 1,400,000. Hivi sasa Wilaya ya Singida peke yake, ina wakazi zaidi 600,000 na ina Halmashauri mbili. Hivi ni kigezo gani kingine kifanywe mpaka Wilaya hii ionekane? Tunajiuliza tumeikosea nini Serikali ya CCM? Kwa sababu wananchi bila kujali kama ni wana-CCM au si wana-CCM, wameendelea kuichagua Serikali ya CCM kwa kishindo. Mwaka 2005 Mkoa wa Singida ulikuwa wa pili kwa kupiga kura nyingi kwa Rais wa CCM na zawadi tumepewa pale Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu, ambapo Waheshimiwa Wabunge ni sehemu yao mmeshuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 ulikuwa Mkoa wa tatu kupiga kura nyingi kwa Rais wa Serikali ya CCM, tufanye nini zaidi ya hapo? Tuambieni kipi kingine mnataka tufanye ili mtusikilize na sisi, mlete mrejesho nyuma? Watu wa

mahesabu wanasema mtie, mtoe, ndiyo nipe nikupe. Sisi tunafanya kila jitihada katika maendeleo na katika kila kitu na kadhalika. Sasa tumefanya nini, inanitia uchungu, naweza nikafika mahali pengine nikatumia lugha ambayo haistahili katika Bunge lako Tukufu. Lakini nasema tunaonewa na sababu hatuijui. Wilaya nyingine zimegawanywa, Singida haigawanywi, Manyoni haigawanywi, Iramba haigawanywi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama alivyojitahidi kwa Wilaya nyinginezo, ikiwa ni pamoja na zile ambazo nimezitaja, atusaidie na sisi watu wa Singida na kwanza sisi ni jirani zake . *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo: Majimbo ya Wilaya ya Singida (Singida Kusini na Singida Kaskazini), yawe Wilaya kamili, kwa sababu sifa zote zipo. Jimbo langu la Singida Kusini liwe Wilaya na Makao Makuu yake yanaweza yakaenda Ikungi, umeme upo, hospitali ipo, maji yapo ya *KONOIKE*, ilimradi Ikungi kuna sifa zote ambazo zinastahili kuwa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Singida Kaskazini ipeleke Makao Makuu Ilongero, umeme upo, maji yapo, uchumi upo na kadhalika. Wilaya ya Manyoni igawanywe. Itigi inastahili kuwa Wilaya kamili, kwa hiyo, Itigi nayo iwe Wilaya kamili na kadhalika. Iramba igawanywe pia Nduguti iwe ni Wilaya kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujazia haya niliyoyasema, tarehe 23 Septemba, 2005 pale Iguguno, Mheshimiwa Rais aliwaahidi watu kwamba, atahakikisha kwamba, Wilaya za Mkoa wa Singida zinagawanywa na Wilaya ya Iramba itagawanywa. Sasa jitihada zote hizo na *commitment* zote hizo na ahadi ya Mheshimiwa Rais, kuna tatizo gani tena?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri, atuonee huruma sisi watu wa Singida, tunahitaji maendeleo, hatuwezi kupata maendeleo kama bado watu tumelundikana, huduma kwa watu zitakuwa hazifiki katika wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulieleza hilo, katika ukurasa wa 55 kifungu namba 68 cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, limezungumzwa suala la MMES. Mpango wa MMES umepokelewa vizuri na wananchi wa Wilaya ya Singida na Jimbo langu Singida Kusini na wameitikia hivi sasa wamejenga na wanaendelea kujenga Sekondari za Kata, kama nilivyosema Kimkoa tuna Sekondari 34 zimejengwa. Lakini mimi peke yangu katika Jimbo langu, kuna Sekondari 11 mpya zimejengwa ukiacha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajika hapa ni mchango wa Serikali wa kusaidia nguvu za wananchi, ambazo zimeonyeshwa kulingana na Sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba, pale wananchi wanapofanya jitihada ya kuonyesha mfano ya kujenga kitu, basi Serikali nayo inatoa nguvu zake. Hicho ndicho ninachongojea kwa sababu wananchi wametekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, lakini nataka niombe mawili katika Mpango MMES: Mosi, Waraka wa Wizara uliopo sasa ni matatizo matupu haufai kuhusu Mpango wa MMES.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, ambayo kwa mtazamo ukiiangalia, kama mambo yote yaliyotajwa mle yatatekelezwa, yatatupeleka mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda nichukue nafasi hii, niwashukuru wanachama wa Chama cha Wananchi *CUF*, kwa kunichagua mimi kuwa mmoja wa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata leo nimesimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuchangia hoja kama Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda nichukue nafasi hii pia kukupongeza wewe na kukushukuru kwa mshikamano uliouonyesha hasa kwa sisi Wapinzani kuonyesha mshikamano mkubwa kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote wanawake bila kujali itikadi ya Chama chochote. Nakupongeza kwa hilo na naomba Mungu aendelee kukupa hiyo roho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kama nilivyosema naona kwamba, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri, ninachotaka kusema labda ni kuongezea kama ushauri au msisitizo wa yale yote ambayo nimeyasikia katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nizungumzie suala zima la pembejeo kwa wakulima, hasa wakulima wa pamba. Kumekuwa na Bodi ya Pamba, ambayo imekuwa ikikata fedha kwa ajili ya mbegu wakati utakapokuwa umefika ili waweze kupata fedha za kununulia mbegu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu hivi vya pass vimeleta tabu sana kwa wananchi wengi, hasa katika Mkoa wa Shinyanga na Mwanza na wale wote ambao nafikiri wanalima zao hili la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba, mkulima anapokuwa anauza, anakatwa hii fedha kwa upendo. Anashauriwa kabisa kwamba, hii fedha itakusaidia wakati utakapokuwa umefika kwa ajili ya kununua mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapokuwa umefika wakati, huyu mkulima anapohitaji kununua ile mbegu, anapangiwa ni kiwango gani ambacho ataweza kununua. Wakati mwingine unakuta yeye anahitaji gunia moja la mbegu, lakini wale ambao wamekata fedha yake na tayari fedha yake wanayo, wanampangia wanamwambia kwamba, utachukua debe moja au madebe mawili, wakati yeye amekusudia anataka labda gunia moja ambalo linatosheleza shamba lake la pamba, ambalo anategemea kupanda katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimekuwa nikijiuliza ni kwa sababu gani hii bodi imeng'ang'ania sana katika eneo hilo kwa ajili ya kumnyanyasa mkulima wa pamba? Kwa uzoefu ambao nimeuchukua katika eneo lile, kwa kweli nimeona hauna maana yoyote, kwa sababu kama wangekuwa na nia njema ya kumtunzia mkulima, Wasukuma wana mazao mengi wanayolima, kama viazi na mahindi. Hili la pembejeo kwa nini lisiende kwenye mahindi na viazi, linang'ang'ania kwenye pamba? Sasa unakuta mkulima anapata shida ni kwa nini hiyo pesa asijitunzie yeye mwenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nikawa nawauliza wale wanaosema kwamba, Wasukuma wanapokuwa wamepata pesa wanakunywa sana pombe, wakinywa sana pombe wanakuwa ile pesa wanaimaliza, ikifika wakati wanakuwa hawana hiyo pesa. Sasa swali linakuja, anapokwenda mnadani kuuza ng'ombe nani anayemtunzia zile pesa? Msukuma anaenda kuuza ng'ombe, anachukua pesa anaweka mfukoni na anaendelea kuwa na mifugo yake kama kawaida. Sasa swali linakuja hawa ni watu gani wanaong'ang'ania kwenye eneo hili la mbegu na kama wanang'ang'ania kuchukua hiyo fedha kwa ajili ya kuwatunzia, basi inapokuwa imefika wakati, wapewe pesa kama jinsi alivyoihifadhi mle, maana yake ile pesa ni ya kwao. Sasa kama ile pesa ni ya kwao, kwa nini wakati unapofika apangiwe kiwango?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu nilikuwa nafikiri kwamba, ifikie mahali waangalie sana katika eneo hili la pembejeo. Kweli mkulima anateseka sana, yaani hakuna chochote anachokipata juu ya utunzwaji wa hiyo pesa yake. Nilikuwa nashauri kwamba, ikiwezekana mkulima ajitunzie pesa yake kama miaka iliyopita. Historia ya zao la pamba siyo kama imeanza juzi au jana, kabla hatujazaliwa Msukuma tayari alikuwa analima pamba. Lakini sasa umekuja ukiritimba, eti wanamtunzia pesa. Sasa ukitafakari sana unaweza kukuta kuna kitu ambacho kinaingia humu katikati, kusababisha huyu mkulima ambaye ni mtu wa chini, maskini, anashindwa kufaidi sana lile zao lake unapokuwa umefika wakati wa kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda tena kuongelea suala zima la Wizara ya Mambo ya Ndani, kuna kitu kimoja ambacho nimekiona kwa muda mrefu kimekuwa sugu sana. Wananchi wamekuwa wakiteseka sana wanapopata tatizo hili, hasa hao watu wanaokamatwa na kuwekwa ndani, linapokuwa limetokea suala la mauaji. Sawa kabisa, wala sikatai wawekwe ndani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ni Wizara ya Mambo ya Ndani au Wizara ya Usalama wa Raia?

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Usalama wa Raia, samahani. Wizara ya Usalama wa Raia, nilikuwa nawaomba labda wajaribu kuangalia tena hili suala, kwa sababu unapokuwa umefika wakati limejitokeza suala la mauaji na bahati mbaya sana suala la mauaji likitokea, wanakamatwa watu wengi kwa sababu wanakuwa hawajajua ni nani kahusika. Sasa wanapokuwa wamewekwa ndani, wale watu wanaweza wakakaa hata miaka 10, kuna watu katika Wilaya ya Maswa wamekaa miaka 10 au 11, wapo kabisa hata mkiniambia sijui kuhusu mwongozo nina ushahidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anawekwa ndani kwa miaka 9, miaka 10, hivi huyo mtu hata akija kuhukumiwa si ameshafungwa tayari? Hebu fikiria hata kama ungekuwa ni wewe, unawekwa ndani wanakwambia upelelezi unaendelea, upelelezi unaendelea, unaendeleaje? Tanzania bwana, ukiangalia historia yake ni watu maarufu sana kwa suala la upelelezi, hilo liko wazi wala siyo siri. Sasa inapofikia wakati wa mauaji, hili linakumbatiwa kwamba, upelelezi unaendelea, kumbe upelelezi unaendelea wanatoa nafasi ya kutoa rushwa huku chini ili wajue jinsi gani upelelezi umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri ifike mahali kwa kweli hao watu waangaliwe, ambaye ana hatia anahukumiwe na ambaye hana hatia, basi aruhusiwe. Nilikuwa nafikiri suala hili ni la msingi na hasa Vijijini watu wanateseka mno. Vijijini watu wakishawekwa ndani, hakuna mtu wa kuwasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika katika Wilaya yangu ya Maswa au katika Mkoa mzima wa Shinyanga, Wasukuma ni watu ambao ni wataratibu mno. Sasa yule akishakamatwa, askari akishakwenda pale akamwambia bwana ndiyo unafungwa, anamwambia twende zizini kwangu, nitakupa ng’ombe wangu hata 20. Sasa utakuta Msukuma anateseka kweli, hakuna mtu anayeogopa kwenda jela kama Msukuma, siwezi kujua katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli suala hili tulipe kipaumbele mno. Naomba tafadhali, utawala huu wa Awamu ya Nne unaonekana uko makini, watawala wako makini, vijana kibao, tunaomba suala hili mlishughulikie kwa umakini, mjaribu kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea tena suala zima la Huduma ya Afya, hasa kwa akinamama. Nasikitika sana na mimi ni mwanamke, yaani unakuta akinamama wengi kule Vijijini wengine wanakufa kwa ajili ya kukosa vifaa eti vya kujifungulia. Hebu angalia, kifaaanachoambiwa ni mpira *(gloves*), anaambiwa wembe, sijui na vitu gani vingine. Msukuma mwingine akitoka kijijini anashangaa, mpira tena, wa kufanyia nini, haelewi mpira ni nini na mpira unahusikana na nini. Sasa anashangaa anajiuliza huko ndani wanaenda tena kucheza mpira, watu wenyewe wagonjwa wanacheza kitu gani huko? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba kwa kweli, Wizara ijaribu kuangalia akinamama wanadhalilika kupita kawaida. Yaani ikifika wakati wa kujifungua, ukimkuta mama utamwonea imani, hali ni mbaya kweli kweli. Siku moja

nilikuwa nasema ingewezakana tukamwomba Mwenyezi Mungu, hawa akinababa wakaanza kujifungua, hili suala wangelimaliza hata leo. Maana yake uchungu unapokuwa umefika, inawezekana mama hata asikuelewe kwamba wewe ni mwanaume, gauni hana na kila kitu hana. Sasa akishajifungua ndiyo anajua yule ni mwanaume, hali inakuwa ni mbaya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nafikiri suala hili la vifaa vya kujifungulia ni dogo sana. Ni aibu hata wanaotusikiliza, eti mama anafika mlangoni wanamwambia samahani vifaa viko wapi? *Nurse* wakati huo kachachamaa anasema starehe yako isinipe shida babu. Yaani hao watu nao ni wa kuangalia kwa makini. Anashindwa kuelewa kwamba, huyo ni mwanamke mwenzie na sasa anahitaji kujifungua. Yule mama hana mpira, hana wembe na hana kitu chochote, anaulizwa mume wako umemwacha wapi, leo ndiyo umejua kumwacha mume wako nyumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafikiri suala hili kwa kweli Wizara ijaribu kuliangalia, wanawake wanadhalilika mno ikifika wakati wa kujifungua. Yaani wanapata tabu kweli kweli. Mama anaweza akapata shida na akateseka, yupo hapo hapo, *nurse* hawezi kumuhudumia kwa sababu ya kukosa vile vifaa. Sasa nafikiri Wizara iangalie, ikiwezekana basi lipatikane fungu jamani na hivyo vifaa ni vitu rahisi mno, mpira sijui shilingi 500 au 1,000, wembe na wenyewe sijui shilingi 20, sasa vitu kama hivyo vinatudhalilisha wanawake jamani, hata nyie akinababa mmetoka kwetu angalau mjaribu kutupa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kurudi kwenye mikopo ya akinamama, hili naliongelea kwa uchungu kwa sababu gani? Nilitegemea Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wengi wangekuwa wanazungumzia akinamama kupita watu wote. Niulize kwa nini? Chama cha Mapinduzi kimepata kura nyingi mno kutoka kwa wanawake, isingekuwa wanawake kwa kweli hayo yote yasingekuwepo. Nawaambia kweli wanawake wamefanya kazi kubwa mno, kuwapatia kura na ni mtaji mkubwa sana wa Chama cha Mapinduzi. Sasa nikawa najiuliza, unapokuwa umefika wakati, mbona hata mkizungumza sisikii mkizungumzia juu ya hawa akinamama? Hawa akinamama inatakiwa kuwajali, siku tukiwajali sisi *CUF*, mjue kwamba, Serikali imekwenda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kwa kweli hawa akinamama wajaribu kuangaliwa na kitu kingine ambacho sasa hivi kimeingizwa, wamewafariji akinamama kwamba, kuna watu wanatoa mikopo kama *FINCAR*, *PRIDE*, akishindwa kulipa yule mama, wiki moja wameshafika kwake kinabebwa kitanda, godoro, eti wanamkwamua badala yake wanachukua hata kile alichokuwa nacho kinaondoka! Nafikiri waangaliwe hata wale watu wanaokopesha mikopo, wajaribu kuiangalia ile riba, wakusudie kumsaidia mama, siyo kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa mwanachama wa *FINCAR* mpaka juzi nilipopata Ubunge, ndiyo nikajitoa. Kwa hiyo, nilichojifunza mle, wale wanafanya biashara, wala hawamsaidii mwanamke hata siku moja. Kwa hiyo, nafikiri suala hili,

wajaribu kuliangalia ili huyu mama atoke mahali alipo, ajaribu kunyanyuka hata mtakavyojieleza kule mwaka 2010 watawaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa napenda kuchangia suala zima la Madiwani. Jamani yaani wote tuliomo humu, ikifika wakati wa uchaguzi, mtu wa kwanza kusema naye ni Diwani sijui nani atakataa? Yaani kwanza, utakayemwendea ni Mheshimiwa Diwani, watu wako vipi katika Kata yako; Mheshimiwa Diwani unasemaje kuhusu hili? Takrima zilikuwa zinaenda kwa Madiwani kibao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashindwa kuwaelewa unapokuwa umefika wakati basi na wao tujaribu kuwasemea, kwa kweli Madiwani wako katika hali ngumu. Katika kipindi kilichopita nilikuwa Diwani. Diwani ana kazi ngumu, ana watu kwake kibao, chakula anachopika kwake hata kwako hukipiki, yaani ana shida kweli. Lakini maslahi yao kwa kweli yamekuwa ni madogo, angalau tufike mahali na yeye apate mshahara hata kama siyo mkubwa, angalau uwe wa maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bila Madiwani kwa kweli hatuna nguvu yoyote, tunapokuwa huko Madiwani wanafanya kazi yetu na tunapokuwa huku tunafanya mawasiliano nao. Basi angalau na wao wajaribu kupata faraja kwamba, hata sisi wenzetu wanatukumbuka. Madiwani mnasikia, nimewaambia wenzangu wamesikia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala zima la wafanyabiashara wa mkaa hasa vijijini, popote pale wanapouza mkaa vijijini. Sasa sielewi wenzangu kule mliko, lakini ninachotaka kusema ni maeneo yote wanayouza mkaa, wafanyabiashara wadogo wadogo. Wafanya biashara wadogo wadogo nafikiri wangepangiwa kiwango cha leseni zao, za kuuza mkaa. Unakuta mtu ana madebe mawili, anakutana na mtu wa maliasili anamwambia ampe leseni, leseni inazidi madebe mawili. Hivi huyo sasa atauza mkaa au ndiyo basi na hayo madebe mawili anategemea kununua chumvi na daftari la mtoto. Huyu mfanyakazi wa maliasili, anamwambia chukua mkaa weka hapa. Hela ya kulipa hana, anategemea auze mkaa ndiyo alipe na hela yenyewe anayotakiwa kulipa haitoshi hata akiuza huo mkaa.

Mheshimwia Naibu Spika, nafikiri Wizara ya Maliasili na Utalii, ijaribu kurudia kuangalia wafanyabiashara wa mkaa ni wananchi maskini na ni wananchi wa hali ya chini mno wanatafutia kipato, hebu wajaribu kuangaliwa na wao wapate nafasi ya kuweza kujipatia angalau kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala la watoto ambao walichaguliwa katika *second selection*, awamu hii ya juzi iliyopita. Ninachotaka kusema hapa, hawa wanafunzi wamechelewa kuingia katika shule za sekondari. Sasa sijui kuna nini kitakachofanyika ili waweze ku-recover yale masomo ambayo wenzao walishaanza kuyasoma. Kwa sababu wanapokuwa wanafanya mtihani, mtihani wao unatoka sawa na wale ambao wameshasoma. Kwa hiyo, wale watajikuta kwamba, wamerushwa hawajafika pale ambapo wenzao wamefika. Nafikiri kupitia Awamu hii ya Nne ya Utawala wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, waangaliwe hawa watoto,

ikiwezekana hata wakati wa likizo, wawaongezewe muda wasipumzike ili waweze kuziba lile pengo ambalo wenzao walikuwa wameshaanza kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama nitamaliza, nataka kuongezea kuhusu walimu. Naweza nikasema kwa kweli hata Wilaya yetu ya Maswa, tumejitahidi sana, tuna shule nyingi za sekondari katika Kata. Lakini kitu kikubwa ambacho nimekiona kina matatizo, ambacho ningeshauri kifanyiwe kazi ni kwamba, walimu hakuna. Kuna shule nyingine hata huko niliko unakuta shule nzima ina walimu wawili tu. Yaani unakuta inakuwa ni kazi ngumu, lakini bado mtoto akishindwa mtihani, wanasema amefeli. Si kweli kwamba amefeli, isipokuwa ameshindwa kufikishwa mahali ambapo angeweza kufika. Walimu hawatoshi na yule mwalimu hawezi akajigawa. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, angalau wajaribu kuangalia ni jinsi gani watafute angalau hata kama ni kuchomoachomoa sehemu, walimu waweze kupatikana ili waweze kuwasaidia hawa watoto, waweze kupata masomo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tena kusema hata nyumba za kuishi hawa walimu angalau katika kila shule iwepo nyumba angalau mmoja au mbili. Kuna sehemu nyingine kuna shule, lakini nyumba jamani inakuwa ni matatizo kweli. Kwa hiyo, ndiyo maana unakuta hali ni ngumu, mwalimu badala ya kufikiria atamfundisha nini motto, anaanza kuwaza ataishi wapi. Mwalimu hawezi akafundisha mtoto wakati anawaza ataishi wapi, itakuwa ni ngumu sana. Naomba na hili lifanyiwe kazi. Mungu amenijalia nafasi bado ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine cha mwisho ambacho nataka kusema ni kwamba, kuna shule nyingine za msingi ambazo mtoto asipoenda shule, mwalimu anamwomba shilingi 100, sasa sijui kama utaratibu huo upo leo, labda tutapata majibu. Vijijini mtoto asipoenda shule, badala ya kutandikwa viboko, eti anaombwa shilingi 100! Sasa sielewi, inawezekana ni ukata wa kipindi cha nyuma kwa walimu na kwa kuwa sasa hivi wameboresha maslahi yao, labda hali itakuwa nzuri.

Kwa sababu hata huyu mwalimu kila mahali mtu anaangalia marupurupu. Sasa mtoto akiombwa pesa, kesho haendi shule kwa sababu anajua atampa mwalimu shilingi 100 kwani kuna shida gani. Kwa hiyo, unakuta hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watoto hao wataiba hela nyumbani, watapeleka shule na itasababisha wawe watoro kwa sababu uwezo wa kulipa shilingi 100 wanao. Naomba Wizara ya Elimu wafuatilie hili suala hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kuwajali Madiwani. Tunapenda kumtambua Mheshimiwa Raphael Msimwita, Diwani wa Kata ya Chirumo katika Jimbo la Mbozi Magharibi na mke wa Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. Ndiyo tumeanza kuwajali jali hivi. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Haroub Said Masoud. Mheshimiwa Lekule Laizer ajiandae na Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia. Lakini kabla sijaanza mchango wangu, napenda kutoa utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyotambua wewe ni miongoni mwa akinamama. Aliyekuwepo kitini asubuhi ya leo ni mwanamama vilevile na Waheshimiwa Wabunge wanawake waliokuwepo hapa, asilimia 30 vilevile ni akinamama. Hii ni uthibitisho kwamba, CCM inawajali akinamama. Si kweli hata siku moja kwamba, CCM haiwajali. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, imetamka na imewajali akinamama. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imewataja, imewatamka na imewajali akinamama. Mimi mwenyewe binafsi, ninawajali akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kwanza nimpongeze Mwenyekiti wetu wa CCM kwa ushindi mkubwa alioupata. Vilevile niwapongeze Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu, kwa sababu juzi walituacha hoi, kuna nyimbo moja inaimbwa unaniacha hoi. Kwa hiyo, na wao walituacha hoi. Kwa nini nimesema hivyo? Walitembea katika ukumbi mzima, hakuwajali Uwaziri Mkuu wala Urais, wakipeana mikono na watu, haijapata kutokea. Wanawajali watu wao na ndiyo maana wakazunguka ukumbi mzima wa Chimwaga, wakiwapa watu mikono na wakizungumza na watu kabla ya mkutano kuanza. Hawakukaa kwanza kwenye meza kuu. Sasa hii ni namna wanavyowajali wananchi. Sasa nasema Mwenyezi Mungu, awajalie waendelee na msimamo huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nisije nikasahau ni kwamba, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja, kwa asilimia mia kwa mia. Imeeleza matarajio yote na imeeleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi kilichopita. Kwa hiyo na mimi nasema kwamba, tuongeze nguvu sote kwa pamoja ili yale yaliyoelezwa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, yaweze kutekelezeka. Lakini vilevile hata speed yake ya kuzungumza Bungeni, ilikuwa ni kubwa na yeye Mheshimiwa Edward Lowassa ni miongoni mwa wale *top ten*, wazungumzaji kwa *speed* humu ndani akiwemo yeye Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. Hawa wakisimama wanazungumza kama cherehani, utaona raha mwenyewe kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme kwanza, mimi binafsi nakishukuru Chama changu cha CCM kwanza, kwa kunipa nafasi katika kura za maoni na kwa kunipa kura za kutosha kabisa ili niwe mgombea. Lakini vilevile kwa Halmashauri Kuu na Kamati Kuu kuridhia ili mimi niwe mgombea wao wa CCM. Vilevile nawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Koani, tena siyo wa CCM watupu, kwa sababu naamini na nawaambia wenzangu pale Wapinzani, walinipa kura nyingi sana, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Awamu iliyopita, nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Mwenyekiti wangu alikuwa Mheshimiwa Sophia Simba. Lakini siku ya mwisho tunaagana katika Kamati, Mheshimiwa Sophia Simba hakuwepo, nikashika mimi nafasi ile, jambo ambalo ni la kihistoria na sitalisahau maishani, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu aliniomba nafasi ili

azungumze machache ya kuagana. Maneno aliyoyatamka ni haya yafuatayo: “Aliniambia kwamba, Makamu Mwenyekiti kwanza, nashukuru kwa ushirikiano wenu mzuri, wewe na Mwenyekiti wako, lakini ninachosema Mungu akipenda tutakutana hapa. Lakini naamini hakuna chama chochote kitakachoweza kutawala katika nchi hii miaka 100 ijayo kama siyo CCM.” Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu alisema.

Mimi pale nikafurahi, nikamkumbatia na nikamwambia kwamba, tutampokea. Kwa sababu maneno yale ni dhahiri kwamba, alikuwa anashuka kwenda katika upande wa pili. Lakini si peke yake na Mheshimiwa Janeth Mashele naye alikuwa katika Kamati hiyo, alitamka maneno yale yale, isipokuwa yeye hakuyatamka kwa dhahiri, aliyatamka kwa siri, alituambia kwamba, mimi nitarejea kwetu na nimemwona juzi Chimwaga pale, yeye na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Sasa hii ndiyo hali ya kisiasa na ya nchi. Unapoona kwamba, upande huu hauuelewi, nende kule, umeona *Imamu* hajui kuswalisha mfuate *Imamu* anayejua kama Haroub Said Masoud, ya nini kumfuata *Imamu* ambaye hajui kuswalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni hapa liliulizwa swali na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Jimbo la Muyuni, kuhusu hoja ya sarafu ile ambayo Marehemu Muasisi Karume, alikuwa hajawekwa katika sarafu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, amwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, tunakumbushia katika Bunge la mwaka 1995/2000, ililetwa hoja Bungeni na aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge Paul Ndobho, ambayo alitamka wazi kabisa kwamba, sura ya Marehemu Nyerere na Marehemu Karume, ziwekwe ndani ya sarafu yetu.

Waziri wa Fedha wa wakati ule, baada ya mjadala mrefu alikubaliana na wazo lile na akasema kwamba, sarafu zilizochapishwa itakuwemo sura ya Marehemu Karume na sura ya Marehemu Nyerere. Mheshimiwa Dr. Mwita Haji Mwita, alipozungumza hapa alieleza wazi kabisa kwamba, sura ya Marehemu Nyerere ilikuwemo lakini ya Marehemu Karume mpaka leo haipo. Sasa si suala tena kama alivyolijibu Mheshimiwa Waziri ya kwamba, kuomba ridhaa. Ridhaa ilikuwa imeshapatikana na Waziri amekubali ndani ya Bunge kwamba, sarafu itachapishwa na sura ya marehemu ikiwemo. Sasa naikumbusha Serikali kwamba, agizo lile lilishakubaliwa, hakuna tena utata mwingine wowote ule.

Ingelikuwa tatizo lile halikujitokeza kwamba, mpaka leo haijachapishwa, Mheshimiwa Dr. Mwita Haji Mwita, asingeliuliza swali lile. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala hili tunadumisha Muungano na ni lazima tumuenzi na yule vile vile. Kwa hiyo, nadhani utalichukua na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa humu ndani katika waliosoma dini za Kiislamu mimi naongoza. Lakini vile vile na *Bible* nimesoma. *Bible* inazungumza kuhusu mtu yeyote anayefanyiwa wema, lazima arejeshe shukrani na *Quran* imesema hayo hayo. Lakini mimi nitatoa tafsiri kwa Kiswahili. *Quran* inasema ifuatavyo, napenda kunukuu kwa Kiswahili. Inasema: “Enyi waja wangu mnapofanyiwa wema, kwa wale wanaokufanyieni toeni shukrani juu yao. Lakini ninyi ambao hamtatoa shukrani juu yao, itakuadhibuni adhabu iliyokuwa kubwa.”

Sasa nashangaa hapa kuna watu wanafanyiwa mema mengi, Serikali, Wabunge, Mawaziri wote wanawafanyia wema, lakini hawatoi shukrani. Sasa nasema navipongeza vyombo vifuatavyo: Kwanza, nampongeza kabisa ndugu yangu Mheshimiwa Capt. John Chiligati, ambaye wakati ule tuliungana pamoja, tukazungumza tukapanga mpaka hatimaye amekubali kujenga Ofisi ya Mkoa ya Uhamiaji katika Jimbo langu la Koani. Huu ndio Muungano, wale wanaosema Muungano tunabezwa kule Unguja, si kweli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, basi weka sawa kama alikuwa nani wakati huo?

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Wakati huo alikuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na ilikuwa Uhamiaji iko kwake na bahati nzuri na sasa hivi Uhamiaji iko kwake. Ofisi ile imeshafunguliwa, imepambwa vizuri sana na ukweli inapendeza kuliko hata hayo Makao Makuu yao ya Uhamiaji. Lakini vile vile si hapo tu, Ofisi yako ya Bunge Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya uongozi wenu mlipokuwepo pale wakati ule, tuliomba Wazanzibari tujengewe Ofisi ya Bunge mkatukubalia. Ramani mkaleta, mkapatiwa kiwanja na hatimaye ikajengwa ndani ya Jimbo langu Tunguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi hiyo ipo tayari na hivi karibuni Mheshimiwa Spika ameniambia samani kwa ajili yake *containers* zameshafika na tumeomba kwamba, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aende akaifungue wakati wowote muafaka. Huo ndio Muungano. Lakini vile vile kulichaguliwa Kamati kule Unguja ya kushughulikia kero za Muungano, mimi kama Mwenyekiti nilichaguliwa na Ofisi ya Waziri Kiongozi. Lakini katika jambo ambalo limenifurahisha sana, nilikuwa Mwenyekiti alikuwemo Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, ambaye alikuwa Mbunge wa Magomeni, alikuwepo Mheshimiwa Hamza, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mheshimiwa Ali Suleiman. Tulihangaika mpaka kiwanja tukakipata, tukaonana na Mheshimiwa Basil Mramba, tukakubaliana baada ya muda si mrefu na jengo lile sasa litafunguliwa, huo ndio Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Mambo ya Muungano, ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, asimamie ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Tuliwapatia kiwanja, wataalamu wakaenda wakakagua wakakikubali, inashangaza baadaye hatimaye wamezungusha ukuta wakasema hapafai, sasa wataalamu hao hawafai, watafutwe wataalam wengine ambao hawataitia Serikali mahali pabaya kama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumza kuhusu habari ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Nakubaliana na nyimbo za kizazi kipya lakini tukienda moja kwa moja kizazi kipya tukasahau na nyimbo zetu za asili, tutapoteza utamaduni wetu. Wenzetu Bara zilikuwepo bendi, sasa hivi hata nyimbo zake huzipati zimetoweka kabisa. Kule Zanzibar kuna nyimbo vile vile za Bakari Abeid kama Mheshimiwa Seif angekuwepo mwenyewe angesikia hapa, “Mazoea yana tabu” na yeye anaipenda nyimbo hii. Nyimbo zile Mazoea yana tabu, tabia zikilingana. Sasa nyimbo hizi zikipotea kabisa, ina maana utamaduni wetu utakwisha. Kuna nyimbo “Mpenzi nipepee nina usingizi nataka kulala,” imeimbwa na Marehemu Seif Salum na nyimbo nyingine kadha

wa kadha za zamani. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri anayehusika, afanye kama zile taarabu za zamani, hazipo zitafutwe ziwekwe makusudi. Utamaduni wetu wa asili utakufa tu hatujui, hatuna nyimbo za Bi Kidude, hatuna nyimbo za Bakar Abeid na bendi za *OTTU Jazz* hatuna, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika Usalama wa Raia. Nawapongeza sana Usalama wa Raia. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lakini natoa tahadhari moja, matokeo mengi ambayo wenyewe wameyagundua wanakutana na baadhi ya askari wachache wamo, kwa nini? Uajiri mbovu, wakubwa wetu Makamanda wa Polisi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, wanawaweka watoto wao mle ndani, hakuna hayo. Wameshawashinda wala unga ndio wanawapeleka pale, matokeo yake juzi tumesikia askari wako kwenye malindo, wameparamia juu ya paa, wameingia ndani, wameiba sehemu kubwa ya unga ambao ulikuwa kidhibiti kwa ajili ya Mahakamani. Ni aibu, nataka utaratibu wa zamani udumishwe, wanyonge wale wakulima na wafanyakazi ndio waajiriwe kwa kazi hizo za Upolisi za nchi hii. Watoto wetu sisi wakubwa baadhi yao wanadeka, si waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano kulikuwa na nchi moja ilikuwa ina mfumo huo, waliajiriwa vijana 30 kwa ajili ya kazi za Udaktari wa Macho, wawili kati yao ndio walikuwa watoto wa Mawaziri. Wakasoma muda wa miaka miwili wakamaliza. Siku ya mwisho ya mtihani kila mmoja amewekwa katika chumba cha *theatre* ili awafanyie operesheni wagonjwa. Mmoja kati ya wale 30 akayaharibu macho yote mawili ya yule mgonjwa, akafeli kabisa kumbe alipogunduliwa ni mtoto wa Waziri fulani. Lakini wa pili akamharibu jicho moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja moja kwa moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono hoja. Napenda kuishukuru Serikali, kwa sababu ya jitihada kubwa sana waliyoifanya wakati wa ukame, wakalisha wananchi wote wenye njaa. Nawashukuru sana hasa katika jimbo langu la Longido. Jimbo la Longido lilikuwa ni jimbo ambalo limepata ukame mkubwa sana, mifugo imekufa, watu hawana chakula, lakini Serikali wamewalisha hawa watu mpaka mvua ikanyesha. Tena namshukuru ndugu yangu, Mheshimiwa Edward Lowassa, amefanya kama mlivyomshukuru wengi, alisaidia sana katika suala la elimu. Mkoa wetu, Wilaya yetu, ilikuwa na wanafunzi wengi sana walikosa nafasi ya kwenda Sekondari, lakini waliokosa aliwaita wawindaji walioko katika Wilaya ya Monduli, wakachanga shilingi 192 milioni, shule zikajengwa watoto 560 wakaenda Sekondari. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu ni nzuri sana. Sasa zimefuatana na hotuba za bajeti mbili nzuri; Hotuba ya Bajeti na ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, hii hotuba ya Waziri Mkuu ime-*support* bajeti. Jambo ambalo nilipenda sana katika hotuba ya Waziri Mkuu ni fedha zilizotolewa na Serikali, shilingi 500 milioni kwa kila mkoa kwa ajili ya watu wasio na uwezo, wenye biashara ndogo ndogo na hizo fedha

zitatumika kwa ajili ya vijana wetu kupata ajira, watajiajiri. Sasa ningependa kusema hivi fedha za mikopo zinazopatikana katika mabenki, fedha zinazopatikana katika Mfuko wa Pembejeo, hawa watu wa ngazi ya chini, hawajawahi kupata hizo fedha?

Sasa naomba hizi fedha zilenge kabisa kwa watu ambao hawana uwezo wa kuchukua fedha za mikopo benki ziende kila Wilaya. Kwa hiyo, ningependekeza kwamba, hizi fedha ziende kila Wilaya kwa sababu najua kwamba, mipango yetu wakati mwingine hatuipangi vizuri, zinaweza zikaelekea upande mmoja walengwa wakakosa. Kwa hiyo, naomba hilo lifanyike. Kwangu kuna *SACCOS* nyingi sana tumefungua za wafugaji, naomba hizi fedha zifike kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kasi ya Awamu ya Nne sijui kama itaendana na kasi za watendaji wote waliomo kwenye Halmashauri. Ni tofauti kabisa kwa sababu katika Halmashauri zetu, fedha zikitolewa na Serikali Kuu, zinakaa miezi sita kwenye akaunti. Hivi kweli kuna Halmashauri ambayo fedha zikifika kwenye akaunti inakosa miradi mpaka miezi sita, mpaka wakati mwingine mwaka wa fedha ukute hizo fedha hazijatumika zinarudi; je, inakubalika kitu kama hicho? Kwa hiyo, nasema kwa kweli Serikali iangalie Halmashauri zetu kwa sababu Halmashauri zetu ni wagonjwa, lakini ziko Serikalini. Fedha za semina, safari, posho, zipo kila siku lakini hakuna miradi inayofanyika. Ukienda kuna majengo yamekaa miaka minne hayajakamilika, lakini fedha ziko kwenye akaunti!

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nizungumzie kidogo suala la mifugo. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuunda Wizara ya Mifugo. Nadhani sasa mifugo imeanza kupatiwa mikakati, kwa sababu Waziri wa Mifugo hana Wizara nyingine ni mifugo tu. Kwa hiyo, hakuna tena cha maji, kilimo ni mifugo tu. Tena amewaweka Madaktari wawili. Nadhani sasa tuna pa kukimbilia, mtusubiri tu kwa sababu tutakuja kutafuta namna ya kufanya mifugo ifikiriwe katika nchi hii. Kwa sababu Serikali ilikuwa na agenda mbili tu kwa mifugo: Mifugo ipunguzwe na mifugo inaharibifu wa mazingira, ndio sauti ya Serikali. Sasa kwa kuwa Rais amelenga kabisa kuunda Wizara, tunaomba basi hii Wizara ihudumie mifugo. Kama mnataka tupunguze mifugo kwanza, mtutafutie masoko na mtutafutie masoko ya nje. Kama mnavyotafuta masoko ya korosho, kahawa, pamba na mazao mengine, mtafute na masoko ya mifugo. Kwa sababu hiyo itakuwa ni kishawishi tuanze kupunguza mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninapingana kabisa na suala la kusema kwamba, mifugo inaharibu mazingira. Sielewi na kama mnataka ushahidi, hebu twendeni katika jimbo langu, kwa sababu kuna mifugo lakini mazingira ni mazuri kuliko nchi nyingine. Nakubaliana na Serikali kwamba, mifugo inaharibu vyanzo vya maji na isiruhusiwe. Lakini kusema kwamba, inaharibu mazingira mengine, sio kweli, nenda Simanjiro. Wanaoharibu mazingira ni wakata mkaa na wakulima, lakini mnawaogopa wakulima mnawaonea wafugaji. Mfugaji hakati miti, isipokuwa tatizo ni Wasukuma, kwa Wasukuma wao wanakata miti. Mikono inawawasha wakiona miti wanakata, kwetu hatukati miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, naomba Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, wapewe semina.

Wafugaji wapewe semina sio kuwalaumu tu. Wafugaji nao wapewe fedha za pembejeo, wapewe mikopo kama wakulima hasa kipindi hiki kwa sababu wamepata hasara sana. Lakini ingekuwa ni wakulima ndio wamepata hasara, Serikali ingetetemeka, ingetafuta namna ya kuwasaidia. Sasa wafugaji nao wamepata hasara, wasaidieni. Suala la madawa Serikali imepunguza kodi ya madawa lakini naona wanaofaidi ni wafanyabiashara tu wa madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie matatizo ambayo tunapiga kelele kila wakati hapa kwamba, kuna upendeleo mbona sisi Kusini hatuna miradi, mbona huku hatuna. Suala la kipaumbele, Serikali iliangalie sana. Nitoe mfano mmoja tu mwaka 2005, Rais aligawa Wilaya baada ya kugawa Wilaya kuna Wilaya tatu zimeanza kujengwa, wangefuata kipaumbele nadhani Wilaya ya Longido ingejengwa, kwa sababu Wilaya ya Longido iko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya. Mtu akitoka Kamwanga kwenda Makao Makuu ya Wilaya au Hospitali ya Wilaya ni kilomita 252. Akitoka kule Natron ni kilomita 285, iko mbali sana na Wilaya. Lakini walipeleka fedha kwenye Wilaya ambayo sio sawa hata na Kata yangu moja kwa ukubwa.

Walimu wa kule kwangu wanakwenda siku mbili Wilayani. Madiwani siku mbili waende Halmashauri, lakini kwingine walikopelekewa fedha Mwalimu anakwenda kuchukua mshahara na kurudi kukuta kipindi chake. Madiwani ni hivyo hivyo. Hivi kweli kama kipaumbele kingekuwa kinaangaliwa, Longido isingepelekewa hizo shilingi milioni 600. Sasa kwa upendeleo huo, utaleta maisha bora kwa kila Mtanzania?

Kwa hali hiyo, ndiyo maana watu wanalalamika kwamba, huku kwangu, huko kwangu, wanaona tofauti kama hizo. Sasa kwa kuwa Wilaya yangu ni mojawapo ambayo jiografia yake ni ngumu sana, naiomba Serikali katika bajeti hii, waifikirie Wilaya ya Longido kama mnataka tuendelee na sisi tupewe fedha za ujenzi wa Wilaya hata ikiwezekana tuanze Halmashauri mapema. Naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabla ya kengele kugongwa, naomba fedha za MMES zipelekwe kwenye Bodi za Shule. Kwangu fedha zote ni Bodi ya Shule ndiyo inasimamia ujenzi, ndiyo inatumia hizo fedha na ndio wanapanga mipango yote. Mkipeleka Halmashauri hakuna chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine jamani nawaomba Wakuu wa Mikoa warudishiwe tena wawe karibu na hizi Halmashauri, kwa sababu sioni mtu anayesimamia hizi Halmashauri mpaka Wizara. Matatizo yatoke kwenye Halmashauri nani kwanza ataleta, hakuna mtu anayeleta mapungufu. Kwa hiyo, bado nasema kwamba, ni afadhali wakati ule Wakuu wa Mikoa walipokuwa wanaangalia hizi Halmashauri ni afadhali kuliko hivi sasa. Hivi vyeti eti kuna *Clean Certificates* nyingi zimenunuliwa. Tunasema zimeongezeka, zimeongezeka kwa sababu wana mbinu za kununua. Kwa hiyo, naomba tuangalie tena hizi Halmashauri zetu kwa sababu hali ni mbaya sana na tusipoangalia hatuendani kabisa na hii kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ningependa kuzungumzia barabara yangu ya Kamwanga lakini naona Mheshimiwa Mramba hayupo. Nilitaka kuzungumza …

**NAIBU SPIKA:** Serikali ipo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Nilitaka kuzungumza kama angekuwepo. Hiyo barabara ya kutoka Rombo mpaka Kamwanga, nyumba 30 za jimboni mwangu zimevunjwa. Sasa nasikia hiyo barabara imeishia hapo, waanze tena kule Sanya Juu. Sasa sijui, haiingii akilini, ikiachwa barabara kule waende kuanza Sanya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Napenda pia kutumia nafasi hii kumtambua Diwani Sabi Luwanzo wa Karagwe, mgeni wa Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia naomba nitoe masahihisho ya jina langu, mimi sio Fausta ni Felister.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahihisho hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Lakini kabla sijachangia hotuba, napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uchaguzi uliopita na kwa kura nyingi za kishindo alizozipata. Nampongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Nampongeza pia ndugu yangu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mwenezi, nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro na Mheshimiwa Rostam Aziz kwa nyadhifa walizozipata katika chama chetu. Naamini kabisa kwamba, tumepata viongozi wazuri, ambao itakapofika mwaka 2010, kwa kweli Wapinzani wanaweza wakapata cha mtema kuni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake ya Mawaziri wa Nchi, ambao wako katika Ofisi yake na Naibu Mawaziri na watendaji wote, ambao wako katika Ofisi yake, kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo imewasilishwa mbele yetu. Niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuona kwamba, katika miaka iliyopita, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, kazi zake hazikufanyika vizuri kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Lakini baada ya kusoma hotuba hii, bado nimeona kwamba, kuna ufinyu mkubwa tu wa bajeti kwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu. Mamlaka hii ilipoanzishwa, ilianzishwa ili kuuendeleza Mji wa Dodoma na Makao Makuu ya Serikali yahamie Dodoma, kama ilivyopangwa. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti wa mwaka hadi mwaka, Serikali haijaweza kuhamia Dodoma, kama ilivyotarajiwa na wananchi wa Dodoma tumebaki tunajiuliza kwamba ni lini ahadi hii ya Serikali itakapotimia?

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona kwenye bajeti ya Serikali kwamba, *CDA* wamepangiwa kupima viwanja kule kunakojengwa Chuo Kikuu, lakini mambo mengine ya kazi za kawaida fedha hazikutengwa kwa ajili hiyo. Naamini kabisa kwamba, fedha zisipotengwa kwa ajili ya uendelezaji na ustawishaji Makao Makuu, ujenzi wa holela utaendelea na matokeo yake Serikali itakapoamua kupanga Mji wa Dodoma, watu watavunjiwa nyumba, watapata hasara, lakini kwa sasa mambo hayo yanafanyika, watu

wanajenga holela, hakuna anayejali.  Naiomba Serikali iongeze fedha kwenye bajeti ya *CDA* ili wafanye kazi zao inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kuhusu fedha ambazo sikuona kama zimetengwa kwa ajili ya kujenga Ofisi za Serikali katika Mkoa wa Dodoma. Tunaamini kwamba, Dodoma ni muda mrefu kweli Serikali imepanga kwamba iwe Makao Makuu ya Chama na Serikali, lakini hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mkoa wa Dodoma.  Ninachokiona kilichoendelea katika mwaka wa fedha uliopita ni nyumba za kuishi ambazo ziko 300 pale Kisasa, lakini hakuna hata Ofisi moja ambayo imejengwa kwa ajili ya Ofisi za Serikali na kuiwezesha Serikali kuhamia Mkoani Dodoma.  Sisi ambao ni viongozi wa wananchi, tunashindwa la kusema kwa wananchi wetu, kwa sababu ni ahadi ya muda mrefu, lakini haitekelezeki. Naiomba Serikali kama kuna uwezekano, Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambayo ni makini na inafanya kazi kwa *speed* inayokubalika, sasa watenge kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mkoa wa Dodoma. Wakijenga Wizara moja moja, kila mwaka wa fedha, naamini itakapofika mwaka 2010, tutakuwa na Wizara tano ambazo zitakuwa zimekamilika na Serikali itapata Ofisi za kufanyia kazi katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, utendaji katika Halmashauri zetu sio mzuri.  Nikubaliane nao kwamba, ni Halmashauri chache sana ambazo zina *Clean Certificate*.  Lakini pia nikubaliane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kuna upungufu mkubwa sana kwa watumishi wa Halmashauri wenye sifa zinazotakiwa.

Lakini sasa tutawasaidiaje hawa Watumishi wa Halmashauri kwa sababu tusilalamike tu kwamba, ripoti zao ni chafu, hawafanyi kazi zinazotakiwa, wanaiba, ni wabadhirifu, sasa tufanyeje?

Naiomba Serikali iwasaidie wafanyakazi wa Halmashauri, tunaelewa kabisa kwamba, wafanyakazi wa Halmshauri wanamishahara midogo, tunelewa kwamba, Halmashauri zetu hazina pesa za kuwasomesha watumishi wao na tunajua kabisa kwamba, Halmashauri hazina uwezo wa kuwapa motisha wafanyakazi ambao wako katika Halmshauri zetu. (*Makofi*)

Sasa naiomba Serikali Kuu, kama inavyowajali watumishi wake, tunaposema Serikali, ni Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa, lakini tunajua fika kwamba, Serikali za Mitaa hazina pesa za kutosha. Naiomba Serikali Kuu, isaidie Halmashauri zetu katika kuwasomesha wafanyakazi ambao wako katika Halmashauri. Naamini kwamba, wafanyakazi wa Halmashauri, kama yupo aliyemaliza shule mwaka 1973, yuko hivyo hivyo, kama hakupenda kujiendeleza mwenyewe.

Kama yupo aliyemaliza shule mwaka 1980, kama hakutaka kujiendeleza mwenyewe kwa pesa zake, yuko hivyo hivyo na ndiyo maana utendaji wao hauridhishi. Naiomba Serikali kwa sababu wote hawa ni watoto wake, wafanyakazi wa Halmashauri

ni watoto wake, wafanyakazi wa Serikali za Mitaa ni watoto, iwafikirie sana hawa watumishi ambao wanafanya kazi katika Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Wafanyakazi hawa pia hawana motisha, Serikali ilipoamua kuwakopesha watumishi wa Serikali Kuu magari na nyumba, watumishi wa Halmshauri hawakuhusishwa. Sasa tunategemea nini, tunategemea ufanisi wakati hawana motisha yoyote. Tunaamini kabisa na tunajua kabisa kwamba, Halmashauri zetu hazina uwezo wa kujenga nyumba na kuwakopesha wafanyakazi wake. Tunaamini katika Halmashauri zetu, gari lililo zuri pale ni la Mkurugenzi tu, kwa hiyo, Halmashauri haiwezi ikawakopesha watumishi wake magari. Sasa naiomba Serikali iwape motisha hawa wafanyakazi wa Halmashauri.

Jambo lingine ni kwamba, katika Halmashauri zetu, maeneo mengi Watendaji Wakuu wa Halmashauri zetu wanakaimu. Nitoe mfano mzuri katika Mkoa wetu wa Dodoma tunazo Halmashauri tano, lakini katika Halmashauri zote hizo tano, Halmashauri moja tu ambayo haikukaimishwa, ni Halmashauri ya Dodoma Vijijini tu. Lakini Halmashauri nne zilizobaki, Watendaji Wakuu wanakaimu, sasa kama wanakaimu ufanisi tutaupataje, ufanisi tutaupata kutoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika ninaiomba Serikali, kama wale wanaokaimu katika nafasi wanastahili, wapewe nafasi hizo ili wawajibike kwa wananchi inavyotakiwa. Lakini kama hawastahili, basi Serikali iwaajiri watumishi wanaofaa kufanya kazi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo kwa wanawake limechangiwa na wengi lakini na mimi pia sitaacha kulichangia. Naishukuru Serikali, kwa kuamua kutenga shilingi milioni 500 kwa akina mama na vijana ili wakopeshwe. Lakini utaratibu ukoje? Mimi Mkoa wangu ni Mkoa wenye ukame sana na wanawake wengi hawana uwezo wa kuwa na dhamana katika mabenki na ninavyoelewa, huwezi kukopa Benki bila kuwa na dhamana. Sasa kwa kuwa lengo ni kumwezesha kila Mtanzania awe na maisha bora, tusipoangalia atakopa Felister Bura, atakopa na mwingine mwenye uwezo wa kujidhamini. Lakini yule mwananchi wangu ambaye ana nyumba ya msonge na ana ng’ombe, atadhamini kitu gani?

Naiomba Serikali basi ikaangalie utaratibu mzima wa kuwakopesha hawa wanawake na vijana. Ninawapigia debe sana wanawake kwa sababu ni waaminifu katika urudishaji mikopo, ni waaminifu katika kutekeleza maagizo ya Serikali na hata maagizo ya benki. Pengine niiombe Serikali, ifanye haraka sasa kurasilimisha ardhi ili wananchi wapate dhamana ya kukopa katika mabenki yetu. Tusipoangalia tutakopa sisi wa mijini, lakini wa vijijini hawataweza kukopa na hatutakwenda nao katika mbio hizi tunazokwenda. Kwa sababu kama 2006, mwananchi hawezi kukopa na tukakopa watu wa mjini, ina maana 2010, tutamkuta anapiga *mark time* pale pale, hajasogea na hata maisha bora kwa kila Mtanzania hatajua maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie sasa kuhusu ghala la Serikali *(SGR)*. Ni muda mrefu sasa viongozi tunaambiwa kwamba, tuwahamasishe wananchi hasa

wanaoishi katika Mikoa ya ukame, kulima mazao yanayostahimili ukame, lakini mazao hayo hayanunuliwi na *SGR.* Tunawaomba wananchi walime mihogo, mtama, uwele, lakini unapofika wakati wa ununuzi wa mazao ya chakula ni mahindi tu ndiyo yananunuliwa. Sasa wananchi wanatuuliza mnatuhamasisha kulima uwele, mtama na mihogo, lakini inapofika wakati wa soko hatuna soko. Sasa niiombe *SGR*, wasifanye ubaguzi katika kununua mazao, la sivyo wawatafutie wakulima wa maeneo ya ukame, soko la mazao wanayolima. Nakumbuka mwaka huu mwanzoni, Serikali ilipokuwa inatafuta jinsi ya kuwalisha watu njaa ilipoingia, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika alisema kwamba, Wilayani kwake kuna mihogo mingi, sasa sidhani kama Serikali ilinunua mihogo hiyo na kugawa kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi naomba nikushuruku sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo, ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa chama chetu. Pamoja na wenzetu ambao wameteuliwa katika nafasi mbalimbali ndani ya Chama cha Mapinduzi, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitatofautiana na wenzangu, kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nzuri sana na hata yule ambaye alikuwa na jambo muhimu la kuzungumzia kwenye hotuba hii, nafikiri tumeshindwa cha kuzungumza zaidi ya kupongeza. Tunachoomba ni yale yote ambayo yameandikwa ndani ya hotuba hii, yaweze kutekelezwa kwa wakati muafaka ndani ya mwaka mmoja. Lakini nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake yote ya Wizara yake, kwa kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais, wakati wa njaa ya kwamba, hakuna Mtanzania ambaye atakufa kwa njaa. kwa kweli wote tumeshuhudia. Nakumbuka Jimboni kwangu watu walipiga simu ofisini kwake. Mkuu wa Mkoa wangu saa sita za usiku alihangaika kuongea na ofisi za Wilayani kuhakikishga kwa nini watu hawajapata chakula na asubuhi wote tulihangaika Wilaya nzima. Naomba nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi*)

Lakini nimpongeze vilevile Mheshimiwa Rais, kwa kumteua Mheshimiwa John Mwakipesile, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya. Sisi tunashukuru kwamba, Mheshimiwa John Mwakipesile alikuwa Mbunge na anatoka Mbeya na anajua machungu ya Mbeya anafanya kazi kwa bidii sana, tunashukuru kwa hilo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu mazingira, lakini niipongeze Serikali kwa uamuzi wa kusikiliza malalamiko ya viongozi wa Wilaya ya Mbarali. Kwa muda mrefu, mimi Mbunge kama mwakilishi wao, mwenye nafasi yakuzungumza ndani ya Bunge, nimekuwa nikiomba msaada wa Serikali Kuu kwamba, watusaidie kutafuta maeneo ya kuwaondoa wafugaji kwenye chanzo cha maji ili waweze kupata sehemu za kudumu, ambazo hazitaathiri maji na hatimaye sasa Serikali imeitikia. Naomba niipongeze na kuishukuru sana. Lakini nimesikia kauli za Waheshimiwa Wabunge wakisikitika kwa nini wafugaji wanaonewa na wengi Kamati ya Mazingira ni

shahidi yangu, wametembelea Jimboni kwangu, wamekaa kwa siku tano, wameona jinsi ile sehemu ilivyokuwa imeharibiwa. Sehemu ambayo ilikuwa ni kivutio, iliyokuwa na chanzo cha maji na maji yanapita chini kupitia *under ground streams*.

Sasa mifugo imekandamiza kiasi kwamba, maji hayawezi tena kupenya na kwenda kwenye Mto Ruaha na sehemu imebaki kuwa jangwa. Sasa nilifikiri kazi muhimu kwa Serikali ni kuwatafutia *route* hawa wafugaji, wapate kupita kwenda mahali ambapo wanaweza wakajihifadhi. Kwa sababu wako pale, hawaelewi waende wapi na nyie mlisikia hapa Mheshimiwa Raynald Mrope anasema, hatutaki ng'ombe wanaotoka Usangu, wana magonjwa wasije kwetu.

Lakini wale ng'ombe sio kwamba, wana ugonjwa, wamezidi kiwango cha eneo ambapo wangeweza kuhifadhiwa na ukiwaambia uwachimbie malambo Mbalali, si rahisi kwa sababu wanahitaji malisho na Wilaya Mbarali ni kame. Ile sehemu kwa sababu ya ule uchepechepe, wakati wa kiangazi wamekuwa wakikimbilia kule kwa ajili ya kupata malisho na maji. Nafikiri ni kazi ya sisi sote wafugaji, sio kwamba wamezaliwa pale Mbarali, nafikiri wametokea Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma na Arusha. Kama wote ni Waheshimiwa Wabunge na wote wale ni watu wetu, nafikiri tungekaa kwa pamoja, tukatafuta muafaka jinsi ya kuwasaidia.

Tujue tunafanya nini kuondoa hilo tatizo. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, sisi hatuwafukuzi, tumekaa na Wamasai kuanzia mwaka 1975, lakini wale watu ni marafiki sana wa misitu, hawakati miti, wanalisha ndani ya msitu na hakuna aliyelalamika na hakuna chanzo cha maji kilichoharibiwa. Tunatofautiana mila, wenzetu wengine wanapokuja la msingi ni kukata miti, waone mifugo yaoe kwa upana zaidi, sasa hicho ndicho kilichoharibu mazingira. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuungane kwa hilo, lakini lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu maeneo ya utawala katika Mikoa mbalimbali. Mkoa wa Mbeya ni mkubwa sana, Wilaya zimegawanywa kwa maeneo makubwa, kwa mfano, Jimbo langu lina ukubwa wa kilomita za mraba elfu 16.5. Lakini lina Tarafa mbili tu na kata 11. Hilo Jimbo ukianza kulizunguka unatumia miezi mitatu bila kuugua mpaka ulimalize Jimbo zima. Lakini unaposikia Majimbo mengine yanagawanywa, Mbeya haijagawanywa Kitarafa kwa muda mrefu na taratibu zote tumeshazifanya kwenye Halmashauri mpaka *RCC* na maombi yapo TAMISEMI, hatujapata bado mafanikio. Lakini tumeleta Mbozi, ukienda Rungwe Magharibi, ukaja Mbarali ni Majimbo yanayohitaji kugawanywa, ili yaweze kutawalika kwa urahisi, kusudi matatizo ya wananchi yaweze kutatuliwa kiurahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza kwa TAMISEMI, iwe ni wakati muafaka wa kuainisha maeneo yote makubwa, kuona watayagawanya vipi. Mapendekezo yao basi, wayalete tuweze kuyapitia na sisi Wabunge, tuweze kusaidia mgawanyo wa maeneo uwe sawa kwa Tanzania nzima na Mbunge uwe na uwezo wa kutembea kwenye eneo lako kama Wabunge wengine, ili wote tuwe sawa na wananchi waweze kuhudumiwa kiusawa. Kwa hiyo, naomba kupendekeza hilo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependa kusemea mishahara ya Maafisa Watendaji, pamoja na Madiwani. Wenzangu wamelizungumza sana, kila mtu analiunga mkono ndani ya Bunge hili kwamba, maslahi yao yatekelezwe na mimi nipo karibu na Mwenyekiti wa Tume ambayo iliteuliwa. Naamini mapendekezo ambayo yatakuja, yataweza kuleta unafuu kwa Madiwani. Sasa Maafisa Watendaji ni mwaka wa tatu tangu wameajiriwa, hawajapata mishahara, ni asilimia 50 tu ndiyo wamepata mshahara. Kule kwangu nina Madiwani 87 na Maafisa Watendeji wa vijiji 87, wanaopata mishahara ni nusu yake, wanaishi kwa kubabaisha, Halmashauri haina kipato tena kilichokuwa kinategemewa, ni ushuru wa mifugo ambao kwa sasa hakuna ushuru, wanategemea ruzuku ya Serikali. Lakini ukiangalia kwenye jedwali ambalo Waziri Mkuu amelitoa, wanasema hatujafikisha taratibu zote za ajira. Sisi tumewasilisha zote, tunaomba basi Waziri muhusika, apitie tena Maafisa Watendaji kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, wapate mishahara yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwa upande wa ofisi za Wakuu wa Wilaya, wanaishi kwa kubabaisha sana, hawana mishahara. Nakumbuka Bajeti ya mwisho, nilipendekeza kwamba, kwa nini ma-*DAS* nao wasiwe ni *vote holder* kama walivyo ma-RAS, ili ofisi za Wakuu wa Wilaya ziweze kuendeshwa kwa ufanisi zaidi, kuliko kuomba kila wakati kwa ma-*RAS*. Kwa hiyo, ningeomba nalo nilipendekeze.

Wenzangu wamezungumza sana kuhusu kupeleka pesa nyingi kwenye Halmashauri. Mimi hili naliunga mkono sana kwamba, pesa ziende kwenye Halmashauri ila usimamizi ndiyo udhibitiwe. Kwa kweli ukishiriki tangu kwenye Kamati ya Fedha kama Mbunge, matumizi yanaenda vizuri. Lakini wanaposema Hati Chafu kama ni kigezo, siungani nao, kwa sababu kuwa na Hati Chafu haina maana kwamba, wizi umetokea, maana yake ni utaratibu wa utunzaji nyaraka za hesabu. Mahesabu hayakutengenezwa ipasavyo, ndiyo yanayosababisha hati iwe chafu. Kwa hiyo, kisiwe kigezo cha kuwanyima Halmashauri isipate pesa kwa kuwa na Hati Chafu na kwa sababu mwelekeo unaonyesha tutapata waweka hazina wapya, ambao tayari wana-*qualification* zinazostahili, naamini kigezo cha Hati Chafu hakitakuwepo tena, nitapata Hati Safi.

Sasa naomba nizungumzie kilio cha Wanambarali mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusu mashamba yale ambayo nimekuwa kila wakati nikisema ni sawasawa na jinsi nilivyokuwa nasema wakati huo kuhusu mazingira ya Mbarali. Mashamba ya *NAFCO* Mbarali yako mawili, ambayo ndiyo chanzo pekee cha kipato cha wananchi. Mashamba haya yanahudumia zaidi ya watu 30,000, vijiji kumi kwenye kila shamba na si wananchi wanaotoka Mbarali tu, hata wanaotoka Wilaya za Iringa na Wilaya nyingine za Mkoa wa Mbeya, wanalima ndani ya mashamba haya. Lakini nilitaka kupendekeza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua yale mashamba yalipendekezwa kuuzwa, *tender* ilitangazwa na wapo walioshinda, ambao wanasubiri uamuzi wa Serikali baada ya *PSRC* kufanya kazi yake ili waweze kukabidhiwa haya mashamba.

Lakini sasa tuko kwenye tatizo la utunzaji wa mazingira, haya mashamba tutakapompa mtu mmoja au watu wawili na maji yanayotumika kwenye kilimo ni yale tu yanayoingia kwenye yale mashamba, kwa maana kwamba sasa wakulima wote wanaolima nje ya yale mashamba, hawatakuwa na nafasi ya kulima tena. Lakini nilifikiri

Serikali ingeangalia kwa undani, kwa sababu tuko kwenye mpango wa kutunza mazingira, wale wakulima wadogo wadogo wote sasa waondolewe kule pembeni kwenye mashamba yale madogo madogo wagawiwe sehemu ndogo ndogo mle ndani mwa yale mashamba ambayo yameshaendelezwa. Wagawiwe hekta moja moja ili waweze kulima mle ndani na waweze kupata kipato cha uhakika, kusudi kule nje kwenye vyanzo vya maji visiingiliwe tena.

Kwa hiyo, nimwombe Waziri Mkuu kwamba, wakae tena waangalie kwa sababu hakuna kipato kingine Wilayani Mbarali. Ukizungumza kwamba, kuna chakula safari hii Mbeya, Mbarali uitoe kwa sababu haina mvua, inategemea kilimo cha umwagiliaji na tangu mwaka 1992 baada ya *NAFCO* kushindwa kulima. Wakulima wamekuwa wakikodi mle ndani ya mashamba, kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Wamekuwa wakitegema kipato chao kwa kutumia mpunga ambao ndiyo zao lao pekee la biashara. Sasa leo unawaambia hampati tena anapewa mtu mmoja. Sasa sijajua hesabu yake; je, huyu mtu mmoja atakeyepata hawa wananchi wanaolima ndani watapata wapi chakula**,** watapata wapi pesa za matumizi ya kawaida? Kwa sababu walikuwa wanategemea kile kitu cha ndani; je, atagawa chakula, atawapa kazi ya kuweza kufanya waweze kupata kipato chao?

Kwa sababu *NAFCO* ilipokuwepo hata wananchi wenyewe walikuwa wanaajiliwa mle ndani, hawakuweza kumudu maisha yao ya kila siku. Lakini baada ya kuambiwa sasa mtakodi yale mashamba na wamekuwa wakilipa shilingi 25,000 kwa hekta moja, vipato vimeongezeka. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifika miaka ya 1980, uliona sasa ni tofauti kabisa. Hali ya Mbarali watu walivyoendelea, walivyobadilika, mashule tumejenga kwa kutumia kipato cha kilimo cha mpunga si kitu kingine na kwa mfano tu ulio rahisi, katika hekta moja ya shamba, mkulima akilima pale anapata magunia 40 na akiuza anapata karibu shilingi milioni 1.8, ukitoa gharama inabaki shilingi 1,200,000 kwa hekta moja. Sasa kwa mwaka mzima kwa hekta hizo 7,000 ambazo ziko kwenye shamba moja, kuna shilingi bilioni nane ambazo zinazalishwa pale kwenye ile Wilaya na hizo pesa zinabaki ndani wa Wilaya ya Mbarali. Sasa leo akipewa mtu mmoja, sielewi unamfanyaje huyu mwananchi aweze kumudu maisha yake ya kila siku, unampa wapi eneo lingine la kulima akitoka mle ndani ya mashamba?

Lakini nimesikia Wabunge hapa wakiomba mabonde yao ya mashamba yakalimwe mpunga. Kwa nini hawa watu ambao wana uwezo, wasipewe haya mabonde ambayo yanahitaji wakulima, yanahitaji wawekezaji, halafu hii sehemu ambayo imeendelezwa basi waachiwe hawa wakulima wadogo wadogo waweze kulima na kumudu maisha yao? Lakini cha kusikitisha mle ndani mwa yale mashamba, kuna kituo cha polisi, kuna shule ambazo zimejengwa kwa MMEM, kuna zahanati ambazo zimesajiliwa mwaka 2005 tu. Maana yake sasa ukimwuzia hilo shamba, unamwuzia na vitu vilivyomo humo ndani. Je hawa wanafunzi utawapeleka wapi, hii zahanati huyu mtu aliyenunua ataruhusu kweli watu waingie humu ndani, sio rahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba hicho, Wanambarali wako huko wanasikiliza, wanangoja kauli yako ya mwisho, ujue utawasaidiaje waendelee kulima mle ndani ya shamba.

Baada ya kusema hayo, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu atahitaji maelezo zaidi, mimi niko tayari, lakini mipango yote ambayo imetekelezwa kwa mfano, stakabadhi za maghala, tumepewa mkopo wa shilingi bilioni moja pale kwenye Shamba la Chimala. Wameweza kupata mkopo wamelima na wamelipa na kuna taasisi mbalimbali ambazo zimesaidia sana na wako tayari kutuunga mkono. Lakini wengi mlikuwa mkiona kwenye vyombo vya habari kwenye *TV*, kwenye magazeti, niseme kwa hili, navishukuru sana vyombo vya habari, vimewasadia wananchi wa Mbarali katika kufikisha kilio chao kwa Serikali. Naamini mlisoma magazeti, mmeona *TV* na mmesikiliza kwamba, kwa kweli wanahitaji haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja asante sana. (*Makofi*)

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, niungane na wenzangu, kumshukuru Mungu, kwa kunipa nafasi hii. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi sasa. Pia niwapongeze Wabunge wenzangu ambao wamepata nyadhifa mbalimbali katika chama chetu cha Mapinduzi. Nimponge Waziri Mkuu na watendaji wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ambazo ziko chini ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii, ambayo ilisomwa jana. Inahitaji uwe mtu wa pekee na wa namna ya pekee, kusema vinginevyo juu ya hotuba hii, kwa kweli ni nzuri. *(Makofi*)

Lakini nimesimama kwa sababu nimeiweka hii hotuba kuipunguza na kuipeleka Mbinga katika Jimbo la Mbinga Mashariki na kuona inakidhi namna gani kwa wanachi wa kule. Lakini kabla sijaelezea, naomba nitoe taarifa tu kwamba, wakati tumeanza Bunge, wenzagu wengine walikuwa wananipa pole kwa sababu waliniona katika vyombo vya habari, nikielezea kuhusu kuungua kwa makaa ya mawe katika Kijiji cha Mtundwalo, Kata ya Luanda, Tarafa ya Namswea, Wilaya ya Mbinga. Serikali imechukua hatua mbalimbali, lakini mpaka sasa tumekwama, moto unaendelea kuwaka na habari nilizokuwanazo mpaka jana, Wizara ya Nishati na Madini, inajaribu kuomba shilingi milioni 50, hazijapatikana kwa kiasi cha wiki tatu sasa. Sijajua madhara ya ule moto yatakuwa ni nini. Lakini ni dhahiri unaelekea eneo ambalo wananchi wanakaa na mto huu unawaka kwa chini chini, kwa hiyo, huwezi kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwenda kule Mkoa wa Manyara juzi hapa, akawapa pole juu ya ajali ya basi, nina hakika vyombo vya Serikali vilikuwa vinaona, kama ni *traffic* walikuwa wameona, lakini mpaka tukio limetokea ndiyo watu tunaanza kulia! Mbunge nilikwenda katika eneo hili la makaa ya mawe ambayo yanaungua, *DC* amekwenda, Mkuu wa Mkoa amekwenda na namshukuru sasa Mheshimiwa Mahanga, wakati akiwa kwenye ziara yake kule tulimwomba alifika. Tumeona tunasubiri nini kuchukua hatua za kuhakikisha moto unazimwa, tunayo mipango ya kwenda na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, naye namshukuru sana kwa hatua ambazo amezichukua. Lakini nilimwambia wote tumekwenda tumeona sasa inafaa tunapokwenda waende wataalam ili wauzime. Maana wale wananchi wanachoka, magari yanapita tu kila siku kuona, ile sio *museum*. Ombi la fedha la Wizara ya Nishati

limekwama Hazina, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia kwako kwa kasi ile ile, kwa sababu unapata ari kwa kuona matatizo bila matatizo ari mpya haipo. Ninaomba sana kupitia kwako Waziri Mkuu, atusaidie ili wataalam hawa maana wako *stand-by* lakini hawana nyenzo ya pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Serikali kwa Wizara zifuatazo: Makamu wa Rais, hasa Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, yeye ameshapeleka wataalam kwenda kufanya *environmental impact assesiment,* tunamshukuru sana. Naishukuru Wizara ya Maji, ambao wamekwenda Mbinga wamepeleka wataalam kuangalia matatizo ya maji na nawashukuru watendaji mbalimbali na Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Monica Mbega. Mkuu wa Mkoa mpya kabisa, ana mvuto kule wa kipekee na anaoneka kutusaidia sana katika Mkoa wetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sizungumzii kuhusu barabara za Mkoa wa Ruvuma au Wilaya ya Mbinga au Jimbo langu, pomaja na ubaya wake kwa sababu moja kubwa. Ni juzi tu Mheshimiwa Rais, alihakikisha kwamba, barabara ya Songea mpaka *Mbamba Bay* itawekewa lami. Sasa sina sababu ya kuendelea kuzungumzia suala hili, maana naona liko kwenye mpango. Lakini sipendi pia kuzungumzia suala la umeme, kwa sababu Wizara hii ina ushirikiano mkubwa sana, Mheshimiwa Msabaha na Meshimiwa Dr. Lawrence Masha, wametusaidia sana na mazungumzo yetu yanazaa matunda. Lakini pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mheshimiwa Rais, kwa kutuhakikishia kwamba, jambo hili liko katika mikono salama.

Niombe tu kwamba, kwa sababu nilikuwa nasikia Wabunge wenzangu wanapoongea, hawaongelei umeme wa Makao Mkuu ya Wilaya wala ya Kata, wanaongelea vijiji na vitongoji. Sasa kwa sababu nimechelewa hata Makao yangu Makuu ya Wilaya hayana na kwa sababu tumeahidiwa kwamba tutakuwa na umeme wa *grid* katika muda wa miaka michache ijayo, basi katika ile *planning* wafikirie katika zile Kata kama za Matili, Luanda, Maguu, Litembo, kwenye hospitali kubwa sana, Linda, Ngima, Kilimani, ziwe katika *planning* ili wanapomaliza wawe wamemaliza haya matatizo. Lakini pia naishukuru Wizara hii, inaandaa mpango wa karibu wa kuipatia umeme Makuu ya Wilaya ya Mbinga.

Naomba nimshukuru pia Waziri Mkuu, alipoitisha Mkutano wa wadau mbalimbali wa mazao ya kilimo. Nilipata bahati ya kuhudhuria kwenye zao la kahawa, tumbaku na korosho. Lakini hapa naomba nizungumzie zao la kahawa, kwa sababu ilikuwa *point* muhimu ya kupewa Ubunge pia. Kwa wale ambao hawatufahamu, eneo ninalotoka sio wakulima sana wa kahawa. Sasa wapinzani walijenga hoja ya kusema kwamba, kama mtampa huyu Ubunge, hajui kahawa, hamwoni kama zao la kahawa litakufa. Ilikuwa ni hoja nzito, lakini namshukuru Mungu, alinipa hekima na kuwajibu na wananchi wengi wa Mbinga ni wakatoliki. Sasa nikawa nawauliza, je, katika ndoa zenu mnapogombana, mnapeleka wapi matatizo?

Wakasema wanapeleka kwa padri, nikauliza padri ameoa? Wakasema hapana, nikasema lakini anatatua matatizo yenu, wakesema safi. Basi mchagueni huyu huyu ambaye halimi kahawa, atatatua matatizo ya kahawa. Sasa, kahawa pamoja na matatizo

ya soko, nashukuru pia katika bajeti ya Mheshimiwa Zakia Meghji, anaondoa ruzuku ya ku-*process* kahawa. Hiyo ni hatua nzuri, inahamasisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeomba pengine kupitia Wizara ya Kilimo, wajaribu kuangalia tena zile Sheria nafikiri za mwaka 2001 za Kahawa *(Coffee Act)*, ambayo inazuia *Multiple Licence*. Unatakiwa uwe na *Licence* moja tu kwa *activity* moja. Kwa hiyo, wakubwa wengine wanachofanya, wanafungua makampuni mengi, lakini mtu yule yule mmoja. Tukifanya hivyo, maana yake mkulima ukiwa na kahawa yako huruhusiwi kwa Sheria hii kui-*process* mpaka ukainunue tena Moshi kwenye mnada. Kwa hiyo, hiki ni kitu ambacho ni *disincentive*. Kwa hiyo, ningeomba pia pamoja na marekebisho ambayo yametolewa na bajeti, suala hili pia liweze kuangaliwa ili ile azma ambayo ipo katika ile bajeti ya Serikali, iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hilo tu, *Coffee Act*, inataka wakulima wale wawe *registered* ili waweze kutambulika. Miaka ile ya 1980 na 1990, watu wengine walipata pembejeo, walikuwa ni watu tu wa sokoni, hawana hata kahawa. Lakini walipata ile faida ya kupata zile pembejeo na Serikali, kwa sababu haifahamiki hii kahawa ni ya nani. Mwaka huu, tunamshukuru Mungu, kahawa imezaa sana. Kwa hiyo na wizi wa kahawa utakuwa mwingi. Kinachofanyika, watu wanachuma kahawa mapema sana, wanaiweka chumbani, wanalala nayo ili kuweza kulinda. Hii inapunguza ubora wa kahawa. Lakini kama watakuwa *registered*, tutapunguza wale wafanyabiashara wengine, ambao hawahusiki na kahawa. Hii ina faida nyingine, kwa sababu watakuwa wanafahamika na kule Mbinga tunayo Benki ya Wananchi, maana yake ni rahisi mkulima huyu kukopeshwa na Benki ya Wananchi wa Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee suala la ruzuku. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasema, ruzuku lazima ifikishwe walipo wakulima. Ni matarajio yangu basi katika kipindi hiki cha mwaka tunachotarajia kukianza mwezi Julai, hii ruzuku ya mbolea itafikishwa wakulima walipo, siyo Mkoani. Naomba niunge tu yale maneno yaliyosemwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 49 na 50, kuhusu madini. Nayaafiki na tunangojea kwa hamu utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeiomba Serikali, imeshughulikia sana suala la njaa, lakini njaa ni *storm* siyo *cause*, *cause* ni kilimo chetu. Sasa, naomba tu kama iliwezekana kuondoa pengine kodi kwa wale wanaoagiza mahindi, hii mbolea bado ni ghali sana. Kama tunaweza tukaondoa kodi ili hawa wakulima *by that specialization*, tukawapa wakalima zaidi, tutapunguza *bill* ya Serikali ya kuagiza chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee mishahara, inaelekea itapanda. Lakini, baada ya ile Tume ya Mheshimiwa Rais nafikiri itapanda zaidi. Sasa, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aangalie namna tutakavyoweza kufikisha hii mishahara kwa hawa wafanyakazi. Benki zetu zinaishia Wilayani na Wilaya nyingine hazina Benki kabisa kama Mkuranga. Sasa watu hawa wanasafiri mwendo mrefu. Kule kwangu mtu anatoka kilomita 80, kilomita 100, usafiri wa shida, anapanda gari wanajazana kule. Gari lenyewe inachukua watu 20, kwenda kufuata mshahara, alale na hana uhakika kama mshahara umefika. Tuangalie utaratibu wa kuhakikisha mwananchi mfanyakazi anapata

mshahara mahali alipo, diyo *contract*. Mimi nafikiri Wanasheria hawajagundua, wangeweza kuwashawishi wananchi, Serikali ingeshtakiwa ili iweze kuwalipa fidia kwa hizi hela ambazo zinapotea shilingi 30,000 au shilingi 40,000. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kuwa, sisi kule Mbinga tunayo Benki ya wananchi na nimeongea na Mwenyekiti wa Benki ya Wananchi, anasema inawezekana Benki ya Wananchi ikiwezeshwa na Serikali kwa kiasi fulani, ikafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waziri Mkuu, tufanye *model* basi. Hata kama tutaanza na Kata moja kule Mbinga au Tarafa moja, tuanze ili hao wafanyakazi wapate mishahara mahali walipo.

La mwisho, kila mtu amekuwa akimshukuru Mungu hapa na Mheshimiwa Mohamed Missanga alipoanza, kila mtu alifurahi. Mimi naomba, niliombe Bunge na Serikali ikubali, tuwe na *National Prayer Day*. Viongozi wetu wa Serikali watuongoze katika kumshukuru Mungu na kumwomba Mungu na pengine kumwomba Mungu msamaha. *(Makofi)*

Sera zetu za Serikali zina nia nzuri, lakini wakati mwingine tunawaumiza wananchi. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameshughulikia vizuri suala la chakula kwa watu wenye njaa. Lakini, inawezekana pia kuna mtu mwingine katika *process* hiyo, hakupata chakula hicho, analaumu na anasema Mungu kwa nini mimi sikupata. Hapa tulitaifisha Shule ya Misheni ya ndugu zetu Waislam na madhehebu mbalimbali mali ya Mungu. Ni vizuri tukaomba msamaha huo kwa Mungu. Kuna wenzetu tumewakosea, Wazee wa *East African Community* mpaka leo kwenye magazeti ukisoma, wengine hawajalipwa, wanalalamika. Tukiwa na mipango mizuri hii ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ametuletea, tukiwa na bajeti nzuri hii ambayo Mheshimiwa Zakia Meghji ametuletea, tukiwa na hotuba nzuri hii ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuletea, tunahitaji turekebishe twende pamoja na Mungu ili tuweze kufanikiwa vizuri zaidi. Nina hakika tukifanya hivi, maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. Amerika pamoja na jeuri yake yote, katika noti ameandika *In God We Trust*. Mwisho, ningekumbusha tu suala hili la Vijiji, Kata na Tarafa. Jimbo la Mbinga Mashariki, lina Kata 24, ni kubwa mno. Ningeomba tuangaliwe ili ziweze kugawanywa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nieleze utaratibu ambao unafuatwa. Katika Kanuni zetu, kuna kitu kinaitwa Daftari la Maamuzi. Kwa hiyo, mambo anaposema Spika, kuna Daftari la Maamuzi, kila anayeongea hapa anaingia humo. Kwa hiyo, kama tulivyoongea siku za nyuma kwamba, wale waliozungumza kwenye hotuba ya bajeti ya Mipango na Uchumi, watakuwa wa mwisho sana kupata nafasi kama wale wengine ambao wameomba kujadili katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa sababu tumepata barua zinatuomba na kusema fanya unaloweza na ujanja wowote ule ili nipate, haiwezekani. Unajua, tukitaka kuendesha Bunge letu kwa amani na utulivu, lazima tutende haki kutoka meza hii. Kwa hiyo, itakuwa ni *embarrassment* kwa Kiti kama nitamchukua mtu aliyezungumza mara moja kwenye bajeti, nikaacha wengine

ambao hawajapata nafasi. Kwa hiyo, naomba barua za namna hiyo msituandikie. Tunaomba ufanye unalotaka, hata ikiwezekana, haiwezekani! Naomba hili tuelewane.

Katika hotuba hii ya Waziri Mkuu, kama itatokea hawa waliokuwa wameomba wameshazungumza, kuna wengine muda upo, basi tunaanza na wale walioongea zamani kwenye bajeti na tutalieleza hilo kwamba, umezungumza mara moja na unapewa ya pili. Mpaka waishe hawa kwanza, ambao hawakuongea na wameomba. Naomba tuelewane hivyo na baadae hivyo hivyo, atakayekuwa amezungumza mara mbili, tutampa yule aliyezungumza mara moja, ama hakuzungumza kabisa. Kwa hiyo, uataratibu tunao. Hakuna kusema ufanye maarifa. Hakuna maarifa hapa. Ni utaratibu tu unaofanyika. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana kwa siku ya leo, kwa kazi nzuri tuliyofanya. Ninaomba niahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi na atakaye kuwa kwenye Kiti asubuhi ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai. *(Makofi)*

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano Tarehe 28 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*